Nipashe
Jumanne Juni 4, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579935
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Mama wa mapacha aliyeachwa na mume alamba 'bingo' milioni 32/-

UKURASA 3





Nipashe
TESA
JE WAJUA
Jumanne Juni 4, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI
Ukurasa 17
JIELIMISHE
Usafi ndio adui wa Kipindupindu
Ukurasa 18
Wanasayansi watengeneza ukungu unaoua 99% ya mbu wa malaria
RAIS MPYA CHUO KIKUU MUHIMBILI:
Kuingiza siasa kunakwamisha tija sekta ya afya nchini
Ukurasa 16

UKURASA 13

# Tril. 9.7/- kutumika kulipa deni la taifa

UKURASA 2



Rais John Magufuli akiwa katika mazungumzo na Askofu Mkuu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Zitto ahoji biashara kufungwa

UKURASA 2

## Ahukumiwa kunyongwa mauaji ya mwanafunzi

**NI** ya mwanafunzi wa Scholastica, wengine miaka minne jela kila mmoja kwa kufanikisha mipango ... *Endelea ukurasa wa 2*

**MICHEZO** YANGA YAIGARAGAZA SIMBA USAJILI NYOTA UK. 32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Zitto aibana serikali kufungwa biashara

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), ameitaka serikali kuchukua hatua kutatua changamoto zinazosababisha kampuni nyingi kupunguza wafanyakazi.

Pia amemwomba Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuunda timu ambayo itafanya kazi ya ukaguzi wa deni la taifa, akieleza kuwa takwimu zinazotolewa hivi sasa si sahihi.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana alipochangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha.

"Tusijidanganye wenye mitaji kwamba wanalipa kodi kubwa. Angalieni takwimu za serikali, theluthi mbili ya makusanyo ya kodi ya mapato ni kodi ya wafanyakazi. Kwa hiyo ni lazima mjenge ajira, watu wapate kazi," alisema.

Alisema nchi kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya kampuni nyingi kufunga biashara huku zingine zikipunguza wafanyakazi.

Alibainisha kuwa katika wiki mbili zilizopita, kampuni mbili zinazojihusisha na habari, zimepunguza zaidi ya wafanyakazi 400 huku moja ikibaki na wafanyakazi 43 kati ya zaidi ya 300 iliokuwa nao.

Zitto pia alisema kampuni kubwa iliyokuwa inanunua tumbaku nchini imelazimika kufunga biashara na kusababisha

INAENDELEA UK. 8

# Tril 9.7/- kulipa deni la taifa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango, inatarajia kutumia Sh. trilioni 11.943 katika bajeti yake ya mwaka ujao wa fedha, huku Sh. trilioni 9.73 zikitengwa kwa ajili ya deni la taifa.

Akiwasilisha hotuba bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliliomba kuidhinisha Sh. trilioni 11.943 kwa wizara hiyo.

Alibainisha kuwa kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 11.21 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 730 ni za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Dk. Mpango alisema Fungu 22 (deni la taifa) lililoko chini ya wizara yake, wanaomba kuidhinishiwa Sh. trilioni 9.73 kwa ajili ya kulipa deni hilo.

Alibainisha kuwa kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 8.88 ni mishahara wakati Sh. trilioni 9.72 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Dk. Mpango alilieleza Bunge kuwa katika mwaka wa fedha 2018/19, wizara iliendelea kusimamia deni la serikali na kuhakikisha linaendelea kuwa himilivu.

Alisema wizara ilipanga kuendelea kuratibu ukopaji kwa kutoa kipaumbele kwenye mikopo yenye masharti nafuu na kuhakikisha mikopo yenye masharti ya kibiashara inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo inayochochea ukuaji wa uchumi.

Baadhi ya miradi inayochochea ukuaji wa uchumi, alisema ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari na mitambo ya kufua umeme.

"Hadi kufikia Aprili, mwaka huu, deni la serikali liliongezeka na kufikia Sh. trilioni 51.03 kutoka Sh. trilioni 49.86 Aprili, mwaka jana. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 2.35, alibainisha.

Alifafanua kuwa kati ya Sh. trilioni 51.03, deni la nje lilikuwa Sh. trilioni 37.78 na kwamba ongezeko la deni la serikali linatokana na kupokewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia

INAENDELEA UK. 26



Msongamano wa wakazi wa jiji, wakifanya manunuzi katika Mtaa wa Kongo, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya maandalizi ya Sikukuu ya Eid El Fitr. **PICHA: JOHN BADI**

**PROTINS REVIEW CLASSES CENTRE**
**P.O.BOX 79696, Dar es Salaam**
**Tel: +255 737 732 57, 1 Mob: +255 759 099 099, +255 654 555000**
**Email: previewcentre@yahoo.com**

**TANGAZO**

Protins Review Centre inatangaza nafasi za kusoma kwa program zifutazo:

- √ Elimu ya secondary kwa miaka miwili (QT) kwa masomo yote
- √ Tuition Sessions kwa wanafunzi wa ordinary Secondary level na Advanced Secondary level
- √ Elimu ya Advanced level kwa mwaka mmoja – michepuo yote.
- √ Kozi za kiingereza levels zote:
  - o **Beginners**
  - o **Intermediate**
  - o **Advanced.**

***Madarasa yenye viyoyozi kwa jili ya kuwezesha mazingira mazuri na ya kuvutia kujifunza.***

**TUPO:** MTAA WA LUMUMBA, Jengo la Furniture Centre, Mnazi mmoja, Ghorofa ya pili.

**WAHI MAPEMA NAFASI NI CHACHE.**

215257902

# Kunyongwa hadi kufa kisa mauaji Scolastica

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi, imemhukumu kunyongwa hadi kufa mshtakiwa wa kwanza wa kesi ya mauaji ya kukusudia ya mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari ya Scholastica, Humphrey Makundi (16) (pichani).

Aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa ni mlinzi wa shule hiyo, Hamisi Chacha, mshtakiwa wa pili na watatu kila mmoja akihukumiwa kutumikia adhabu ya miaka minne jela kwa kosa la kushiriki jinai baada ya mauaji hayo.

Akisoma Hukumu hiyo jana, Jaji Firmin Matogolo, alisema mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ametiwa hatiani kwa kosa la kuua kwa kukusudia kinyume cha kifungu namba 196 cha Kanuni ya Adhabu cha Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2002.

Jaji Matogoro alisema maelezo ya ungamo yaliyotolewa na mshitakiwa huyo mbele ya mlinzi wa amani yanatosha kumtia hatiani.

Alisema kuwa, ushahidi wa mshtakiwa huyo alioutoa mahakamani hapo kuwa kabla ya kutoa maelezo hayo ya ungamo aliteshwa na Jeshi la Polisi ili kukiri maelezo hayo inaonyesha ni uongo kwa sababu hakueleza kwa mlinzi huyo wa amani.

Jaji huyo alisema kuwa mateso na maumivu aliyoyasema ameyapata ambapo malidai kuchonywa na pasi katika paja lake pamoja na kuingiziwa chupa sehemu yake ya haja kubwa hukuweza kulalamika kwa Hakimu

aliposomewa maelezo ya awali na wala majeraha hayo yasingeweza kupona kwa haraka na alipopelekwa magereza asingepokelewa kabla ya kupelekwa hospitali.

Aliendelea kueleza kuwa ushahidi wa mshtakiwa huyo wa kwanza kwenda kuonyesha silaha ambayo ni panga alilotumia kuuwa unatosha kumtia lhatiani pia katika kosa hilo la kutenda mauaji kwa kukusudia.

Akisoma adhabu kwa mshtakiwa huyo wa kwanza, Jaji Matogolo alisema kosa hilo la kuua kwa kukusudia lina adhabu moja ya kunyongwa hadi kufa, kwa kuwa ni kinyume cha kifungu namba 167 ya Kanuni ya Adhabu cha Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2002.

Kwa upande wa mshtakiwa wa pili ambaye ni mmiliki wa Shule ya Scolastica, Edward Shao pamoja na mshtakiwa wa tatu ambaye ni mwalimu wa nidhamu, wao walishiriki katika kuutupa mwili wa marehemu Humphrey Makundi mtoni, lakini hakuna ushahidi unaoonyesha wameshiriki kufanya mauaji.

"Hakuna ushahidi ulioletwa mahakamani hapa na upande wa mashitaka kuonyesha mshtakiwa wa pili na tatu walishiriki kuuwa

INAENDELEA UK. 26

# Mama wa mapacha wanne aliyetelekezwa alamba mil. 32/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wamemchangia zaidi ya Sh. milioni 32, mkazi wa Kinondoni jijini Dar es Salaam, Radhia Solomon, aliyejifungua mapacha wanne, lakini akatekelezwa na mume.

Fedha hizo zimetokana na wabunge wanaume 248 kukatwa Sh. 100,000, huku wanawake 145 wakikatwa Sh. 50,000 na kupata kiasi cha Sh. 32,050,000.

Mama huyo alitinga jana bungeni akiwa na watoto wake akisaidiwa na mama yake mzazi, mama yake mkubwa na Afisa ustawi wa jamii.

Akitambulisha wageni baada ya kipindi cha maswali na majibu, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimtambulisha Radhia na kueleza kuwa baada ya kujifungua mumewe alimkimbia kukwepa kuwajibika.

"Naomba nimtambulishe kwenu Radhia Solomon, ambaye alijifungua watoto wanne kwa uzazi mmoja, lakini bahati mbaya mwanaume wake alikimbia majukumu, baada ya kupata watoto wanne ilimhitaji kupata usaidizi na kutokana na maisha ya Dar es Salaam ni ngumu kidogo," alisema Spika Ndugai.

Ndugai alisema mama huyo anasaidiwa kulea watoto na mama yake mzazi, mama yake mkubwa na Afisa ustawi wa jamii.

"Kwa hiyo ndugu zangu amekuja hapa ili sisi kama Bunge tukemee wanaume ambao hawawajibiki, lakini pia kama kawaida tumsaidie," alisema.

Kabla ya kufikia muafaka wa kumchangia, Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rukia Ahmed Kassim, alisema kwa sababu wanaume wamezoea kutelekeza watoto, anapendekeza wabunge wanawake wachangie Sh. 50,000 na wanaume wachangie Sh. 100,000, hoja iliyoungwa mkono na Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Susan Lyimo.

Hata hivyo, Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma alipendekeza wabunge wakatwe posho ya siku nzima ili wamsaidie mama huyo. Akihitimisha hoja, Spika Ndugai alisema wabunge wamekubaliana kuchanga fedha hizo ambapo wabunge wanawake watatoa Sh. 50,000 huku wanaume Sh. 100,000. "Kwa hiyo kupitia mbunge wenu tutawasiliana jinsi ya kupata mchango huu,"alisema.

Januari 8, mwaka huu Radhia alijifungua pacha hao wanne katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

## Raia wa Sweden chupuchupu jela

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imemhukumu Mkurugenzi wa Kampuni ya Biabana, Anna Kristina Edler (54) na mume wake, Anders Svensson (58) kulipa faini ya Sh. milioni 20 au kwenda jela mwaka mmoja na nusu.

Hata hivyo, washtakiwa walifanikiwa kulipa faini hiyo.

Hukumu hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, baada ya kukiri kuajiri raia wa nje ya nchi na kujihusisha na kazi bila kuwa na kibali nchini.

Washtakiwa hao ambao pia ni raia wa Sweden wanakabiliwa na mashtaka mawili, ikiwamo kufanya kazi nchini bila kuwa na kibali.

Hakimu alisema kwa kuwa washtakiwa wamekiri makosa yao, mahakama yake inawatia hatiani.

"Mahakama hii inawatia hatiani na inawahukumu kulipa faini ya Sh. milioni 20 au kwenda jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja na nusu., alisema Hakimu Shaidi.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali, Daisy Makakala, alidai kati ya Agosti 18, mwaka jana na Aprili 3, mwaka huu, eneo la Mikocheni, mshtakiwa Elder, akiwa mkurugenzi wa kampuni ya Biabana Ltd, alimwajiri Anders na kufanya kazi katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na kibali kutoka Idara ya Uhamiaji.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa siku na eneo la tukio la kwanza mshtakiwa Enders alijihusisha na kazi kama mwajiriwa wa kampuni ya Biabana LTD bila kuwa na kibali kinachotolewa na Uhamiaji.

NMB
Karibu yako
Unaweza KUPOTEZEA
hili tangazo...
Smart money.
Smart choice
www.nmbbank.co.tz

# Wakunwa utekelezaji katazo mifuko plastiki

**Na Mary Geofrey**

ZOEZI la utekelezaji wa katazo la matumizi, usambazaji na utengenezaji wa mifuko ya plastiki limefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na ushirikano mkubwa ulioonyeshwa na Watanzania katika kutekeleza katazo hilo la serikali.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi wameeleza kuridhishwa na uamuzi wa serikali wa kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo imekuwa ikichangia uchafu na uharibifu wa mazingira.

"Ninaunga mkono juhudi ya serikali katika kulinda mazingira kwa kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki na nitaendelea kuhamasisha wananchi wenzangu katika umuhimu wa zoezi zima, ili kusiwe na shuruti katika kutekeleza agizo la serikali," alisema mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, John Mwakikuti.

Alisema maeneo mengi ya nchini yamekuwa yakiathirika kutokana na matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo imekuwa ikileta taswira mbaya ya mazingira kwa namna inavyozagaa hasa katika maeneo ya fukwe na kuleta athari za kimazingira.

Mwakikuti pia alitoa wito kwa Watanzania kutumia mifuko mbadala ambayo ni rafiki kwa mazingira na pia kutumia katazo hilo la serikali kuwa wabunifu wa kutengeneza mbadala wa mifuko ya plastiki na kuwa sehemu ya kuingiza kipato.

Hatua ya utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki imepongezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, kwa kusema mbali ya utekelezaji wa agizo hilo, NEMC itaendelea kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya mifuko mbadala na umuhimu wa utunzaji mazingira.

"Tayari maofisa wa NEMC wapo maeneo mbalimbali ya nchi katika kuhakikisha katazo la serikali linatekelezeka kwa vitendo na ushirikiano umekuwa mkubwa kutoka kwa wadau wa mazingira katika kutoa elimu na kuhamasisha jamii kutumia mifuko mbadala," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema NEMC imejipanga kuhakikisha elimu ya

INAENDELEA UK.8



Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Kambarage, jijini Dodoma, Suzan Mkenda (kulia), akimkabidhi zawadi za vitu mbalimbali vikiwemo vyakula kwa Aisha Abdi kwaajili ya watoto yatima wa Kituo cha Rahma, wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo juzi. **PICHA: NMB**

# Utaratibu mpya maduka kubadilishia fedha waja

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imelieleza Bunge sababu za kuyafunga maduka ya kubadilishia fedha katika majiji ya Dar es Salaam na Arusha, huku ikibainisha kuwa inaandaa utaratibu mpya kwa ajili ya uendeshaji wa maduka hayo.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana hotuba kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema serikali iliamua kuchukua hatua dhidi ya maduka hayo baada ya kubaini yanaendeshwa bila kufuata sheria.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu, wizara kupitia Benki Kuu (BoT) ilifanya ukaguzi wa maduka hayo katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya jukumu lake la msingi katika kusimamia sekta ya fedha.

Alisema katika ukaguzi huo ilibainika maduka mengi ya kubadilishia fedha yanaendesha shughuli zake bila kuzingatia sheria na kanuni za kubadilishia fedha za mwaka 1992 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017.

Alibainisha kuwa upungufu uliobainika ni pamoja na uondoshwaji katika mfumo rasmi wa fedha na kuelekezwa kwenye mifumo ya utakatishaji fedha haramu.

Dk. Mpango alisema dosari nyingine iliyobainika ni maduka kutumika kupokea amana kutoka kwa wafanyabiashara kinyume cha leseni za biashara husika, kudhoofisha thamani ya shilingi na kuathiri usalama wa nchi kwa ujumla.

"Hata hivyo, BoT ilichukua tahadhari ya kutosha kuhakikisha huduma ya ubadilishaji fedha za kigeni inaendelea nchini kwa huduma hiyo kutolewa na benki zote pamoja na Shirika la Posta," alisema.

Waziri Mpango alisema serikali imeandaa kanuni mpya kwa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni ambazo zitaelekeza jinsi ya kuomba leseni za uendeshwaji maduka hayo kwa mtu binafsi au taasisi yoyote kwa masharti ya kuzingatia shughuli hizo.

INAENDELEA UK.8

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
3-06-2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano **tarehe 5/6/2019** kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SONGEA** Ngaka Coal Mining kuelekea **KILOMBERO**. Gari hilo lenye namba za usajili:

**T 116 DCG / T 901 CZT**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **19.50** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.70** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.60** |

2. Njia itakayotumika: **SONGEA Ngaka Coal Mining mpaka KILOMBERO kupitia IRINGA,** Gari litasafiri muda wa mchana tu (***kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215258802

# Spika azuia hotuba upinzani kisa Mdee

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amezuia kusomwa bungeni kwa hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka ujao wa fedha kwa madai ya kuandaliwa na 'mtu' aliyeko nje, huku ikiwa na lugha ya kuudhi.

Mara tu baada ya Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mashimba Ndaki, kuwasilisha maoni ya kamati hiyo, Spika Ndugai alisimama bungeni jana na kueleza kuwa upinzani hautawasilisha taarifa yake kutokana na kuwa na makosa mengi ikiwamo lugha ya kuudhi.

"Haitakuwa hivyo kwa sababu ya makosa yao, sijui kama kuna haja, mtaona jinsi ilivyo, sijui kwa nini wanafanya hivyo, mkiacha huko ndani, lugha mnazotumia ni masikitiko makubwa.

Vitabu hivi vinakaa muda mrefu, wanakuja vitukuu vyetu kufanya 'reference'(rejea). Huu ni ushauri wa bure tu," alisema.

Spika Ndugai pia alisema hotuba ya kambi hiyo iliyotarajiwa kusomwa bungeni jana na Naibu Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, David Silinde, iliandaliwa na mtu ambaye alikuwa nje ya Bunge.

Haiwezekani Bunge limekuweka pembeni halafu wewe unapitisha kwa mlango wa nyuma, unakuja tu kuweka," Spika Ndugai alisema, akimaanisha hotuba hiyo imeandaliwa na Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, Halima Mdee, ambaye amefungiwa kushiriki shughuli za Bunge.

Mdee ambaye pia ni Mbunge wa Kawe (Chadema), alifungiwa kushiriki mikutano mitatu ya Bunge kuanzia mkutano huu wa Bunge la Bajeti kutokana na kupatikana na hatia ya utovu wa nidhamu alipounga mkono kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kwamba anafikiri "huo ni udhaifu wa Bunge".

Kitabu cha hotuba ya upinzani iliyowasilishwa bungeni kisha kuzuiwa kusomwa na Spika jana, ilikuwa na kichwa kilichosomeka "Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb), kuhusu bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/20".

# Bil. 2.7/- kuboresha mazingira ya biashara

Na Romana Mallya

TRADEMARK East Africa (TMEA) pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), zimetiliana saini mkataba wa makubaliano wa Sh. milioni 2.7 kwa ajili ya kusaidia majadiliano ya pamoja kati ya sekta binafsi na serikali kwenye maeneo ambayo yataweka mazingira mazuri ya kibiashara na kuvutia uwekezaji zaidi.

Mkataba huo ulisainiwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkaazi wa TMEA Tanzania, John Ulanga na Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, ambapo utekelezaji wake ni wa miaka mitatu kuanzia sasa na utaisha Juni, 2022.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Ulanga alisema fedha hizo zina lengo la kusaidia majadiliano ya pamoja baina ya sekta binafsi na ya umma kwenye maeneo maalum ambayo ni miundombinu ya kibiashara, sera za kibiashara, usafirishaji, kodi, ushuru wa forodha, viwango na athari za viwango vya vyakula.

"Lengo ni kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji zaidi Tanzania... tunataka sekta hizi ziweze kukaa kwa pamoja ili kuangalia maeneo ambayo watayaboresha zaidi," alisema.

Alisema pande zote mbili zikifanya kazi kwa ushirikiano, mafanikio makubwa yatapatikana na gharama za kufanya biashara zitapungua na kuifanya nchi kuwavutia wawekezaji.

"TradeMark inaamini umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali kuwa utawezesha mazungumzo yenye kuleta tija kwa nchi hii."

Alisema kulingana na geografia ya nchi, Tanzania ina faida kubwa kwa nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Naye, Simbeye aliishukuru TMEA kwa kuendelea kusaidia maendeleo ya sekta binafsi nchini kukua.

"Kusainiwa kwa mkataba huu leo kati ya sekta binafsi na TMEA ni moja ya mafanikio makubwa. Mradi huu unakwenda kujenga misingi ya awali ya majadiliano ambayo yanawezeshwa na TMEA na tayari wadau 13 wamehusishwa na taratibu za majadiliano ngazi ya kitaifa," alisema.

Alisema kati ya mwaka 2014 hadi 2017 TMEA walitoa ruzuku ya dola za Marekani 600,000 (sawa na Sh. bilioni 1.4) kwa TPSF kuiwezesha sekta binafsi kuwa na nafasi kwenye masuala ya sera ya Afrika Mashariki. "Hii inaonyesha kwamba TMEA imejitoa kuboresha sekta binafsi kwenye nchi na ni mdau kwenye ajenda za kibiashara nchini," alisema.

## Exim yawa mdau uchangiaji damu

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Exim Tanzania pamoja na Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS) wameingia kwenye makubaliano ya utekelezaji wa pamoja wa uchangiaji wa damu utakaohusisha matawi yote ya benki hiyo nchini.

Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa benki hiyo ya uwajibikaji kwa jamii unaofahamika kama 'Exim Cares' Ushirikino huo ulizinduliwa rasmi jana katika tukio la uchangiaji wa damu lililoandaliwa na benki hiyo kwenye tawi lake katika Manispaa ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro ikiwa ni urasimishaji wa jitihada za benki hiyo kwa kipindi cha miaka minane mfululizo katika uchangiaji wa damu nchini.

Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Staniley Kafu, alisema unaenda sambamba na kauli mbiu ya benki hiyo inayosema "Exim kazini leo kwa ajili ya kesho" na kwamba unalenga kuchangisha damu na kutoa elimu ya umuhimu wa kuchangia damu katika mpango wa taifa.

"Kampeni hii ni sehemu ya uthibitisho kuwa benki ya Exim iko makini kutafuta njia za ubunifu za kuhudumia wateja wake na muhimu zaidi, inajitolea kuhakikisha inashiriki kuleta mabadiliko chanya katika jamii," alisema Kafu.

Akizungumzia kuhusu makubaliano hayo na NBTS, Kafu, alisema benki hiyo itawezesha mpango na utekelezaji wa uchangiaji damu kwenye kambi nane (8) za

INAENDELEA UK.8

NMB
Karibu yako
Ila kama unataka mchongo
Smart money.
Smart choice
www.nmbbank.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Lugha za kuwanyanyapaa wenye ualbino ziepukwe

**KATI** ya mambo ambayo yanawatia simamzi wenzetu wenye ualbino na kuwakosesha amani ya kuishi kama watu wengine hapa duniani ni lugha zinazotumika kuwaita na vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa.

Mara kwa mara tumesikia kundi la watu wenye ualbino likifanyiwa vitendo hivyo vikiwamo vya kukatwa viungo vyao na kuuawa kwa sababu ya imani za kishirikina.

Vitendo hivyo vilishamiri sana mwanzoni mwa miaka ya 2006, 2007, 2008 mpaka 2015 na kufanya nchi kuingia doa ndani na nje kwenye jumuiya za kimataifa kutokana na baadhi ya Watanzania kufanya ukatili huo dhidi ya watu wenye ualbino.

Vitendo hivyo ni pamoja na kukatwa viungo, kuwaua, ufukuaji wa makaburi na mambo ya kishirikina.

Shirika la Under The Same Sun (UTSS), ambalo liliundwa nchini Canada mwaka 2008 na kusajiliwa kisheria hapa nchini mwaka 2009 kwa dhumuni la kuunga mkono juhudi za serikali katika kulinda na kutetea haki za kibinadamu za kundi hilo, linafanya juhudi za kuelimisha umma ili kuelewa chanzo cha ualbino, changamoto wanazokabiliana nazo, wajibu wa jamii katika kutatua changamoto hizo ili kuhakikisha usalama wa kila raia nchini.

Kupitia vyombo vya habari elimu inayotolewa na Shirika hilo itawafikia watu wengi zaidi na vitendo hivyo vinaweza kukomeshwa, na wenzetu wakaishi maisha ya amani kama wanavyoishi watu wengine.

Elimu kwa umma kuhusu ualbino inayotolewa na UTSS ni matokeo ya ugunduzi usio na shaka kwamba, Watanzania wengi hawana taarifa sahihi kuhusu ualbino na jamii nyingi zimejiundia imani potofu dhidi ya kundi hilo na hivyo kuliweka katika hatari ya kudhulumiwa haki zao.

Kazi kubwa ya wanahabari ni kuhakikisha wanatumia lugha sahihi wakati wa kuporipoti habari za kundi hilo ili hata jamii inaposoma, kusikilia au kuangalia kwenye vyombo hivyo inajifunza na kupata maneno sahihi ya kutamka, badala ya kutumia maneno ya kuudhi au ya kunyanyapaa.

Lugha isiyo sahihi kuwaita watu wa kundi hilo ni zeruzeru, albino, watu wenye ulemavu wa ngozi na maalbino.

UTSS imetoa lugha sahihi inayopaswa kuliita kundi hilo kuwa ni 'Watu wenye ualbino'.

Lugha zisizo sahihi zinapotumika kwa kundi fulani huonyesha unyanyapaa. Kwa mfano kumuita mtu kipofu, kiziwi, bubu au kiwete haipendezi na kumfanya mwenye ulemavu huo kujiona anatengwa kwenye jamii.

UTSS imeona umuhimu wa kutafuta fursa ya kufikisha elimu hii kupitia vyombo vya habari kupeleka kwa jamii kwasababu vyombo hivi ni kama mhimili wa nne wa dola. Vyombo vya habari vinapotoa ujumbe unakuwa umefikia takribani nchi nzima na kwa muda mfupi.

Vyombo vya habari kupitia kalamu zao vinaweza kuleta amani au kusababisha machafuko kama ujumbe hautafikishwa sahihi. Vyombo hivi vinaaminika na jamii na vinapotoa habari sahihi ni rahisi kwa Watanzania kujifunza kwa urahisi na uharaka.

Vyombo vya habari vina jukumu kubwa la kuheshimu na kutekeleza ombi la UTSS la kuhakikisha lugha potofu dhidi ya kundi hilo inaepukwa na kutumia lugha sahihi ili jamii nayo ielimike na kuacha kuita majina yanayonyanyapaa kundi hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Moses Ismail

# RC Makonda na wenzake watatue vizuizi vitambulisho vya Machinga

**MKUU** wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametangaza vita dhidi ya wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama 'Machinga' wanaofanyabiashara katika mkoa huo bila ya kuwa na vitambulisho vilivyotolewa kwa ajili yao maarufu kama vitambulisho vya wamachinga.

Makonda alisisitiza wiki iliyopita kuwa wafanyabiashara wasio na vitambulisho wachukue jitihada za kuvipata kufikia jana (Juni 3), vinginevyo hawataruhusiwa kufanya biashara zao pamoja na hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

Hii inatokana na kile kinachoonekana kupungua kwa kasi ya Wamachinga wanaojiandikisha ili kupatiwa vitambulisho hivyo, vinavyowapa uhuru wa kufanya biashara zao katika eneo lolote la nchi hii linaloruhusiwa.

Zoezi la kutoa vitambulisho hivyo kwa malipo ya Sh. 20,000 kwa kila kitambulisho, lilizinduliwa na Rais John Magufuli kwa kugawa jumla ya vitambulisho 670,000 kwa mikoa yote ya Tanzania Bara.

Kila mkoa ulipewa vitambulisho 25,000 ili viwafikie wajasiriamali wote wenye mitaji chini ya Sh. milioni 4 na hivyo kuongeza wigo wa kukusanya mapato ya serikali.

Mbali ya lengo hilo, vitambulisho hivyo pia vilitolewa kwa nia ya dhati kabisa ya Rais Magufuli ya kuona kuwa wafanyabiashara wote wadogo nchini wanafanya shughuli zao kwa uhuru na kwa hali ya kistaarabu kinyume na ile hali ya mikikimikiki ya kukimbizana na Mgambo.

Tofauti na mikoa mingine, Dar es Salaam ulipewa vitambulisho vingi zaidi, kiasi cha vitambulisho 175,000 kwa kuzingatia ukweli kuwa ndio mkoa wenye wamachinga wengi, ikilinganishwa na mikoa mingine.

Kinyume na matarajio ya serikali, si kwa Dar es Salaam tu, zoezi la 'ugawaji' vitambulisho hivyo linaonekana kusuasua na hilo limewafanya baadhi ya wakuu wa mikoa kubuni mbinu za kuhakikisha zoezi halikwami ndani ya himaya zao.

Iwapo kila mkuu wa mkoa atafanikiwa kugawa vitambulisho vyote 25,000, kwa malipo ya Sh. 20,000, atakuwa amewezesha serikali kuingiza jumla ya Sh. milioni 500, wakati mkoa wa Dar es Salaam ukitarajiwa kuingiza jumla ya Sh. bilioni 3.5 kwa vitambulisho vyake 175,000.

Ni ukweli kwa mujibu wa Muungwana kwamba wamachinga walio wengi hawajaweza kununua vitambulisho hivyo kutokana na sababu mbalimbali.

Kuna wanaolalamikia urasimu wa upatikanaji wa vitambulisho hivyo, wakati wakuu wa mikoa wakitaka kuhakikisha wamachinga wanapata vitambulisho.

Na ndiyo maana wakuu wengine wa mikoa wamefikia hatua ya kutaka kuviuza vitambulisho hivyo hata kwa kada zisizohusika, wakiwamo waandishi wa habari.

Hii ni ishara kuwa kuna tatizo katika utekelezaji wa zoezi hilo.

Muungwana anaona kuwa njia nyepesi ya kutatua kinachokwamisha kununuliwa kwa vitambulisho hivyo ni kwa pande zinazohusika, yaani serikali na wamachinga kukaa pamoja na kujadiliana.

Lengo likiwa kubaini changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi wenye tija.

Rais alipozindua mpango huo, Desemba 10 mwaka jana, ulionekana kupokewa kwa furaha na wamachinga wengi kwani ni suluhu ya 'dhahama' ya kushikana mashati baina yao na Mgambo na kuirasimisha sekta yao.

Ni maoni ya Muungwana kwamba kuwachukulia wamachinga kama watu wabishi wasiotaka kufuata utaratibu bila ya kusikiliza sababu wanazotoa juu ya tatizo hilo, kunaweza kusaidie upande wowote na hivyo kufisha lengo lililokusudiwa na Rais Magufuli.

Na ndiyo maana ninasema changamoto zinazojitokeza sasa zitafutiwe mbinu za kuziondoa, badala ya 'kutunishiana misuli.'

Ninasema hilo halitosaidia upande wowote na hasa kwa wamachinga ambao kabla ya kuingia kwa serikali ya awamu ya tano walikuwa kwenye mapambano ya 'kudumu' dhidi ya mamlaka zenye dhamana ya kusimamia sekta ya biashara.

Utulivu wa sasa unaoruhusu wamachinga kufanyabiashara zao kwa salama ni tunu kubwa kwa serikali ya awamu ya tano na unapaswa kulindwa kwa majadiliano na si kurudi tena katika zama za kutumia nguvu za Mgambo.

# Neema wananchi 2,017 kupisha bomba la mafuta

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WANANCHI 2,017 mkoani Kagera wanatarajiwa kupewa fidia ya ardhi na mali zilizopitiwa na bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) litakalotokea Hoima nchi Uganda kuingilia mkoani humo hadi Chogoleani mkoani Tanga.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati wa ufunguzi wa kongamano la wadau wa mradi wa bomba la mafuta mkoani Kagera lilifanyika mjini Bukoba.

Waziri Kalemani alisema wananchi waliotathiminiwa mali zao wakati wa utafiti wa upitishaji wa bomba hilo wataanza kupatiwa taarifa za tathmini wiki ijayo.

Alisema kuwa kata 20, vijiji 34 na vitongoji 117 katika wilaya za Missenyi, Muleba na Biharamulo ni maeneo ambayo yamepitiwa na yenye makazi na mali za wananchi.

Aidha, alisema kwa mikoa minane ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Manyara, Arusha, Singida, na Tanga wananchi 10,000 walifanyiwa tathmini ya kulipwa kiasi cha Sh. bilioni 50 kwani asilimia 80 za majadiliano ya Serikali ya Tanzania na Uganda yameshafikiwa.

Kwa mujibu wa Dk. Kalemani, bomba hilo litakuwa na urefu wa kilomita 1,445 kwa upande wa Tanzania kutokea Hioma nchini Uganda ikiwa kilomita 1,147 zitakuwa Uganda sawa na asilimia 20, ambapo litapita katika wilaya 24 na kata 134 kwenye mikoa hiyo.

"Nchi yetu tumepata bahati ya asilimia 80 zote zinapita kwenye mikoa yetu minane iliyotajwa kwa urefu wake wa kilomita 1445... ukiangalia Uganda wanakilomita 1,147 pekee," alisema Kalemani.

Alieleza mradi wa ujenzi wa bomba hilo utakuwa na vituo sita vyenye kusukuma mafuta ghafi, ambapo viwili vitakuwa upande wa Uganda na vinne Tanzania.

Kwa mkoa wa Kagera kimoja kitajengwa wilayani Mussenyi eneo la Kyaka, wakati mkoani Singida vitakuwa viwili na mkoani Tanga viwili vikiwa na kambi 12 za wafanyakazi, mbili zikiwa mkoani Kagera.

Aliongeza kuwa ujenzi wa mradi huo utaanza Septemba na utakamilika kwa muda wa miaka mitatu kwa gharama ya dola za Marekani bilioni 3.

## Polisi yafunguka kunaswa mtuhumiwa sugu 'Teleza'

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kigoma limetaja mmoja wa watuhumiwa sugu wa kikundi cha kihalifu maarufu kama 'Teleza' kinachofanya matukio mbalimbali ikiwamo kujeruhi na kubaka wanawake.

Aidha, Jeshi hilo limesema linatarajia kuwapeleka mahakamani watuhumiwa nane wa 'Teleza' kwa tuhuma mbalimbali za uhalifu.

Miongoni mwa tuhuma hizo ni kujeruhi wanawake sita na kuvunja nyumba mbalimbali katika maeneo ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Akizungumza na Nipashe jana Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Martin Otieno, alisema mtuhumiwa sungu ambaye alikuwa akitafutwa kwa muda mrefu Hussein Hamisi Rajabu (28) maarufu 'Orosho Teleza' mkazi wa Vamia Mwanga Manispaa ya Kigoma/Ujiji amekamatwa wilayani Kasulu.

Kamanda Otieno alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Mei 30, mwaka huu majira ya usiku eneo la Murusi karibu na stendi ya mabasi Wilaya ya Kasulu ambaye anakabiliwa na tuhuma za kujeruhi wanawake na kuvunja nyumba mbalimbali katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Alisema baada ya mtuhumiwa huyo kukamatwa wanawake sitawalifika katika Kituo cha Polisi Kati na kumtambua mtuhumiwa huyo

INAENDELEA UK. 8



# Exim yawa mdau uchangiaji damu

INATOKA UK. 5

uchangiaji damu katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Tanga, Mtwara na Zanzibar, huku ofisi ya Mpango wa Taifa Damu Salama wakisimamia masuala yote ya kitabibu katika mpango huo.

"Zaidi benki ya Exim kwa kushirikiana na wadau wote wa mpango huu wakiwamo Mpango wa Taifa Damu Salama, Wizara ya Afya na wadau wa habari tutahusika na kuratibu mikakati ya uelimishaji na uhamasishaji wa wananchi, ili waweze kujitokeza kwa wingi katika suala hili muhimu kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kuchangia Damu Duniani," alisema Kafu.

Menaja wa NBTS Kanda ya Kaskazini, Dk. Edson Mollel, alisema ofisi hiyo inahitaji kukusanya chupa (units) 526,000 za damu, ili kukidhi mahitaji ya kila mwaka kwa nchi nzima ambapo kiasi kilichopatikana mwaka jana ilikuwa ni chupa 307,835 sawa na asilimia 58 ya mahitaji.

"Mwaka huu lengo ni kukusanya chupa 357,000 za damu na kupitia maadhimisho ya mwaka huu pekee tumejipanga kukusanya chupa 41,920 na ndio maana tunaridhishwa sana wanapojitokeza wadau kama benki ya Exim, ili kutuunga mkono...uhitaji wa damu ni mkubwa." "Hatua hii ni mfano wa kuigwa kwa kuwa benki ya Exim na wafanyakazi wake wanakuwa sehemu ya jamii wanayoihudumia kwa ukaribu zaidi na pia wanathibitisha rasmi mioyo yao ya kujitolea kwa hali na mali kwa jamii wanayoihudumia," alisema. Benki ya Exim imeendelea kuonyesha uwajibikaji wake katika kusaidia sekta ya afya kupitia mipango mbalimbali na miradi ya kijamii. Katika miaka minane iliyopita, benki imechangia zaidi ya lita 100 za damu katika benki ya damu taifa.

# Zitto aibana serikali kufungwa biashara

INATOKA UK. 2

watu zaidi ya 3,000 kukosa ajira.

Kuhusu deni la taifa, Zitto alisema usimamizi wake ni tatizo kwa kuzingatia kilichoelezwa katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka miwili iliyopita.

Alisema kuna upotoshaji mkubwa kuhusu taarifa za deni hilo kwa kuwa mfumo wa malipo na mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za deni haiwiani.

"Matokeo yake ni kwamba tuna madeni ambayo hayapo 'recorded'. Kwa mfano, katika ripoti ya CAG ya mwaka jana, kuna madeni ya zaidi ya Sh. trilioni mbili ambayo kumbukumbu zake hazionekani.

"CAG amekwenda kwa watu waliolikopesha taifa wanasema kuna fedha ambazo wamezitoa lakini Hazina wanasema kuwa hawajazipata fedha hizo.

"Hii ni kwa sababu ya mfumo mbovu wa usimamizi. Kwa hiyo, hata deni tunaloambiwa na Waziri Mpango ni asilimia hii ya Pato la Taifa, sijui ya mauzo na kadhalika ni deni ambalo rekodi yake siyo sahihi," alisema.

Mbunge huyo amemwomba Spika kwa manufaa ya taifa, kwa mara ya kwanza aruhusu ukaguzi maalum wa Deni la Taifa ili kupata takwimu sahihi za deni hilo.

Aliongeza kuwa hata utunzaji wa kumbukumbu za deni hilo unafanyika kwa kutumia madaftari aina ya 'counter books' huku akihoji ufanisi wa aina hiyo ya utunzaji wa taarifa za serikali.

"Nakuomba Mheshimiwa Spika, uruhusu ukaguzi maalum ili kujua tunadaiwa nini na tunadaiwa na nani kwa sababu inawezekana kuna madeni hewa," alisema.

**WEZI WATATU**

Mbunge wa Nzega Mjini, Hussein Bashe (CCM), alihoji kuhusu serikali kutowakamata watu watatu wanaoingiza sukari kwa njia ya panya nchini.

"Kuna watu wanaingiza sukari za viwandani kwa njia ya panya, wanaiingiza sokoni, kwanini hawa wezi watatu tu wanaojulikana hawakatwi? Tunaenda kuharibu soko lote la sukari, Hili swali nimeliuliza kwa miaka miwili katika Kamati ya Bajeti lakini huwa sipati jibu.

"Tuaanzisha kodi za kwenda kuua viwanda vyetu, siyo 'fair' (haki), Waziri Mpango tunakubebesha dhambi nyingi, una mambo mengi, walazimishe polisi, walazimishe Wizara ya Mambo ya Ndani wachukue hatua sekta nzima inateketea. Hivi kweli Waziri Mpango Coca-Cola ataingiza Industrial Sugar, aipeleke Kariakoo akauze?" Bashe alihoji.

Akichangia mjadala huo, Mbunge wa Mombo, David Silinde (Chadema), alisema hafurahishwi na kile alichokiita propaganda zinazofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango.

"Mioyoni mwetu haturidhiki jinsi Wizara ya Fedha inavyofanya kazi, uchumi hauendeshwi kwa propaganda, nasema hivi; Dk. Mpango yule wa Tume ya Mipango na huyu wa Wizara ya Fedha ni watu wawili tofauti kabisa. Wizara inafanya mambo bila ya ruhusa ya Bunge.

"Angalieni hawa wataalamu ndiyo wanatumika kuvuruga utaratibu, sera yetu ni ya viwanda katika bajeti imekuwa ni lawama juu ya lawama," alisema.

Mbunge huyo aliishauri wizara hiyo kuwekeza kwenye sekta binafsi badala ya kujikita kwenye kukusanya kodi tu na kuangalia mazingira ya kibiashara kwa kuwa ya sasa si rafiki kwa wafanyabiashara.

Mbunge wa Tanga Mjini, Musa Mbaruk (CUF), alitaka serikali kuwasaidia wafanyabiashara katika biashara zao kutokana na mfumuko wa bei.

"Tuwasaidie wafanyabiashara, mfumuko wa bei upo juu. Mwaka jana, tambi ilikuwa Sh. 1,800 leo ipo juu Sh. 2,000, mwananchi wa kawaida unapomwambia mfumo wa bei umepungua, hakuelewi, tunasema uchumi umekuaa, hapana," alisema.

# Polisi yafunguka kunaswa mtuhumiwa sugu 'Teleza'

INATOKA UK. 7

wakati wa gwaride la utambuzi.

Alisema watuhumiwa nane wanashikiliwa na Jeshi la Polisi baada ya kukamatwa katika oparesheni ya kuwasaka, na kwamba wanatarajia kuwapeleka mahakamani kwa makosa ya kujeruhi na shambulio la kudhulu mwili.

Aidha Kamanda Otieno aliwataka wanawake sita ambao ni walalamikaji katika kesi hiyo waliojitokeza kumtambua mtuhumiwa huyo waendelee na msimamo huo kwa kufika mahakamani kutoa ushahidi.

Alisema oparesheni ya kuwatafuta wahalifu pamoja na majambazi itakuwa endelevu katika maeneo yote ya Mkoa wa Kigoma ili kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani. Aidha Kamanda Otieno alisema ametoa majina ya mtuhumiwa mmoja sugu peke yake, huku majina ya watuhumiwa wengine saba yamehifadhiwa kwa taratibu za upelelezi unaoendelea wa kuwabaini wote wanaojeruhi wanawake.

Alisema watuhumiwa hao wanatuhumiwa kwa makosa ya kujeruhi wanawake na kuvunja nyumba.

Hata hivyo, alisema kati ya wanawake waliojitokeza polisi, hakuna aliyedai kubakwa.

Kumekuwapo na malalamiko kuwa wahalifu wa kikundi cha 'teleza' pamoja na vitendo vingine vya kihalifu wanabaka wanawake kisha kutokomea bila kukamatwa kutokana na kujipata mafuta yanayoteleza.

# Wakunwa utekelezaji katazo mifuko plastiki

INATOKA UK. 4

matumizi sahihi ya mifuko mbadala na umuhimu wa utunzaji wa mazingira inawafikiwa Watanzania na kuwafanya watekeleze agizo la serikali pasipo kushurutishwa au serikali kutumia nguvu.

"Jukumu la kutunza mazingira ni la kila mwananchi sisi ni wasimamizi tu wa sheria zilizowekwa, hivyo ni lazima tushirikiane kuhakikisha mazingira yanabaki kuwa salama ili vizazi vijavyo viendelee kukuta mazingira yapo salama," alisema.

Dk. Gwamaka pia aliwashukuru wadau mbalimbali hasa vyombo vya habari katika kufanikisha katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki linatekelezeka kwa kuhakikisha taarifa zinawafikia wananchi wote katika njia tofauti lengo likiwa ujumbe ufike na utekelezaji ufanyike.

Nao waratibu wa baraza kutoka kanda mbalimbali za NEMC nchini walishukuru zoezi hilo kufanikiwa katika maeneo mengi nchini bila kupata kipingamizi chochote kutoka kwa wananchi kutokana na elimu na uhamasisha mkubwa uliofanywa na serikali kwa kushirikana na wadau.

"Mifuko ya plastiki imekuwa kero kwa wananchi wengi kutokana na uhalisia kwamba mifuko ya plastiki haiozi mara baada ya kuitumia hivyo mbadala wa mifuko hii unakwenda kuondoa tatizo hilo ambalo limekuwa likiathiri mazingira," alisema moja ya waratibu wa NEMC Kanda ya Kusini.

# Utaratibu mpya maduka kubadilishia fedha waja

INATOKA UK. 4

Alisema shughuli hizo zinalenga kuweka mazingira mazuri ya biashara ambayo hayatatoa athari kwa sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla.

Dk. Mpango alisema matarajio ya serikali ni kwamba udhibiti huo utaziwezesha benki za biashara na taasisi zingine kuuza fedha za kigeni kwenye soko la fedha na hatimaye kuongeza akiba ya fedha za kigeni.

Alisema serikali inatoa tahadhari kwa wananchi kutoshiriki kwenye biashara ya kubadilisha fedha za kigeni kwa njia zisizo sahihi.

MISAADA NA MIKOPO

Waziri Mpango alisema katika mwaka huu wa fedha, wizara yake ilipanga kuratibu upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu ya kiasi cha Sh. trilioni 2.67 kutoka kwa washirika wa maendeleo ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alibainisha kuwa hadi Aprili, mwaka huu, misaada na mikopo ilifikia Sh. trilioni 1.7, sawa na asilimia 86 ya lengo la kipindi hicho.

Dk. Mpango pia alilieleza Bunge kuwa katika mwaka huu wa fedha, wizara hiyo pia huratibu upatikanaji wa mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara na jumla ya Sh. trilioni 8.9. Kati yake, Sh. trilioni 3.11 ni mikopo ya nje, Sh. trilioni 1.19 ni mikopo ya ndani na Sh. trilioni 4.6 ni mikopo ya ndani ya kulipia hatifungani zilizoiva.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Aprili mwaka huu, Sh. bilioni 692.3 zilikopwa kutoka nje, Sh. trilioni 3.3 zilikopwa kutoka soko la ndani zikijumuisha malipo ya dhamana za serikali zilizoiva.

## TANGAZO




absa
It takes a solid foundation to make it to the Top 40 Index on Africa's leading stock exchange.
Whether it's taking your business places, growing your wealth or building a legacy, we are a well-capitalised organisation with the global reach to help get you there.
As one of the largest companies listed on the Top 40 Index on the Johannesburg Stock Exchange, we have a market capitalisation of over US$12 billion (as at 31 December 2017), and a balance sheet of over US$97 billion in assets, enabling us to deliver the best solutions for our varied client portfolio.
www.absa.africa
Absa Group, proudly serving you as Barclays in Tanzania.
BARCLAYS
© Absa Group Limited Reg No 1986/003934/06. All rights reserved
215246601

# Mbunge ahoji uhaba wa walimu mkoani Dodoma

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Felister Bura, amehoji mpango wa serikali wa kuajiri walimu wa kutosha katika mkoa wa Dodoma kutokana na kuwa na upungufu wa watumishi wa kada hiyo kwa asilimia 38.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema mkoa huo una mahitaji ya walimu 11,676 kwa uwiano wa 1:40 kwa shule za msingi, lakini kwa sasa waliopo ni 7,382, hivyo kuwa na upungufu wa walimu 4,410 sawa na asilimia 38.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema serikali imekuwa ikiajiri na kuwapanga walimu kwenye halmashauri kwa awamu.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19 serikali imeajiri walimu 14,422 kati ya hao 10,695 ni wa shule za msingi na 3,727 ni wa shule za sekondari," alisema.

Waitara alisema mkoa huo umepatiwa walimu 699 wa shule za msingi kati ya walimu 10,695 walioajiriwa.

"Serikali itaendelea kuajiri walimu kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha," alisema.

# Ujenzi reli SGR wakaribia asilimia 50

BUNGE limeelezwa kuwa ujenzi wa reli ya kati ya kisasa (SGR) awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro urefu wa kilometa 300 umefikia asilimia 47.87, kwa mujibu wa taarifa ya Machi, mwaka huu.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, wakati akijibu swali la Mbunge wa Msalala (CCM), Ezekiel Maige.

Katika swali lake, Maige alisema Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 imeielekeza serikali kujenga upya reli hiyo na Rais tayari ameshapata fedha za mkopo kutoka serikali ya China kwa ajili ya utekelezaji huo.

"Je, utekelezaji wa ahadi hiyo ya CCM na Rais John Magufuli kwa mradi huu umefikia hatua gani? Na kwa kuwa Isaka ni eneo la makutano ya Reli ya Tabora-Mwanza na reli mpya kati ya Isaka hadi Kenza na hatimaye Kigali-Rwanda, je, serikali iko tayari kuifanya Isaka kuwa ndiyo karakana kuu?" Alihoji.

Pia alihoji serikali imejipangaje kuwasaidia wananchi waishio jirani na mradi huo, ili wanufaike kiuchumi wakati wa ujenzi huo.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Nditiye alisema serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) inaendelea na ujenzi wa reli hiyo kwa awamu na kwamba awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza urefu wa kilometa 1,219.

Alifafanua kuwa ujenzi huo ni kutoka Tabora hadi Kigoma urefu wa kilometa 411, Kaliua- Mpanda hadi Karema kilometa 320, Isaka hadi Rusumo kilometa 393 na Uvinza kuelekea Musongati kilometa 150.

"Hivi sasa ujenzi wa awamu ya kwanza utekelezaji wake umefikia asilimia 47.87 na ujenzi wa kipande cha pili kutoka Morogoro hadi Makutupora kilometa 422 umefikia asilimia 7.96 kwa mujibu wa taarifa ya Machi, mwaka huu," alisema.

Aidha, alisema mpango wa serikali ni kuendelea kuifanya Isaka kuwa Bandari Kavu kwa ajili ya kuhudumia shehena itakayobebwa na reli ya sasa (Meter Gauge) na pia ya kisasa SGR.

"Aidha, kwenye mradi wa ukarabati wa reli iliyopo kupitia mkopo wa Benki ya Dunia itahusisha na ujenzi wa kituo kikubwa cha kuhudumia shehena," alisema.

Hata hivyo alisema uamuzi wa kujenga au kutojenga karakana kuu Isaka utafanywa wakati wa kufanya usanifu wa misingi kutoka Makutupora - Mwanza.

"Kwa sasa, reli mpya inayojengwa kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora itakuwa na karakana kuu katika eneo la Kwala, Ruvu mkoani Pwani," alisema.

Pamoja na hayo, Nditiye alisema serikali inatambua umuhimu wa kuwasaidia wananchi waishio jirani na mradi kwa kupata manufaa na kwamba mradi huo unatarajiwa kutoa ajira kwa wazawa, kutumia malighafi za ndani kwa zile zinazopatikana nchini.



Meneja wa Data wa Benki ya Stanbic Tanzania, Ally Masoud (wa pili kushoto), akimkabidhi mwasisi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Watoto Wetu Tanzania, Evans Tegete, mfano wa hundi ya thamani ya Sh. milioni 20, ikiwa ni mwendelezo wa benki hiyo kusaidia ujenzi wa madarasa kwenye kituo hicho kilichopo Kijiji cha Mazizi Kata ya Msata mkoani Pwani hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atangaza neema kwa wakulima

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametangaza neema ya kuanza kununua mahindi nchini kutokana na kupata masoko makubwa kwenye nchi za kusini mwa Tanzania ambazo zinahitaji tani milioni moja.

Kutokana na hali hiyo, wiki hii Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) zitaanza kununua na kukusanya mahindi kutoka kwa wakulima.

Hasunga alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Aida Khenani, ambaye alihoji serikali imejipangaje mwaka huu katika ununuzi wa mahindi kwa kuwa hivi sasa ni msimu wa mavuno.

Akijibu swali hilo, Hasunga alikiri kuwa kwenye msimu uliopita kulikuwa na changamoto ya masoko ya zao hilo, lakini serikali imekuwa ikihakikisha inatafuta masoko. "Hivi sasa tumepata masoko makubwa ya mahindi nchi za kusini. Kwa sasa Rwanda wanahitaji zaidi ya tani 100,000, Burundi zaidi ya tani 100,000, Zimbabwe tani 800,000 za mahindi na nchi zingine nyingi zinahitaji kwa wingi," alisema.

Hasunga alisema hivi sasa soko la mahindi ni kubwa na kutoa wito kwa wakulima wa mahindi kujitokeza kueleza kiasi alicho nacho ili kushirikiana na serikali.

Aidha, alisema taasisi nyingine ambayo imepewa jukumu kupeleka mahindi nchini Zimbabwe itaanza kununua mahindi wiki hii.

Aliwataka wakulima kukaa mkao wa kula kwa kuwa hivi sasa ni wakati wa kula mkate mzuri.


Katika swali la msingi, Mbunge wa Namtumbo (CCM), Edward Ngonyani, alisema Mkoa wa Ruvuma umepata mnunuzi wa tumbaku ambaye amekubali kuwawezesha Chama cha Ushirika (Sonamcu) kufufua kiwanda cha kuchambua tumbaku na kugeuza 'green leaf' kuwa 'dry leaf'.

"Aidha, kutokana na changamoto za kodi na soko mnunuzi huyo hajatekeleza azma yake. Je, serikali inasaidiaje kutatua changamoto zinazomkabili mnunuzi huyo?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, alisema kutokana na kuondoka kwa kampuni mbili za ununuzi wa zao hilo mkoani humo mwaka 2014/15, wakulima walikosa soko la uhakika, hivyo serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali walifanya jitihada za kutatua changamoto hiyo.

Alisema jitihada hizo zilisaidia kupatikana kwa mnunuzi wa tumbaku ambaye ni kampuni ya Premium Active Tanzania Limited (PATL) ambayo ilianza kununua kilo 250,000 na sasa imeongeza hadi kilo 1, 000,000.

Kwa msingi huo, alisema Wizara ya Kilimo iko tayari kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na mwekezaji huyo kutafuta ufumbuzi wa changamoto ili kuhakikisha kampuni inatimiza azma hiyo.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA

# Wajasiriamali wataka mashine za mifuko

**Na Novatus Makunga,**
ARUSHA

WAJASIRIAMALI wadogo ambao kwa sasa wamejikita katika utengenezaji wamifuko ya karatasi, kutokana na zuio la mifuko ya plastiki mkoani Arusha, wameliomba Shirika la Viwanda Vidogo (Sido), kuanza mchakato wa kuwatafutia mashine ndogo zitakazopatikana kwa gharama nafuu.

Ombi hilo limetolewa jana katika mafunzo ya uboreshaji wa mifuko ya karatasi kwa mahitaji halisi ya soko iliyoandaliwa na shirika hilo katika Mkoa wa Arusha, baada ya serikali kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia Juni Mosi, mwaka huu.

Akizungumza katika mafunzo hayo, mmoja wa wajasiriamali hao, Neema Mollel, alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha

Watanzania wenyewe wanakamata soko la mifuko, badala ya kutegemea wageni kama ilivyokuwa kwa mifuko ya plastiki.

"Hatuhitaji tena kuanza kuagiza mifuko hii ya karatasi kutoka China na kwingineko kwani malighafi zote zinapatikana hapa nchini na nzuri zaidi hivi sasa Watanzania tunajitambua na ni vyema sisi wadogo na wenzetu wa kati na wakubwa, tukahakikishe tunakamata soko," alisema.

Mollel alisema kupitia aina mbalimbali ya mafunzo, wameanza uzalishaji wa kawaida kwa kutumia vifaa vidogo vinavyopatikana madukani na akatoa rai kwa Sido kuhakikisha inatafuta mashine kwa ajili ya wajasiriamali wadogo kuzalisha mifuko kwa ufanisi zaidi.

Naye Georgina Tenga, kutoka Kijiji cha Shangarai wilayani Arumeru, alisema kupitia upatikanaji wa fursa hiyo ya uzalishaji wa mifuko, lengo lake kubwa ni kumiliki kiwanda kikubwa na kuwa mfanyabiashara maarufu wa mifuko.

Aliungwa mkono na Mohammed Sadiq ambaye ni fundi ujenzi wa nyumba anayeishi eneo la Sokoni One katika Jiji la Arusha ambaye alisema mabadiliko ya matumizi ya mifuko ni fursa nzuri kwa Watanzania waliojipanga katika kujikwamua kutoka hali duni.

"Kama huko nyuma tulilala, huu si wakati tena wa kuzubaa. Tunachotakiwa ni kuchangamka. Bahati mbaya wenzetu wa jirani mara nyingi wamekuwa wepesi na wajanja katika kusoma ramani na kutumia fursa zetu kabla sisi hatujazinduka," alisema Sadiq.

Mkufunzi wa Masuala ya Biashara, Bahati Mpoki, aliwataka wajasiriamali hao kama wanataka kufanikiwa katika malengo yao, wahakikishe wanafanya kazi kwa ufanisi na kwa kujituma, mifuko wanayozalisha inakuwa bora na uzalishaji huo uwe kwa gharama ndogo.

"Hakuna asiyetumia mifuko katika shughuli zake za kila siku, hivyo hapa hakuna wasiwasi wa soko kama baadhi yenu mlivyoonyesha. Fursa hii imekuja na soko ambalo halihitaji kutumia nguvu kubwa," alibainisha Mpoki.

Naye mkufunzi wa uzalishaji, Lukindo Rodgers, alisema umakini unatakiwa katika kudhibiti upotevu wa malighafi hususani karatasi, katika ukataji kwa kuhakikisha wanakuwa na vipimo sahihi kutegemeana na kila hitaji la mfuko.

Meneja wa Sido Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, alisema tayari wameanza mchakato wa upatikanaji wa mashine za gharama nafuu kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wa uzalishaji wa mifuko mbadala.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Jackson Sipitieck, akizungumza na wadau wa maendeleo juzi, kuhusu miradi ya maendeleo inayofanyika kwenye wilaya hiyo. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wasifu NGO kudhibiti mila potofu

**Na Jaliwason Jasson,**
HANANG

WANANCHI wa Halmashauri ya Hanang mkoani Manyara, wamesema mashirika yasiyo ya kiserikali yana mchango mkubwa katika kudhibiti mila kandamizi kama vile ukeketaji na ukatili wa kijinsia.

Kauli hiyo waliitoa jana kwa nyakati tofauti walipozungumza na Nipashe namna wanavyoshirikiana na asasi za kiraia kukomesha mila potofu ambazo zimekuwa zikitawala maeneo mengi ya kifugaji.

Mkazi wa kijiji Cha Mureru, Felista Giyamu, alisema zamani ilikuwa shida kwa jamii ya wafugaji kuacha kuwakeketa watoto wa kike, lakini

Shirika la Ujamaa Community Resource Team (UCRT) walipofika wameibadilisha jamii hiyo kwa kuwaelimisha madhara ya ukeketaji na kusababisha wengi kubadilika.

Alisema shirika hilo limewasaidia wanawake kuanza kurithishwa mali kama ng'ombe na vitu vingine tofauti na zamani kwa kuwa hawakuruhusiwa kurithi chochote.

"Kiukweli ukeketaji unaendelea kupungua na watoto wa kike wameanza kuthaminiwa tofauti na zamani. Mtoto wa kiume akiota jino moja anaanza kugawiwa ng'ombe na ndugu zake," alisema Giyamu.

Alisema watoto wa kiume ndio walikuwa wanapelekwa shule na ndio walikuwa wanatibiwa wakiugua, lakini wa kike walikuwa hawapewi fursa za namna yoyote zaidi ya kuwaozesha.

Meruna Makuya, mkazi wa Kijiji cha Ming'enyi alisema UCRT wana mchango mkubwa kwa kuwa wamewasaidia kupinga mila kandamizi na kujua

matumizi bora ya ardhi na kubadili mitazamo hasi iliyokuwapo dhidi ya wanawake.

Aliongeza kuwa ilikuwa ngumu kwa wazee kuelewa kwa kuwa walikuwa wanawaambia kukeketwa wamerithi toka kwa bibi na babu zao, hivyo kuacha itakuwa ngumu.

Mkazi nwingine wa Kijiji cha Gasaboy, Andrew Hhaya, alikiri asasi hiyo kutokomeza ukeketaji, huku akidai wanaume waliwaweza kwa kuwaambia wanawake wakubali kuacha kukeketwa watawaoa maana wengine walikuwa na hofu ya kutokuolewa.

Mratibu Msaidizi wa UCRT, Albet Masuja, alisema kupitia ufadhili wanaoupata kutoka Shirika la Oxfam, wameibadilisha jamii ya

Wabarabaig iliyokuwa inawakeketa watoto wa kike. Masuja alifafanua kuwa wamewatetea wanawake na wakaanza kumiliki ardhi, akitolea mfano wa kuwamilikisha ardhi wajane 121.

Aliongeza kuwa wamewafundisha wanawake ujasiriamali, kilimo cha alizeti na kuingia kwenye vikoba ili waachane na kazi za ukeketaji.

# Madiwani waomba mafunzo ya maadili

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

BAADHI ya Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli mkoani hapa, wamesema kuna umuhimu kwa viongozi wa kuchaguliwa hususani madiwani, kupatiwa mafunzo ya maadili pindi wanapochaguliwa.

Wamesema hali hiyo itawajengea uwezo wa kufanya uamuzi wenye tija kwa ajili ya kuepuka mgongano wa kimaslahi.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Issac Joseph mwishoni mwa wiki, wakati wa mafunzo ya maadili yaliyotolewa na maofisa wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya

Kaskazini kwa madiwani na viongozi wa wilaya hiyo, juu ya kufanya uamuzi ambao hauleti mgongano wa kimaslahi.

"Tunashukuru kwa semina hii nzuri ambayo imetupa uelewa mpana juu ya mgongano wa maslahi, wakati wa kufanya uamuzi na athari zake. Niombe ofisi yenu iwe inatupatia elimu baada ya kuchaguliwa, lakini pia ziwapo semina za kila mara kwa ajili ya kutujenga ili kuzingatia misingi ya utawala bora," alisema.

Joseph alitumia fursa hiyo kuiomba sekretarieti hiyo kutenga muda hata wa saa moja, kwenda wilayani humo wakati

wa vikao vya Baraza la Madiwani, ili madiwani ambao hawakuhudhuria semina hiyo wapata elimu juu ya mgongano wa maslahi na jinsi ya kuepuka viashiria vinavyoweza kusababisha mgongano wa maslahi.

Katibu Msaidizi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kaskazini, Anna Mbasha, alisema viongozi wanapaswa kujizuia kupokea zawadi kutoka kwa watu wenye maslahi binafsi, ili kuepuka migongano ya maslahi wakati wanapofanya uamuzi kwenye maeneo yao ya kazi.

"Viongozi wote wa umma mnatakiwa kutekeleza majukumu yenu kwa uaminifu, huruma, kujizuia na tamaa ili kuepuka mgongano wa maslahi ambao unaweza kusababisha wananchi kukosa imani na serikali, lakini pia kusababisha uvunjifu wa amani," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Stephen Ulaya, alisema kuna umuhimu mkubwa wa viongozi wa umma, hasa wa kuchaguliwa kwa sababu Baraza la Madiwani ndicho chombo kinachofanya uamuzi wa mambo yote ya halmashauri kwa niaba ya wananchi waliowachagua.







Askofu Mkuu wa Kanisa la Assemblies of God (TAG) Jimbo la Kilimanjaro Magharibi, Dk. Benjamin Bukuku, akipanda mti kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 80 ya kanisa hilo, tangu kuanzishwa kwake mwaka 1939, yaliyofanyika katika kanisa la Amani Soweto, Moshi Mjini, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wataka elimu zaidi saratani tezi dume

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Mkoa wa Kilimanjaro wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuendelea kutoa elimu juu ya saratani ya tezi dume, ili kuhakikisha wanaume wanajitokeza kwa wingi katika kupima afya zao.

Wakizungunza na Nipashe kwa nyakati tofauti, Sabastiani Msofe, alisema wananchi hawana elimu ya kutosha juu ya saratani ya tezi dume hali inayowafanya kuchelewa kufika kwenye matibabu, hivyo kupoteza maisha.

Alisema bado katika jamii kuna imani potofu juu ya tezi dume, na kuwa serikali hainabudi kuingilia kati kutoa elimu katika kila mikutano ya vijiji, kata na viongozi wa dini watoe elimu kwa wakati.

"Tunaiomba serikali kutoa agizo kwa wataalamu kuanzia ngazi za vijiji kufika kwa kila mkutano wa kijiji, kata, wilaya na hata mkoa kutoa elimu ya afya ya kuzungumzia magonjwa ya saratani hasa tezi dume ili kuleta afueni kwa wanaume," alisema Rafael Elisante na kuongeza:

"Ikiwa viongozi wa vijiji, tarafa, kata, wilaya na mkoa watapewa agizo la kuhakikisha wanaweka ajenda ya afya katika mikutano yao, halmashauri zitume mtaalamu wa afya kufika na kuelezea magonjwa ya saratani itasaidia kubadilisha maisha ya Watanzania na kupata taifa la watu wenye afya bora ambapo wataweza kuleta maendeleo."

Grace Lucas, mkazi wa Wilaya ya Siha, alisema katika baadhi ya makabila wamekuwa wakiogopa kwenda kupima na hata wakigundulika kuwa na saratani hiyo wamekuwa wakikaidi kutumia dawa.

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

# Katazo biashara kwenye umeme

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wametahadharishwa kujiepusha kufanya biashara chini ya miundombinu ya umeme hasa katika kipindi hiki cha mvua, ili kuepuka madhara yanayoweza kuwapata.

Rai hiyo ilitolewa jana na Meneja wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco) mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Mahawa Mkaka, alipozungumza na gazeti hili ambapo alisema vitendo vya ufanyaji wa biashara chini ya miundombinu ya umeme inaweza kuhatarisha maisha yao.

Mhandisi Mkaka alisema kipindi hiki cha mvua miundombinu imekuwa ikiharibika kutokana na upepo mkali, huku pia mvua hizo zimekuwa zikiendana na radi ambapo ni hatari pindi wananchi wakiendelea kufanya biashara chini ya miundombinu hiyo hasa chini ya transfoma.

Alisema ni jukumu la wazazi kuhakikisha mvua zinazoendelea kunyesha zinaweza kusababisha madhara kwa kuanguka kwa nguzo pamoja na kukatika kwa nyaya za umeme kutokana na kuangukiwa na miti.

Meneja huyo alisema kutokana na madhara hayo ni vyema wananchi wakajijengea tabia ya kuvaa viatu pamoja na kuepuka kukanyaga maji ovyo kwani umeme unasafiri kwa kasi sana ndani ya maji.

"Nawasihi sana wananchi ili kuepukana na kupigwa na shoti ni vyema basi wakachukua tahadhari kwa kuvaa viatu, lakini pia waepuke kukanyaga maji ovyo kwani ni hatari sana endapo utakuta nyaya imekatika na kugusa maji kwani umeme huwa na tabia ya kutembea na maji," alisema Mhandisi Mkaka.

Alitoa wito kwa wananchi kuchukua tahadhari kubwa pindi panapotokea tatizo lolote linalohusu Tanesco na kuwataka kutogusa nyaya watakapoona zipo chini na badala yake watoe taarifa ofisi za Tanesco ili kuepuka madhara makubwa ikiwamo vifo.

# Mkakati wa kudhibiti wizi wabuniwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Kata ya Shirimatunda Manispaa ya Moshi wametakiwa kuwa chachu ya usalama katika eneo lao kwa kuanzisha kamati za ulinzi na usalama zitakazohusika kufanya doria ili kukomesha vitendo vya wizi vilivyo shamiri.

Hayo yalibainishwa jana na Diwani wa Kata ya Shirimatunda, Francis Shio, katika mkutano wa maendeleo na wananchi wa kata hiyo. Shio alisema wizi katika Kata ya Shirimatunda umezidi kushamiri kutokana na hali ya uchumi kubadilika, ambapo watu wanarahisisha maisha kwa kujipatia kipato kwa njia ya wizi, jambo ambalo limesababisha kutoweka kwa hali ya usalama.

"Hali ya uchumi imebadilika, na mfumo wa maisha ni lazima ubadilike, watu wanajitafutia kipato kwa njia za wizi, ni lazima wananchi mjitoe kuanzisha kamati za usalama ili kukomesha wimbi la wizi linaloimaliza kata yetu," alisema Shio.

Aidha, Shio aliwataka wananchi kutojenga katika hifadhi za barabara ili kuepuka usumbufu na hasara ya kubomoa majengo hayo wakati wa kupisha ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Inspecta wa Polisi Kanda ya Moshi Magharibi David Gabriel, aliwataka wananchi kuacha itikadi za vyama na dini na kuwataka kuwa pamoja katika kuhakikisha usalama unapatikana katika kata hiyo.

Alisema suala la ulinzi ni suala nyeti kwani kusipokuwa na usalama katika jamii husika wananchi watashindwa kujihusisha na shughuli zao za kimaendeleo.

Joseph Mushi, mkazi wa kata hiyo, alisema suala la wizi limekithiri na kuwa ikiwa watapewa muongozo sahihi wa namna ya kuanzisha kamati hizo za ulinzi na usalama zinaweza kutokomeza matukio ya kihalifu.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 4, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## JE WAJUA



Ukurasa 18

**Wanasayansi watengeneza ukungu unaoua 99% ya mbu wa malaria**

Ukurasa 17



## JIELIMISHE
Usafi ndio adui wa Kipindupindu




# RAIS MPYA CHUO KIKUU MUHIMBILI:
# Kuingiza siasa kunakwamisha tija sekta ya afya nchini

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# Umuhimu wa kuripoti haraka kituo cha polisi unapopoteza simu ya mkononi

NDUGU, mwananchi mwenzangu, kwanza nianze na kukupa pole kwa majukumu ya kila siku pamoja na hongera kubwa kwa kujishughulisha, kama Mtanzania mwenye kuhitaji maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla.

Dunia yetu imeingia katika maendeleo ya teknolojia ya mitandao, hivyo kutokuwa na ufahamu wa mitandao ni kukosa kitu muhimu katika maisha, maana tunakoelekea kila kitu kitahusisha mitandao, isipokuwa mambo machache sana.

Hebu jiulize swali kama umewahi kutoka nyumbani ukasahau simu yako ya mkononi, je siku hiyo utafanya kazi vizuri?.

Jibu liko wazi hakuna aliyeko salama katika zama hizi kwamba anaweza kukwepa teknolojia, la hasha ni ngumu.

Tujifunze kwanini ni muhimu kupata elimu hii ya makosa yanayohusiana na mitandao.

**ATHARI**

Kwanza kila mmoja ajue kwamba katika matumizi ya mitandao (hapa nina maana ya intaneti) lazima utajikuta ni muathirika wa matumizi ya mitandao ya kijamii, mfano whatsapp, facebook, tweeter, instagram, snapchart, blogs, websites, forums n.k.

Katika matumizi hayo kila mmoja wetu huenda akajikuta mtenda makosa ya kimtandao kwa namna moja ama nyingine.

Ukiipitia sheria ya makosa ya kimtandao (the cyber crime act 2015) utajua kabisa kwamba hakuna ambaye hataonekana hatendi kosa lolote la kimtandao katika jamii, japo watu huzidiana ukubwa wa makosa yenyewe.

Hivyo ni wazi kwamba kila mmoja wetu ni muathirika wa matumizi ya intaneti, hivyo anahitaji elimu hii.

**MIFUMO**

Kwa asilimia kubwa ya watu duniani kote ni watumiaji wa simu za mkononi maarufu kama smartphone.

Simu hizi zimegawanyika katika mifumo mbalimbali kutegemeana na mfumo uliowekwa ndani ya simu yenyewe, kama vile:-android, windows, rim, ios, droids n.k.

Asilimia kubwa ya watu duniani hutumia simu zenye mfumo wa android ambapo ndipo mwandishi wa makala haya amejikita zaidi katika kuelimisha kuhusiana na simu za aina hiyo.

**KURIPOTI POLISI**

Pengine swali ni kwanini unashauriwa kuripoti haraka kituo cha polisi mara unapopoteza simu ya mkononi?



Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**

Zipo sababu kadha wa kadha za kiusalama ambazo zinaweza kuwa hatari kwa mwanachi aliyepoteza simu bila kuchukua hatua ambazo zinaweza kumkuta, iwapo simu hiyo itafika mikononi mwa watu wabaya (wahalifu) wa kimitandao.

Kutokana na kwamba upelelezi wa makosa ya kimtandao huwa mgumu na unahitaji utaalamu wa hali ya juu, ni muhimu kutoa taarifa mapema.

Nitataja sababu mbili muhimu za kuzingatiwa kutokana na ukweli kwamba mada hii ni ndefu sana kitaalamu.

**UWEPO WA MFUMO DHAIFU WA ULINZI**

Simu za android ambazo mmiliki wake ni kampuni ya google, haina ulinzi wa kutosha kuweza kumzuia mtu asiyekuwa mhusika kuingia kwenye mfumo na kufanya anachotaka.

Hapa nina maana hata kama umeweka security kama pin, password, fingerprint au patten, zipo njia kadha wa kadha za kuondoa ulinzi wako iwapo anayefanya hivyo ana lengo la kutenda uhalifu.

Uzoefu unaonyesha watu wengi waliopoteza simu wanalalamikia kusambazwa kwa picha zao za usiri katika mitandao mbalimbali ya kijamii pamoja na kuibiwa fedha kwenye huduma za mitandao ya kifedha kama m-pesa, tigo pesa n.k.

Katika eneo hili pia ni hatari kwa mtu aliyepoteza simu kwani kwa kukosa ulinzi wa simu hiyo, mhalifu anaweza kupata nafasi ya kuingia katika mitandao ya kijamii, blogs, you tube channels, gallari ya simu na kufanya mambo mbalimbali mabaya, ama anaweza kutapeli watu kutumia akaunti ya mhusika na kufanya mambo mengine mengi mabaya ambayo ni uhalifu kama uhalifu mwingine.

**WADUKUZI WA KIMTANDAO (hackers & hacking mods applications)**

Wapo watu wanaitwa wadukuzi. Hawa ni watu ambao wanatumia mfumo kudhohofisha kifaa chenye mfumo na kuweza kupenya, kisha kufanya wanachotaka ndani ya kifaa husika.

Kitaalamu wanatumia hacking mods applications ambazo zina uwezo wa kufanya chochote atakachohitaji kwenye kifaa husika.

Mfano zipo ambazo zina uwezo wa kurudisha vitu ulivyowahi kufuta kama picha, video na ujumbe wowote, ama ambazo zina uwezo wa kutuma taarifa za muhanga kuanzia sauti, ujumbe wa maneno wa kawaida na hata taarifa zote utakazopokea na kutuma kwa njia ya mitandao ya kijamii na barua pepe.

Hii ni hatari na ni kosa kisheria hata zile za kimataifa.

**UNAWEZAJE KUWA MUATHIRIKA WA KOSA LA KIMTANDAO?**

Kumbuka mambo yaliyotajwa hapo juu yanapotokea kwenye simu uliyoipoteza kunaweza kusababisha makosa ya kimtandao ambayo pia ni jinai.

Mtuhumiwa namba moja atakuwa ni yule aliyepoteza simu kwa uzembe ambaye hakuripoti upotevu wa simu yake katika kituo cha polisi.

Hivyo, sheria iko wazi utawajibishwa kwa kutumia kifaa chako (simu) kufanyia uhalifu wa kimtandao. Mfano ukipoteza simu au kuibiwa, haujatoa taarifa, mtu aliyeokota akasambaza picha chafu, akatapeli watu, akatuma jumbe za matusi, yote hayo ni makosa kisheria na polisi watafanya kazi yao ya kuchunguza na kumkamata mmiliki wa simu.

Kwa hiyo utajikuta kwenye matatizo pasipo kutenda kosa.

Hivyo kuripoti kituoni mara tu unapoibiwa au kupoteza simu ya mkononi ni suala la msingi kwa watumiaji wote wa simu za mkononi ili usije kujikuta unatuhumiwa uhalifu pasipo kutenda kosa.

***Imetolewa na Kitengo cha Uhusiano, Polisi Makao Makuu, Dar es Salaam. barua pepe habari.phq@tpf.go.tz au habariphq@gm***

---

## TUJIFUNZE KISWAHILI



**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Funzo la mjinga taabu

'TAABU' ni hali ya kuwa na shida, mashaka, kero au usumbufu. Maana yake mtu mjinga huishia kujifunza kutokana na shida au taabu kwa sababu ya kupuuza ushauri. Methali hii hutumiwa kumwelezea mtu anayepuuza ushauri anaopewa.

Nimekuwa nikiwakosoa waandishi wanaotumia maneno ya kihuni au kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kana kwamba maneno ya kigeni wanayotumia hayamo kwenye Kiswahili ilhali (jambo linaloelezwa ni kinyume cha ukweli ulivyo) yamo, ila ni uvivu wa waandishi kuyatafuta kwenye kamusi mbalimbali za Kiswahili.

Kutokana na umaarufu wa lugha ya Kiswahili, vituo vingi vya redio duniani hutangaza taarifa zao za habari kwa lugha ya Kiswahili: Redio za Umoja wa Mataifa, Marekani, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Urusi, India, Japan na nchi kadhaa za Afrika. Kama hiyo haitoshi, sasa baadhi ya nchi za Afrika zinaomba Tanzania kuzipelekea walimu wa kufundisha Kiswahili. Hii yadhihirisha jinsi lugha ya Kiswahili inavyopendwa duniani.

Baadhi ya viongozi wa nchi za Afrika wameshauri Kiswahili kiwe lugha ya taifa ya Afrika yote. Ndo maana wahenga walijua hili mapema walipokisema: "Usijivunie cha mwenzako." Maana yake usijivunie kitu ambacho si chako. Methali hii yaweza kutumiwa kutukumbusha kuwa hatupaswi kuvionea fahari vitu vya wenzetu bali vitu vyetu wenyewe.

Pamoja na mapenzi waliyonayo watu wa mataifa mbalimbali, sisi ambao ndiwo wenye asili ya lugha ya Kiswahili, ama hatujui thamani yake au tunaidharau lugha hii adhimu (iliyo na sifa na heshima kubwa) inayohusudiwa (kutamani mafanikio, kitu au uwezo mwingine; kitendo cha mtu kutamani kuwa kama alivyo mwingine) duniani kote.

Nimeandika mara kadhaa umuhimu wa kuienzi lugha ya Kiswahili lakini kadiri ninavyosisitiza ndivyo waandishi wenzangu wanavyozidi kuingiza maneno ya kihuni au kuchanganya Kiswahili na Kiingereza kwenye habari na makala za magazeti yao kama ilivyo redioni na kwenye runinga!

Takriban robotatu ya Watanzania hawajui 'nasuri' ni kitu gani ila wanajua 'fistula' ambalo ni neno la Kiingereza. 'Nasuri' (Kiswahili cha 'fistula') ndilo neno la Kiswahili linalopaswa kutumiwa badala ya lile la Kiingereza – 'fistula.'

'Nasuri' ni ugonjwa uwapatao wanawake ambapo tundu la mkojo limepasuka na kusababisha mkojo utoke mara kwa mara bila kukusudiwa; tundu linalotokea katika misuli kati ya uke na kibofu cha mkojo au kati ya uke na njia ya haja kubwa ama sehemu zote mbili.

Tukiacha hilo, baadhi ya maneno yatumiwayo vibaya ni: lakini, kwa niaba yangu, wakilisha, mwisho wa siku n.k. 'Lakini' ni tamko la kuonesha kasoro ya jambo; neno linaloonesha uwepo wa upungufu, au hitilafu.

Neno hili hutumiwa sana na wanasiasa wanapoeleza kazi zilizofanywa. Kwa mfano: "Serikali imejenga barabara nyingi nchini lakini pia inajenga njia ya reli ya kisasa kati ya Tanzania na Rwanda ..." Neno 'lakini' halikutumika ipasavyo kwani ni neno linaloonesha upungufu, kasoro au hitilafu ya jambo. Ni sahihi kusema: "Serikali imejenga barabara nyingi nchini, pia reli ya kisasa kati ya Tanzania na Rwanda ..."

Wanasiasa wanapotoa hotuba husikika wakisema: "Kwa 'niaba yangu' namshukuru kiongozi wetu mpendwa kwa kutimiza ahadi yake ya kutupatia maji safi na salama baada ya miaka kadhaa." Neno 'niaba' maana yake ni badala ya mtu au watu wengine. Isemwe: "Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu, namshukuru kiongozi wetu mpendwa kwa kutimiza ahadi yake ya kutupatia maji safi na salama ..." Yaani unashukuru kwa niaba ya waliokutuma.

'Mwisho' maana yake ni hali ya kumalizika; tamati, ukomo wa jambo, hitimisho. Wengi wetu wamezoea kusema, kwa mfano: "Mwaka jana nililima sana lakini 'mwisho wa siku' sikuambulia kitu."

Kilimo hakifanywi kwa siku moja hata isemwe 'mwisho wa siku' kwani hufanywa kwa msimu yaani kipindi maalum katika mwaka ambapo hali ya hewa mahsusi au jambo fulani hutokea. 'Siku' ni muda wa saa 24 kuanzia saa moja asubuhi hadi asubuhi inayofuata. Sijui mtu awezaje kulima na kuvuna kwa siku moja!

Vilevile kuna tofauti ya wakilisha na wasilisha. 'Wakilisha' kwa muktadha ninaoujadili ni neno lenye maana mbili: Kwanza ni kitendo cha kufanya jambo kwa niaba ya mtu mwingine. Kwa mfano, Rais, kiongozi au mtu yeyote aweza kumteua mwakilishi (mtu anayefanya jambo kwa niaba ya mwingine/wengine) ili amwakilishe kwenye tukio fulani.

'Wasilisha' (kitenzi elekezi) ni fikisha kitu au ujumbe mahala fulani; toa maelezo au mhadhara kwa kikundi cha watu au mbele ya watu.

Neno 'chama' lina maana zaidi ya moja. Kwanza ni kikundi cha watu wenye itikadi au lengo moja; kundi lenye kufuata kaida au silka fulani zenye kuegemea dini, siasa au msimamo ya jamii, uchumi au jambo lingine lolote lenye maazimio maalumu. Kwa ufupi ni muungano wa watu wenye lengo moja.

Ni upotoshaji wa lugha ya Kiswahili kusema au kuandika: 'chama la wana', 'chama lao', au 'chama letu.' Ufasaha wa Kiswahili ni 'chama cha wana', 'chama chao' na 'chama chetu.' Siku hizi klabu ya kandanda yaitwa 'chama letu' au 'chama lao' na kushabikiwa sana na waandishi wa habari za michezo!

***Methali: Asiye na nadhari, siandamani naye.***

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

MAKALA MAALUM

MALEZI
NA MICHAEL ENEZA

# Kuna njia ya lazima ya kulea watoto, au ni mazingira tu?

MOJA ya maeneo yenye idadi kubwa ya wataalamu ambao mara nyingi wanatokea fani tofauti na hakuna uhakika kama taaluma zao zinashabihiana, yaani kama wanafundisha kitu kile kile kuhusu mada hiyo hiyo ni suala la malezi ya watoto.

Kuna aina tatu muhimu za fikra kuhusu malezi ya watoto, moja ni ya kitaalamu ambayo mchepuo wake ni elimu ya mtoto na jinsi hitaji la malezi (wanaita 'pedagogy' kwa hisia za Kiyunani/Kiingereza) linavyoinuka hapo. Nyingine ni ile inayoendana na dini, ambayo kimsingi ni kutafsiri sheria za dini ziwe msingi wa malezi, kuwa malezi bora ni yale yanayompeleka mtoto katika dini, hivyo kuwa mtu bora katika jamii.

Kuna eneo la tatu ambalo unaweza kusema ni busara ya kawaida ambayo kimsingi haihitaji kwenda shule, na mara nyingi zaidi hutolewa pale mhusika akiulizwa halafu anatoa kile ambacho amekishuhudia katika maisha.

Hapo hakuna suala la taaluma wala misahafu na kuwatayarisha watoto kufuata hiki au kile katika maisha ila kuwajali watoto kama sehemu ya familia, na hapo lipo suala la mazingira ya mhusika, kama ni mama anayelea watoto peke yake au ipo ndoa.

Na pia kuna suala la furaha katika maisha kwa ujumla au furaha katika ndoa inayoathiri malezi ya mtoto, na hapo ndipo ukawaida unapokuwa busara, kuwa dini na elimu zinakuwa hazina jawabu.

Tatizo la mitazamo ya kielimu na kidini ni kuwa inategemea sana kile ambacho wataalamu wa uchumi wanaita 'ceteris paribus,' kuwa 'kila kitu kikibaki kama kilivyo,' au 'kila kitu kikienda sawa' ndivyo itakavyokuwa.

Sasa kupambanua jambo lolote linalogusa maisha au shughuli ya muda mrefu kwa msingi wa 'kila kitu kikibaki kama kilivyo' au 'kila kitu kikienda sawa' siyo busara, kwani dunia inabadilika.


Na neno au dhana ya 'dunia' kimsingi humaanisha mahusiano, kwa maana ya nafasi ya mtu katika maisha ya mtu mwingine, ana thamani gani au kuna fursa gani za kuthamanisha, kuna mapungufu gani na maisha ya kila siku yanapambanuaje, au kutatua mapungufu hayo. Hilo likiingizwa katika mielekeo ya elimu au dini huvuruga kinachojadiliwa.

Moja ya vigezo muhimu vya hisia au dhana za malezi ya watoto kwa misingi ya taaluma ya elimu ambayo inashabihiana sana na ile ya dini ni umuhimu wa malezi ya 'wazazi wote wawili,' kuwa endapo kuna upungufu katika hilo mtoto anaathirika.

Siyo rahisi kuhoji usahihi wa dhana hiyo ila unaweza kuuliza 'kwa kiasi gani,' na ukiangalia kwa upande huo unakuta suala la msingi siyo kuwepo kwa wazazi wawili ila kuelewana, hivyo fursa za kujua au kuelewa hisia za mzazi mwingine zinakuwepo. Endapo uelewano haupo, kuwepo tu kwa ndoa siyo mwarobaini.

Hilo lina maana pia kuwa endapo uelewano upo, kutokuwepo kwa ndoa vile vile siyo sumu au kipingamizi

"Siyo rahisi kuhoji usahihi wa dhana hiyo ila unaweza kuuliza 'kwa kiasi gani,' na ukiangalia kwa upande huo unakuta suala la msingi siyo kuwepo kwa wazazi wawili ila kuelewana, hivyo fursa za kujua au kuelewa hisia za mzazi mwingine zinakuwepo. Endapo uelewano haupo, kuwepo tu kwa ndoa siyo mwarobaini.



Malezi kama haya ni muhimu kwa makuzi ya mtoto. **PICHA: MTANDAO**

katika malezi, kwani mama anayelea pekee lakini ana mtu wa uhakika ambaye anamsikiliza wakiongea jambo lolote, atamudu upeo au matazamio ya wanae.

Hata kama siyo kila wanachohitaji kitapatikana, na hata kama wataishi kwa uchache, inatosha kuwa huyo mama awe anaridhika kiasi fulani na kile ambacho mwenza wake anakifanya, au anajitahidi kukifanya.

Akiwa katika hali hiyo ya kuridhika kimsingi watoto hawawezi kukata tamaa, ila akiwa katika huzuni na sononeko la kila wakati, hawezi kutoa mwelekeo kwa wanae kwani hata ari ya kutumia muda ipasavyo kwa mahitaji yao inapungua.

Inaweza kuwa ni kutumia muda mwingi nyumbani kuliko mizunguko, na inaweza pia kuwa ni hata kuwahudumia tu, ndiyo maana pale masikitiko hayo (kimsingi ni ya kukataliwa, au kubezwa) yanapoanza mapema, kuna uwezekano mkubwa wa kichanga kutupwa chooni au jalalani kwani mama hana motisha ya kukilea.

Hao wanaojadili malezi ya watoto kwa msingi wa 'haki za mtoto' wanakuwa kama wanafundisha tu. Mwanamke hajizalii mwenyewe; baba akimkataa mtoto ni kama kumlaani, anaweza hata akafa.

Utaaluma huu au uduni wa utaaluma ('pedantry' kwa Kiyunani/Kiingereza) ni kunukuu tu au kurudia kile ambacho kinaelezwa katika vitabu au amri za makuhani, na siyo inavyokuwa katika hali halisi.

Ndiyo maana ukiangalia unakuta kuwa kielelezo kikuu au msingi halisi wa malezi ni jadi, siyo taaluma (elimu ya mtoto na malezi yanayoendana na hitaji hilo) au dini (kanuni za kumsuka mtu bora katika jamii) kwani jadi inaunganisha watu katika maisha ya kawaida, lugha yao, hisia zao, wanavyojali, kushtuka au kubeza. Hawatumii taaluma wala dini, ila hisia za jadi.

Dhana ya jadi siyo sawa na dhana ya utamaduni, kwani kwa kawaida neno utamaduni halina tofauti kubwa na dini, kwa sababu utamaduni una mlolongo wa kanuni za kufuatwa na huwa zinaendana na mazingira ya ibada katika mkusanyiko au jamii husika.

Jadi ni kitu tofauti kwani haina taasisi ila marejeo ya kitaasisi, wakati utamaduni una taasisi na kazi yake muhimu zaidi ni kutoa maamuzi pale migongano inapotokea, kile ambacho wanataaluma wanaita 'kutoa haki' kana kwamba dhana ya haki inaongoza shughuli za kisheria kwa jumla, na siyo jeuri, na hasa jeuri ya pesa au mamlaka.

Jadi ni pamoja na hitaji la kila mtu kuwa huru, linalopuuziwa takriban kote kwingine - iwe ni utamaduni, licha ya kudengulia suala hilo kiasi fulani, taaluma au dini, ambako kinachosisitizwa katika maeneo hayo ni kanuni, sheria, utii - hata uitwe

INAENDELEA UK.18

ELIMU

NA RAPHAEL KIBIRITI

# RAIS MPYA CHUO KIKUU MUHIMBILI:
# Kuingiza siasa kunakwamisha tija sekta ya afya nchini

AFYA bora na imara ni mzizi wa furaha na ustawi wa binadamu yeyote.

Kimsingi, afya bora ina mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi kwa sababu wananchi katika taifa lolote lile wanapokuwa wako vizuri kiafya wanaishi kwa muda mrefu.

Aidha, wanakuwa na tija katika uzalishaji na hivyo kuendeleza jamii na taifa lao kwa ujumla wake.

Na ndiyo maana afya ni moja ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs).

Lengo Namba 3 la SDGs linahimiza nchi zihakikishe watu wake na kwa kila rika wanakuwa na afya bora.

Kuna mambo mengi yanayochangia nchi kufanikisha hilo la kutoa huduma bora za kiafya kwa wananchi wake na mojawapo ya hayo ni rasilimali watu ya kutosha yenye ujuzi stahiki katika sekta ya afya.

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), ndiyo chungu kikuu kinachotegemewa nchini kutoa wataalamu wa afya wenye dhamana ya kuhakikisha afya za Watanzania ziko timamu katika suala zima la kusukuma gurudumu la maendeleo mbele.

Hivi karibuni chuo kikuu hicho kilifanya uchaguzi wake ambapo kilipata Rais wa serikali mpya ya wanafunzi. Nipashe kupitia kwa mwandishi wake ilifanya mahojiano na Costantine Alex Ntanguligwa, Rais wa serikali mpya ya wanafunzi MUHAS kuhusiana na mambo mbalimbali ya uchaguzi huo, lakini pia hali halisi ya sekta ya afya nchini.

***Ifuatayo ni sehemu ya kwanza ya mahojiano hayo.***

**SWALI:** TUNAPOZUNGUMZIA Rais wa Wanafunzi Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), tunazungumzia mtu wa aina gani na anaongoza akina nani?

**JIBU:** AHSANTE, kwa hilo cha kwanza lazima tufahamu kwamba katika nchi yetu kuna sheria ambayo inazitambua serikali za wanafunzi kisheria, ambayo ni University Charter ya mwaka 2007 ambapo article ya 6 na ibara ya 30 na 31 inazitambua serikali za wanafunzi kisheria. Hivyo tuna wajibu wa kusimamia maslahi ya wanafunzi wetu. Hata hivyo, katika chuo chetu kuna watu wa aina tofauti tofauti.

**SWALI:** Kivipi?

**JIBU:** Chuo chetu cha MUHAS kina wanafunzi wenye diploma, wanafunzi wa digrii na wanafunzi wa post graduate (Baada ya digrii ya kwanza) kuanzia level ya masters of medicine (Shahada ya uzamili katika tiba), masters of science (shahada ya uzamili katika sayansi) mpaka super specialties (shahada za ubingwa maalum).



Rais wa Serikali mpya ya MUHAS, Constantine Alex Ntanguligwa.

Kwa hiyo katika serikali yetu, sisi uongozi wetu wa serikali ya wanafunzi unaishia kwa wanafunzi wa undergraduate.

**SWALI**: Unaweza ukafafanua zaidi hapo?

**JIBU:** Ufafanuzi zaidi ni kwamba wanafunzi ambao sisi tunawaongoza na kwa mujibu wa katiba yetu inawatambua wanafunzi hao wa undergraduate kuwa ni wanafunzi wote waliosajiliwa na kuwa admitted katika chuo chetu. Kwa hiyo serikali ya wanafunzi, mimi huwa ninapenda kusema kwamba ni daraja kati ya wanafunzi na menejimenti ya chuo na huwa napenda sana kusema na kuwaambia viongozi wenzangu kwamba taaluma ya wanafunzi katika chuo inategemea vitu vitatu.

**SWALI:** Vitu gani hivyo?

**JIBU:** Kwamba kuna sehemu ambayo chuo kinafanya kazi yake na sehemu ya mwanafunzi mwenyewe. Aidha, kuna sehemu ya kiongozi. Sasa chuo kama chuo kazi yao na wajibu wao wa msingi ni kuhakikihsa wanatoa elimu bora inayoendana na viwango na inayokidhi mahitaji ya sasa kwa huyu mwanafunzi. Lakini tunafahamu katika process (mchakato) hii kuna changamoto ambazo zinaweza kutokea za hapa na pale mwanafunzi kama amedhulumiwa haki zake, lakini kuna kipindi ambacho mwanafunzi naye anakosea na hapo unakuja umuhimu wa uongozi wa wanafunzi.

**SWALI:** Ni upi huo?

**JIBU:** Kupunguza hiyo 'gap' na kuwasaidia wanafunzi wetu kwa kuwatetea katika sekta zote za kisheria lakini vilevile kurahisisha mawasiliano baina ya uongozi wa chuo na wanafunzi kukitokea shida, kukitokea wana matatizo, kwa hiyo viongozi wana-act (wanachukua jukumu) kama daraja, kwamba ni lazima wawaeleze wanafunzi kutimiza wajibu wao, huku chuo kikitimiza wajibu wake, kwa sababu tumepewa nguvu hiyo kisheria.

**SWALI:** Kuna mchakato wa kumpata rais kila mahali na katika ngazi tofauti za kiutawala. Kwa hapa MUHAS, rais anapatikana kwa taratibu zipi na sifa zake zinakuwa ni zipi?

**JIBU:** Eee tukirejea Kanuni zetu za Uchaguzi za mwaka 2014, zinaeleza utaratibu mzima wa kupata marais katika chuo chetu. Eee na utaratibu wa awali kabisa huwa unaanza na serikali inayomaliza muda wake kwa kupitia katika Bunge. Katiba yetu imelipa Bunge nguvu ya kuteua tume ya uchaguzi ya mwaka huo, yaani mwaka mpya wa uongozi. Kwa hiyo bungeni Spika amepewa nguvu ya kuteua tume ya watu watano.

**SWALI:** Ni wapi hao?

**JIBU:** Tume inakuwa na mwakilishi mmoja kutoka Kila School (shule). Sisi chuo chetu kina shule tano, school ya medicine (shule ya tiba) ambayo ina jumuisha wanafunzi wa udaktari, wanafunzi wa maabara na wanafunzi wa mionzi tiba. Kuna School ya Nursing (shule ya uuguzi) nayo inahusisha wauguzi, School ya Dentistry inahusisha wataalamu wa meno, School ya Public Health (shule ya afya ya umma) inahusisha maofisa afya na wataalamu wa mazingira. Vilevile shule ya ufaamasia inayohusisha wataalamu wa dawa.

**SWALI:** Kwa hiyo Spika anatakiwa kufanya nini?



Rais wa Serikali mpya ya MUHAS ( watanoi kutoka kushoto) akiwa na wanafunzi wenzake waliokuwa wakimuunga mkono. **(PICHA:MTANDAO)**

**JIBU:** Kwa hiyo katika tume hii ya uchaguzi, Spika anatakiwa kuchagua mwakilishi kutoka kila school na kutengeneza tume ya watu watano na anaileta bungeni na Bunge linaidhinisha kupitisha hiyo tume. Lakini baada ya hapo tume inatakiwa kukaa na kuchagua mwenyekiti wao na katibu. Na katika kikao hicho ambacho wanakaa pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria anayemaliza muda wake, wanalazimika kutoa utaratibu na ratiba na kupanga bajeti ya uchaguzi wa mwaka huo.

**SWALI:** Na baada ya hapo nini kinaendelea?

**JIBU:** Then (kisha) hayo yakishatimia tume ya uchaguzi inaanza kutangaza rasmi chaguzi ndogo. Kama ilivyo kwenye nchi, huwa na sisi tunaanza na chaguzi ndogo, chaguzi za viongozi wa madarasa, viongozi wa makazi na mabweni yetu hapa, viongozi wa vitivyo au school na mwisho wa siku uchaguzi wa urais. kwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni zetu, zimeeleza wazi nani anastahili kuwa kiongozi wa serikali ya MUHAS.

**SWALI:** Unaweza kunitajia baadhi ya kanuni?

**JIBU:** Cha kwanza kabisa kwenye taaluma yake lazima awe na GPA ya kuanzia 2.3 kwenda juu kutoka mwaka uliopita wa masomo, lakini vilevile hatakiwi kuwa na nyadhifa yoyote katika chama chochote cha kisiasa. Kwa hiyo hatakiwi labda kuwa katibu wa hamasa au mwenyekiti wa tawi au mjumbe wa siasa wa chama chochote. Ieleweke wazi hazuiwi kuwa mwanachama wa chama, lakini haruhusiwi kuwa kiongozi wa chama. Hivyo ukishakuwa kiongozi wa chama chochote cha siasa, unakosa sifa za kuwa kiongozi hapa kwenye serikali yetu ya wanafunzi.

**SWALI:** Kuna mengine?

**JIBU:** Vilevile unapokwenda kuomba ridhaa kwenye nafasi ya urais, lazima uwe na walau wadhamini kama ilivyo kwenye nchi, watu walau 20 kutoka kwenye kila school nilizozieleza au zaidi na saini na kila kitu. Lakini pia lazima usiwe na kosa lolote la jinai au kosa lolote la kushtakiwa mahakamani, ndani na nje ya nchi. Pia lazima uwe na nidhamu (good conduct wanasema kwa Kiingereza) na uwe mwana MUHAS au active member (mwanachama hai) wa jumuiya yetu.

**SWALI:** Kuna ratiba maalumu ya uchaguzi wa rais ?

**JIBU:** Kwa kawaida kama nilivyosema chaguzi ndogo zinaanza lakini kwa mujibu wa katiba yetu, uchaguzi wa urais lazima uwe ndani ya wiki moja kabla ya ratiba za uchaguzi kwisha. Hivyo zinaanza chaguzi ndogo, then (kisha) kampeni za urais ambazo huwa zinafunguliwa na mshauri wa wanafunzi. Na kama ilivyo kwenye nchi tunatangaza nia, tunachukua fomu, tunafuata masharti mengine yote. Hivyo tume inatuchuja wagombea na hatimaye inatangaza rasmi majina ya wagombea. Kwamba hawa sasa ndio wagombea rasmi wa urais na mshauri wa wanafunzi anafungua kampeni rasmi.

**SWALI:** Kuna muda wa kampeni za urais hapa MUHAS?

**JIBU:** Hapa kwetu huwa tuna kampeni za takribani wiki moja za urais. Na katika hizi kampeni kuna matukio mawili makubwa yanafanyika ambayo ni midahalo ya kubishana kwa hoja, kutangaza sera na wana-MUHAS wanapewa nafasi ya kuuliza maswali. Kwa hiyo katika kipindi chote hiki, kuna midahalo miwili na kampeni zinakuwa zinaendelea madarasani na sehemu zingine na hatimaye sasa tume inatangaza rasmi siku ya uchaguzi na wana-MUHAS wanapewa fursa ya kuchagua hatimaye rais anayewafaa. Kwa hiyo kwa ufupi utaratibu wetu wa uchaguzi huwa hivyo.

**SWALI:** Kampeni kwenye maeneo mengine kama ya kisiasa kwa nafasi ya urais, huwa na matukio mbalimbali yakiwemo ya fitina, kasheshe, rushwa na mengineyo.Unaweza ukazieleza vipi kampeni za urais ambazo hatimaye umeibuka mshindi?

**JIBU:** Kama ilivyo kwenye nchi, kwa sababu tunaamini kabisa kwamba serikali za wanafunzi zinatengeneza viongozi wajao, so katika nchi kuna mambo ambayo kwenye uchaguzi yamekatazwa na ninafikiri ni kwa nia njema na lengo jema la kulea viongozi watarajiwa. Kwa mfano kuna vitu vitano kwa mujibu wa kanuni na taratibu zetu za uchaguzi vimekatazwa katika kampeni. Kwanza ni matumizi ya rushwa, kupokea au kutoa rushwa kwa namna yoyote ni against (kinyume) cha kanuni za uchaguzi, kwa hiyo haitakiwa kabisa. Lakini vilevile kama wanafunzi, sisi ni vijana wakati mwingine kuanza kurushiana maneno ya hapa na pale hutokea.

**SWALI:** Kwa hiyo inakuwaje?

**JIBU:** Ndiyo maana tumekatazwa kabisa lugha ya matusi kwenye hizi kampeni zetu. Eee na namna yoyote ya unyanyasaji wa kijinsia au maneno yoyote yanayoonekana ya udhalilishaji. Lakini vilevile tumekatazwa kutumia unyanyasaji labda wa rangi, ubaguzi wa rangi, wa jinsia, vilevile ukabila na vyote ambavyo kimsingi, nchi yetu inakataza visivyoendana na misingi ya usawa. Hivyo katika kampeni zetu tunakatazwa vilevile kutumia hivyo vitu. Aidha, kutumia nguvu (physical violence) kumekatazwa kabisa katika kampeni zetu. Yaani hakuna haja ya kutumia nguvu, kwani tuko kwenye jamii ya kisomi, ni lazima tubishane kwa hoja na mwisho wa siku, watu wapewe nafasi ya kuona yule anayewafaa. Kwa hiyo hakuna haja ya kutumia nguvu au polisi ya nini! Lakini vilevile huruhusiwi kuharibu kampeni ya mwenzako, kama ambavyo tunashuhudia kwenye ngazi ya nchi, huyu anafanya kampeni watu wanavamiwa kwenye misafara na nini. Kwa hiyo kampeni zinapaswa kuwa za haki kwa sababu sisi tuko kwenye jamii ya kisomi na kuna kila sababu ya kuto-entertain (kuendekeza) vitendo vya namna hiyo kwa sababu, tunayoyalea leo, kesho ndiyo yanatokea kwenye nchi. kwa hiyo uchaguzi lazima uwe wa wa amani, wa demokrasia, watu wapewe haki yao na uhuru na hivyo mwisho wa siku ndiyo nature (asili) ya chaguzi tulio nao Muhimbili tunapotafuta uongozi wa watu.

SWALI: Tunapozungumzia MUHAS, ni chungu cha kutoa wataalamu katika kada ya afya kwa ustawi wa nchi kwa ujumla wake, unazungumziaje sekta ya afya nchini ukiwa mwanafunzi wa udaktari?

JIBU: Sekta yetu ya afya ina changamoto nyingi kwa sasa na changamoto hizi zinaweza zikawa kwenye makundi mbalimbali. Tuna changamoto ya rasilimali watu, tunaweza kuwa na changamoto ya vifaa tiba lakini vilevile tunaweza pia kuwa na changamoto ya inayojitokeza sasa hivi ya kuingiza siasa kwenye kada ya afya. Ni kweli tunafahamu siasa ni sehemu ya maisha, na usiposhiriki, itakuathiri kwa namna moja au nyingine.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**

JIELIMISHE

## USAFI NDIO ADUI WA KIPINDUPINDU

KIPINDUPINDU ni ugonjwa hatari unaosababishwa na bakteria aitwaye "vibriocholerae" ambaye huathiri zaidi utumbo mwembamba.

Bakteria hao husababisha kuhara na kutapika sana, lakini pia homa kali.

Kwa kawaida bacteria hawa hupatikana katika vyakula au maji machafu na kinyesi kutoka mtu aliye na maambukizi.

Kwa hali hiyo, ugonjwa huu huambukizwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na usambazaji wa maji machafu na barafu zilizotengenezwa kwa maji machafu.

Lakini pia vyakula na vinywaji vilivyo na bakteria, mboga zilizopandwa kwenye maji taka na samaki na dagaa waliovuliwa kwenye maji machafu.

MAKUNDI YANAYOWEZA KUAMBUKIZWA HARAKA

Kuna makundi ambayo yanaweza kuambukizwa kwa haraka zaidi.

Hayo ni pamoja na wasafiri, sehemu zenye mikusanyiko ya watu wanaokula kama hotelini, harusini na kadhalika.

Lakini pia wafanyakazi wa afya, waandaaji wa vyakula mtaani (Mama ntilie), wakazi wa makazi duni, wavuvi na watoto.

DALILI ZA KIPINDUPINDU

Dalili za ugonjwa wa kipindupindu zinaweza kuonekana ndani ya saa chache au siku tano baada ya maambukizi.

Dalili hizo ni pamoja na kuharisha maji maji (maji yanayofanana na maji ya mchele), kutapika, mapigo ya moyo kwenda haraka na upungufu wa maji mwilini unaosababisha kusinyaa kwa ngozi, ukavu wa mdomo, koo, na pua.

Lakini dalili zingine ni pamoja na kushuka kwa shinikizo la damu, maumivu ya misuli na kiu cha mara kwa mara.

Maambukizi ya kipindupindu ni ya kawaida kwa makazi ya mijini na vijijini au katika mazingira yenye upungufu wa maji safi.

JINSI YA KUZUIA KIPINDUPINDU

Njia za kuzuia kukumbwa na ugonjwa huu hatari ni pamoja na kuzingatia njia sahihi za usafi kwa kunawa mikono kwa sabuni mara kwa mara, hasa baada ya kutumia choo na kabla ya kushika chakula.

Aidha, matumizi ya vyoo wakati wote na kutumia maji safi na salama yaliyochemshwa, ama yaliyochanganywa na dawa ya kuua wadudu.

Lakini pia inashauriwa kutumia maji ya chupa kwa matumizi ya kunywa, kuandaa chakula au vinywaji, kutengeneza barafu na kusafisha meno.

Vilevile kuosha uso na mikono, kuosha vyombo, matunda pamoja na mboga.

ULAJI

Wataalamu wanashauri pia kwamba mtu asile chakula kibichi kama vile matunda na mboga ambazo hazijamenywa, maziwa ambayo hayajachemshwa na nyama au samaki ambao hawajapikwa. **DW**



Maeneo kama haya ndiyo chanzo cha ugonjwa wa kipindupindu. **PICHA: MTANDAO**



Malezi yanajumulisha pia suala la watoto kuhimizwa kumjua Mungu. **PICHA: MTAND**

# Kuna njia ya lazima ya kulea w

**Inaendelea Uk. 15**

'utakatifu.'

Unaweza kusema kuwa kama ilivyo katika maisha, kuna mvutano usioisha kati ya utamaduni wa sheria na dini unavyokinzana na hitaji la uhuru wa kila mmoja katika jamii, na watoto wanakuwa sehemu ya ukinzani huo kwani ni kielelezo cha mahitaji ya lazima kujisikia una thamani, na mzigo unaosumbua katika suala zima la kuwa huru.

Wanawake kote duniani wamekuwa katika simanzi ya kutambua nini chenye thamani katika maisha, kati ya kazi na familia na hasa kati ya kazi na watoto, na jawabu ni kuwekwa ngazi ya wazi.

Kwanza ni kazi, halafu inafuata familia kwa maana ya kuwa na ndoa (kama unadhifu wa maisha kwa jumla) na watoto mwisho, ukitaka.

Huhitaji kujua historia ya dhana ya dini kujua kuwa huu ni uasi, kwani msingi wa imani katika kuumba ni 'zaeni muongezeke, mkaijaze nchi,' lakini makuhani baadaye wametanguliza ndoa.

Na nchi ikiwa na neema, maisha ya baadaye hayategemei watoto, mwanamke huwa na ndoa ya kujistarehesha bila bughudha ya watoto. Au akizaa mtoto mmoja anadeka, aharibike.

Malezi yana matatizo kwani yamechanganywa na mahusiano

## JE, WAJUA?

# Wanasayansi watengeneza ukungu unaoua 99% ya mbu wa malaria



Mbu jike aina ya Anopheles wanyonyao damu, ambao huua zaidi ya watu 400,000 kwa mwaka. **PICHA: MTANDAO**

UKUNGU (fangasi) ambao umeboreshwa kisayansi kutoa sumu ya buibui, unaweza kuua idadi kubwa ya mbu wanaoambukiza malaria, utafiti mpya wa kisayansi umebaini.

Majaribio ya ukungu huo, ambayo yamefanyika nchini Burkina Faso, Afrika Magharibi, yameonyesha kuwa idadi ya mbu iliteketezwa kwa asilimia 99 ndani ya siku 45.

Watafiti wanasema si lengo lao kutokomeza mbu hao, bali kusaidia kuzuia maambukizi ya malaria.

Ugonjwa wa malaria, unaoambukizwa na mbu jike aina ya Anopheles wanyonyao damu, huua zaidi ya watu 400,000 kwa mwaka.

Duniani kote, wagonjwa milioni 219 wa malaria kila mwaka huripotiwa.

Utafiti huo umefanywa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Maryland cha nchini Marekani na kituo cha utafiti cha IRSS cha Burkina Faso.

Wataalamu hao kwanza walianza kwa kutambua kuvu ama ukungu aina ya Metarhizium pingshaense ambao kiasili hudhuru mbu waambukizao malaria.

Hatua iliyofuatia ilikuwa ni kuuongezea nguvu ukungu huo.

"Kuvu hiyo ni rahisi kuiongezea kitu kisayansi, hivyo ni rahisi kuifanyia uhandisi jeni," anasema Profesa Raymond St Leger, kutoka Chuo Kikuu cha Maryland.

Wanasayansi hao wakageukia sumu itokanayo na aina ya buibui wa funnel kutoka nchini Australia.

Vipimo vya maabara vikathibitisha ufanisi wa kiwango cha juu cha sumu hiyo katika kuteketeza mbu.

Baada ya maabara, wataalamu hao wakatengeneza kijiji maalum kwa ajili ya utafiti nchini Burkina Faso.

Kijiji hicho kilizungushiwa neti ili kuzuia ukungu ama mbu kutoka kwenye eneo la utafiti.

Neti kubwa zilifungwa kwenye kijiji hicho ili kuzuia mbu na ukungu kutoka.

Kisha ukungu huo ukachanganywa na mafuta ya ufuta na kumwagiwa kwenye mashuka meusi ya pamba.

Mbu hao walidhurika punde tu walipotua kwenye mashuka hayo. Watafiti walianza kazi hiyo na mbu 1,500.

Matokeo ya utafiti huo, yaliyochapishwa kwenye jarida la kisayansi yalionyesha kuwa idadi ya mbu inaongezeka kama wakiachwa bila ya ukungu.

Ila, baada ya ukungu wenye sumu kuingizwa kwenye kijiji hicho, walisalia mbu 13 tu baada ya siku 45.

Bwawa la mbu kuzaliana pia liliwekwa kwenye kijiji hicho.

Aina mpya za kupambana na malaria zinahitajika kwa haraka duniani, kutokana na mbu hao kutengeneza usugu wa dawa.

Shirika la Afya Duniani (WHO) tayari limeshaonya kuwa idadi ya wagonjwa itaendelea kuongezeka kwenye nchi 10 ambazo zimeathirika zaidi na malaria barani Afrika. BBC

# RIPOTI

## 'WATOTO MILIONI 280 DUNIANI KOTE WANA MAISHA BORA SASA'



Watoto wakiwa masomoni, ambapo ripoti ya Save the Children inaonyesha kwamba hali za maisha yao zinaboreka. **PICHA: MTANDAO**

RIPOTI kuhusu hali ya watoto duniani iliyochapishwa na shirika la wahisani linaloshughulikia haki za watoto la Save the Children, inaonyesha maendeleo makubwa katika sekta za afya, elimu na usalama katika nchi kadhaa.

Save the Children inasema katika ripoti yake ya kila mwaka kwamba hali ya maisha ya watoto duniani imeimarika katika jumla ya nchi 173 kati ya 176, ambazo ilizifanyia utafiti.

Angalau watoto milioni 280 duniani kote wana maisha bora, ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka 20 iliyopita.

Hata hivyo, ripoti hiyo inaonyesha kwamba robo ya watoto duniani kote bado wananyimwa haki ya usalama na kufurahia utoto, ambapo wengi wanakimbia makazi yao au kukwama katika nchi zilizo na mizozo.

Singapore inashika nafasi ya juu katika viwango vya ulinzi na huduma kwa watoto, ikifuatiwa na mataifa manane ya Ulaya ikiwemo Ujerumani pamoja na Korea Kusini.

Katika nafasi ya mwisho ziko nchi za Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Chad, Mali na Sudan Kusini, licha ya kushuhudiwa maendeleo katika miaka ya karibuni.

Niger ni mojawapo ya nchi iliyopiga hatua kubwa katika kuboresha maisha ya watoto ndani ya miongo miwili iliyopita ikifuatiwa na Rwanda, Sierra Leone, na Ethiopia.

Marekani iko nafasi ya 36 katika ripoti ya mwaka huu, ikiwa sawa na China. Mkurugenzi wa shirika la Save the Children, Carolyn Miles anasema ripoti hiyo ilizingatia viashiria vinane vya ukuaji wa mtoto ikiwa ni pamoja na mtoto kunusurika, elimu, ajira za watoto na ndoa za mapema.

Anasema kwa kulinganisha na mwaka 2000. "Kumekuwa na maendeleo mazuri ukiangalia dunia yote."

Aidha, anabainisha kwamba kiasi ya watoto milioni 420 wanaishi katika maeneo yaliyo na mizozo duniani kote, ikiwa ni mara mbili ya idadi ya mwaka 1995 na takribani watoto milioni 31 hivi leo wamelazimika kuyakimbia makazi yao.

Ripoti hiyo iliyotolewa kuelekea siku ya mtoto duniani ambayo huwa ni Juni Mosi, inakadiria kuwa jumla ya watoto milioni 690 wanaporwa utoto wao kutokana na maradhi, vifo, ndoa za utotoni, mimba za mapema, utapiamlo au kushindwa kuhudhuria shule. Ripoti inabainisha kwamba kwa kulinganisha na mwaka 2000, vifo vya watoto chini ya miaka 5 vimepungua kwa asilimia 49, ajira za watoto, utapiamlo sugu na ndoa za utotoni pia zimepungua kwa asilimia 40.

Ripoti hiyo inasema kati ya viashiria vinane vilivyotumika, kiashiria kimoja kimeonekana kuchomoza zaidi ambacho ni idadi ya watoto wanaoishi katika maeneo yenye mizozo au walioathiriwa na vurugu.

**DW**

# atoto, au ni mazingira tu?

kwa jumla, na wasimamizi wa utamaduni.

Ni hasa ule wa dini, unatilia maanani zaidi mahusiano na siyo malezi. Utasikia mhubiri anampa tahadhari mwanamke mwenye mwenza anayemjali kwa hali zote akae naye mbali kwa kigezo kuwa 'siyo mtu sahihi' kwani ana mke.

Sasa mwanamke huyo akisikiliza ushauri huo akaharibu mahusiano hayo, ni wapi mhubiri atakapomletea mtu mwingine anayejali, pia mwenye uwezo kimaisha kuweza kufuatilia ndoto zake, na papo hapo awe hana mke na ampende hata amwoe? Na hata ikitokea kwa mwanamke mmoja, huwezi kusema ni 'formula' kila mwanamke afuate.

Tatizo ni hisia ya wasimamizi wa utamaduni - na mafundisho lukuki ya taaluma ni 'calibrated,' yaani yametegwa yaendane na yale ya dini, siyo kwa utimilifu wa mafundisho kidhehebu ila kwa hisia za jumla.

Kwa mfano hakuna mtu wa dini atakayemwambia mwanamke 'shikamana na mtu huyo ila usimgombanishe na mkewe.'

Kimsingi hilo ndiyo lingekuwa jibu sahihi, kuwezesha kila mwanamke mwenye jukumu la kuangalia watoto apate mwenza wa kumpa matumaini na hivyo wanae wakue wakijiamini, kuwa mtoto akihitaji kitu kwa mama, akimwambia baba au 'uncle' atamsikiliza.

Siyo lazima huyo 'uncle' afunge ndoa na huyo mwanamke, kutimiza masharti ya utamaduni ambayo mara nyingi yanajitahidi kuchukua sura ya taaluma, kuwa ni 'utafiti,' n.k.



Ujuzi kwa watoto ni muhimu katika malezi

# Sekondari 15 zachuana Dar kumsaka aliyeiva kitaaluma

• Ni waliovuka mchujo wa shule 200 •Mvuto wao; nidhamu, malezi, taaluma

**NA MOSHI LUSONZO**

MALEZI mabaya ya watoto, kutoka kwa wazazi na, walezi, yana mchango mkubwa wa kusababisha idadi kubwa ya watoto kushindwa kuhimili changamoto zinazowazunguka, ikiwamo kufanya vizuri katika mitihani ya kumaliza masomo yao.

Hata Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inasimamia katika hoja hiyo, ikimuwajibisha mzazi kisheria katika kutekeleza jukumu hilo la malezi yanayomuongoza katika njia sahihi, na ulinzi wa usalama wake kiafya na kiusalama.

Ni mtazamo ulioibuliwa katika mjadala uliofanyika hivi karibuni wakati wa fainali ya mashindano ya kitaaluma ya Ramadhan Quiz, yaliyoandaliwa na Taasisi ya An Nahl na kuhusisha shule za sekondari 15 za sekondari, jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Vijana wa Kiislam Tanzania, Hassan Majaliwa, anasema baadhi ya wazazi wameshindwa kutimiza majukumu yao ya malezi, badala yake wanawaacha watoto wafanye wanavyotaka, ili kuwazuia kufanya kazi ambazo zingeweza kuwajenga kiakili na kuwapa hali ya kujiamini.

Anasema, katika miaka ya hivi karibuni malezi ya aina hiyo yamepotea na badala yake watoto wanakuzwa katika mfumo wa kisasa, ambao unawaweka katika hatari ya kutomudu kukabiliana na changamoto za kimaisha.

Anataja baadhi ya mazingira, kwamba kuna watoto wanakuzwa tangu kuzaliwa katika mazingira ya kudekezwa na hawafanyi kazi za kukuza akili zao.

Majaliwa anasema, ni lazima wazazi waanze kujitambua na kuepuka aina hiyo ya maisha, kwa ajili ya kuwapa afya ya akili watoto wao, ili waweze kutambua na kutafutia suluhu changamoto zinakazojitokeza, kufanya vizuri katika masomo yao.

"Kitaalamu malezi mabaya yanamjenga mtoto katika udumavu wa kialiki, kushindwa kumudu mazingira yake kwa kuogopa kukosea na hata anapokuwa shuleni hawezi kutumia akili yake kikamilifu," anasema Majaliwa.

Pia, anashauri kuwapo mfumo rafiki utakaoweza kuwakutanisha wazazi, wanafunzi na walimu katika kujadiliana maendeleo ya mtoto, pale itakapobainika kuna sehemu au hatua haikutekeleza wajibu wake, ielezwe na kujirekebisha.

Majaliwa anapongeza asasi iliyoandaa mashindano hayo, lengo lake ni kuinua ufahamu wa wanafunzi kuhusu masomo yao na mazingira yanayozunguka maisha yao kila siku. "Shindano kama hili ni sehemu ya kuzindua akili za wanafunzi, kwani inawafanya kutumia akili zao kufahamu mambo mbalimbali yanayohusu masomo, dini na mazingira yao," anaeleza.

Pia, anawageukia wanafunzi kwamba ni lazima watambue kuzingatia hadhi na heshima kuanzia kipindi wanachosoma, kupitia wajibu wa kufanya bidii masomoni, ili kukamilisha ndoto zao zitakazowaingiza kirahisi katika soko la ajira, ambalo liko bayana kwamba ni gumu.

"Kama ukisoma kwa bidii na ukafaulu vizuri, uhakika wa kupata ajira utakuwa mkubwa, lakini ukidumaa kutokana na malezi uliyopewa au kwa uvivu tu, itakuwa vigumu kupata kazi," anasisitiza Majaliwa.

Mwenyekiti wa Idara ya Vijana kutoka An Nahl, Ally Mnondwa, anasema mashindano hayo ambayo yanafanyika kila mwaka, yalishirikisha shule 200 za jiji la Dar es Salaam, kati ya hizo 15 ziliingia kwenye fainali.

Washindi na washiriki wa shindano hilo walikabidhiwa zawadi mbalimbali ikiwamo vitabu mbalimbali vya masomo.

Katika shindano hilo, shule ya Al Farook, ilishika nafasi ya kwanza, mshindi wa pili shule ya Al Jebra na wa tatu walikuwa Luqman.

"Lengo la An Nahl kuendelea kufanya shindano hili ni kuhakikisha wanafunzi wanakuwa makini katika kutafuta mbinu mbalimbali za kielimu na katika mazingira yao na kisha kutafuta ufumbuzi wa haraka," anasema Mnondwa.




Baadhi ya wanafunzi kutoka shule 15 wakishiriki mashindano hayo ya kitaaluma. **PICHA: MTANDAO.**

Mmoja wa washiriki, Ahmed Adam, anasema katika shindano hilo amejifunza vitu mbalimbali kutoka kwa wenzake na kumfanya kupanua uwezo wake wa kufikiri na kutambua jambo kwa haraka.

"Tangu nilipoanza kushiriki katika Ramadhan Quiz, nimejifunza mengi na kunifanya akili yangu kupata mwanga juu ya masomo," anasema na kuongeza:

"Nasikitika shule yetu kushika nafasi ya pili lakini mwakani tunaweza kufika mbali kama tukifanya maandalizi ya kutosha."

Anasema katika mfululizo wa shindano hilo amepitia changamoto nyingi, ikiwamo kukabiliana na wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa ufahamu, ambayo inawasaidia kujifunza vizuri hatimaye wameshika nafasi hiyo.

Mwanafunzi, Aisha Suleiman, anaeleza kwamba kwa upande wake amefurahishwa na shindano hilo kwa sababu amekutana na wanafunzi tofauti na kupata nafasi ya kujadiliana masuala tofauti ya kielimu.

"Nimepata nafasi ya kuzungumza na wanafunzi wenzangu na kupeana mbinu mbalimbali za kielimu, japokuwa hatukuingia katika fainali lakini nimepata faida kubwa," anasema.

Hata hivyo, Mnondwa, anasema taasisi yake inaendelea na mkakati wake wa kuwakutanisha wanafunzi wa shule mbalimbali katika program zao tofauti ikiwamo mijadala na makongamano inayowahusisha wanafunzi wanaojiunga na shule za juu na vyuo.




# WADAU SABATO KASIKA

**BAADHI ya wananchi wamekuwa wakijichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga watuhumiwa kiasi cha kuwatia majeraha, wengine vifo. Wadau wanajadili.**




**REHEMA MMANGA (MWANASHERIA, MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

JAMBO la msingi kutambua ni kwamba kujichukulia sheria mkononi ni kosa la Jinai na ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa kuwa mtu anapofanya hivyo, maana yake ni kwamba anazuia vyombo vya dola kufanya kazi zake. Niwakumbushe tu kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, hakuna maana ya neno kujichukulia sheria mkononi, lakini mtu anapojichukulia sheria mkononi, kitendo hicho kinatafsiriwa kwenye sheria hiyo. Vilevile kosa linalotendwa kufuatia vitendo hivyo, wakati mwingine linaweza kuwa tofauti na lingine kulingana na jinsi aliyejichukulia sheria mkononi alivyotenda kosa lenyewe. Ukisoma kifungu cha 225 kujeruhi, kufungu cha 196 kuua, kifungu cha 195 kuua bila kukusudia na kifungu cha 228 kusababisha madhara. Kumekuwa na dhana iliyojengeka ndani ya jamii kuwa mhalifu anapofikishwa kwenye vyombo vya dola, haadhibiwi kama jamii yenyewe inavyotaka na hasa pale inapoona watuhumiwa wakirudi mitaani. Vitendo hivi wapo wengine ambao wanavifanya kwa kufuata mkumbo tu au kushabikia kitu ambacho unaweza kukuta hawakijui, lakini kwasababu wameona wenzao wanafanya, nao wanaingia katika mtego huo. Tuendelee kuwakumbusha Watanzania kwamba kujichukulia sheria mkononi ni kosa la jinai, kwa kukiuka sheria ya kufanya kazi ya kutoa haki ambayo siyo yako unapomwadhibu mtuhumiwa bila kumfikisha katika vyombo vya dola, ambavyo kimsingi ndivyo vyenye dhamana ya kushughulika na wahalifu.



**JONAS MNEMBUKA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA mtu yeyote anayethamini uhai wa mwenzake siyo rahisi kuchukua sheria mkononi. Hata mimi ninachukia tabia hiyo, kwani ninapenda wote tuwe watiifu kwa sheria za nchi na linapotokea tatizo, ni muhimu taratibu za kisheria zikazingatiwa. Kwa watu waliostarabika hawawezi kufanya jambo la aina hiyo kwa kuwapiga hadi kuwaua ama kuwaumiza wengine bila kuwa na uhakika wa makosa wanayotuhumiwa nayo. Hata kama wana makosa wanatakiwa kupelekwa kwenye vyombo vya sheria ili wahukumiwe kulingana na makosa yao, siyo kupigwa tu eti kwa sababu wamefanya makosa fulani ambayo hayajathibitishwa. Inawezekana kweli mtu amefanya kosa la kuiba, au tukio lolote ambalo halifai katika jamii, lakini taratibu zipo, akamatwe na akabidhiwe kwenye vyombo vya dola ili sheria ichukue mkondo wake. Kinachochangia haya yote ni ukosefu wa elimu kuhusu makosa mbalimbali ambayo jamii inatendeana mitaani na badala yake watu wanafanya mambo kwa mazoea tu, na wakisikia kelele za kuitia mwizi, kila mmoja anainuka na silaha yake kwenda kujeruhi au kuua bila kujua huyo mwizi ameiba nini au amesingiziwa. Matokeo unakuta mtu anauawa kwa wizi wa kijiko au kitu kingine kidogo. Vyombo vya dola vijitahidi kutoa elimu kwa umma kutambua hilo ili kuepusha mtindo huu wa kujichukulia sheria mkononi. Ni muhimu kutambua kuwa hakuna mwenye haki ya kuondoa uhai wa mwenzake. Elimu itolewe kwa wingi ili tuondokane na tabia hii mbaya. Kwani ninaamini kwamba kama waathirika wangepelekwa kwenye vyombo vya sheria, hakika wasingepata madhara waliyoyapata kwa sababu huko ingejulikana huyu alilewa na huyu alipotea, lakini siyo wezi.



**MARIAM MJAGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MTINDO wa kujichukulia sheria mkononi ni ushabiki ambao mtu anashabiki jambo bila kujua madhara wala faida yake. Katika mazingira hayo inawezekana wapo waliowahi kuua ndugu zao bila kujua. Vyombo vya dola vilishazuia watu kujichukulia sheria mkononi vikiwa na maana nzuri tu kwamba jamii inatakiwa kumchukua mtu inayemtilia shaka na kumfikisha kunakohusika na pia taarifa zitolewe wahalifu washughulikiwe kisheria. Lakini inasikitisha kuona baadhi ya watu wakiendelea kuumiza wenzao kwa tuhuma za kufanya matukio ya kihalifu. Wanasahau kwamba kila mara Jeshi la Polisi nchini limekuwa likikemea na kutoa onyo kali kwa watu wote wenye mtindo huo wa kujichukulia sheria mkononi kuacha mara moja. Jeshi limeendelea kuchukua hatua kali za kisheria kwa kufuatilia na kuwakamata wote wenye tabia hiyo. Mbali na kuwachukulia hatua za kisheria, pia limekuwa likihimiza jamii kutoa taarifa ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahalifu au mtu yeyote anayetiliwa shaka katika maeneo yao. Kwangu mimi ninaona kwamba hii ni elimu tosha ambayo ingesaidia kumaliza tatizo la watu kujichukulia sheria mkononi. Lakini inasikitisha kuona bado kuna watu kama hawaelewi kitu. Umefika wakati sasa watu wote wakiwamo wenye ushawishi mkubwa katika jamii kusaidia kukemea na kutoa elimu juu ya madhara ya kujichukulia sheria mkononi ili wananchi watambue umuhimu wa kutii na kufuata sheria za nchi zilizopo.



**GEORGE GAMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

TABIA hii ni mbaya sana. Kwa mfano kuna tukio la mwaka 2010 lilitokea Kimara Mwisho, Dar es Salaam. Kijana mkazi wa Goba aliteketezwa kwa moto baada ya watu wasio na huruma kumchoma wakimtuhumu kwa wizi. Waliofanya hivyo walikuwa ni madereva wa bodaboda baada ya kumtuhumu kuiba pikipiki ya mmoja wao. Baadaye ilikuja kufahamika kuwa hakuwa mwizi kama ilivyodhaniwa na madereva hao bali alifika hapo kwa fundi akiwa na pikipiki yake ili atengenezewe na ndipo alipoazima moja ya pikipiki zilizokuwa kwa fundi kwenda kununua mafuta alioagizwa na fundi. Akiwa njiani, mwenye pikipiki alimwona na kuwaambia wenzake na kuanza kumfukuzia akidhani kaibiwa na alipofika Kimara Kona aliegesha na kwenda sheli kununua mafuta. Madereva hao hawakumuona eneo hilo wakaamua kurudi, lakini wakiwa njiani walimwona tena kijana huyo akirudi na pikipiki hiyo akiwa amebeba mafuta na ndipo walipomdhibiti na kisha kuanza kumshambulia, wakammwagia mafuta aliyokuwa amebeba na kumuwashia moto akateketea. Inauma sana tena sana, kijana wa watu alikwenda kwa fundi kutengeneza pikipiki yake, kisha fundi akamuazima mojawapo ya pikipiki alizokuwa akitengeneza, ili akanunue mafuta, lakini matokeo yake akauawa kwa kudhaniwa ni mwizi. Hivi kulikuwa na ugumu gani kumpa nafasi ajieleze? Au walishindwa nini kumfikisha kituo cha polisi ili kujua ukweli? Watanzania tubadilike, tuache mtindo wa kujichukulia sheria mkononi. Jambo hili halihitaji elimu kubwa kulielewa bali tumetawaliwa na tabia mbaya.



**THOMAS NGAWAIYA (MKURUGENZI WA TAASISI YA UTAWALA BORA)**

HAKUNA mtu au chombo chochote kinachoruhusiwa kutoa adhabu ya kosa lolote isipokuwa ni mahakama pekee, kwasababu kisheria mtu yeyote mkosaji anatakiwa kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria ili ushahidi uweze kubaini makosa yake na kutoa adhabu inayostahili. Kwakuwa mambo haya yamekuwa yakiendelea bila kikomo, ninatoa wito kwa vyombo vinavyohusika na ulinzi wa amani pamoja na chombo cha mahakama kuchukua hatua kali ikiwa na pamoja na kuongeza adhabu kali ili mambo haya yasiweze kujirudia. Siyo vizuri jamii kufumbia macho mambo haya. Ni vyema pia wahusika wakaacha mara moja kuchukua sheria mkononi na pia mahakama ziwe zinatoa adhabu kali sana kwa watu wa aina hiyo ili iwe fundisho kwa wengine. Inasikitisha kuona watu wasio na hatia wakiuawa kwa visingizio kwamba wameiba au wana macho mekundu ama aina yoyote ya kosa, kwani kama nilivyosema, mtu mwenye kosa anafikishwa kwenye vyombo vya sheria. Chonde chonde kuchukua sheria mkononi inakatazwa na Katiba ya nchi pamoja na sheria zote. Ombi langu ni kwamba vyombo husika vifanye kazi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa raia kwani inaweza kuwa na mchango mkubwa wa kukomesha vitendo hivyo kwenye jamii yetu ambayo imekuwa ikidhani mtu akiiba au akifanya kosa lolote ni kupigwa na kuuawa.





## Ahadi serikali ujenzi hospitali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI wilayani Mbarali, imesema itahakikisha inasimamia kwa ukaribu ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo, ili kuhakikisha unakamilika kabla ya muda uliotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo.

Mwishoni mwa wiki, Waziri Jafo alikagua ujenzi wa hospitali hiyo na kuagiza ikamilike kabla ya Juni 30 na kuanza kutumika, huku akisisitiza kuwa endapo haitakamilika kibarua cha mkurugenzi kitakuwa kwenye hati hati.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema watahakikisha wanasimamia ujenzi huo usiku na mchana ili kufikia Julai mosi mwaka huu ianze kutumika.

Alisema Serikali Kuu ilileta Sh. bilioni 1.5 mwaka jana na wanakusudia kukamilisha ujenzi huo kwa gharama ya Sh. milioni 900 pekee na kwamba fedha zitakazobaki watazitumia kwenye shughuli zingine endapo serikali itaridhia.

"Jengo lipo lilishajengwa kwa hiyo tunatakiwa kulimalizia na sasa tunaendelea kulikamilisha kwa speed (kasi) kubwa kwa hiyo kabla ya Juni 30 tutakuwa tumekamilisha tena kwa kiwango kinachotakiwa," alisema Mfune.

Kuhusu nyaraka za mradi huo ambazo zilikuwa hazijulikani zilipo, Mfune alisema suala hilo linachunguzwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), na kwamba hawatakiwi kuingilia. Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alisema kwa sasa wanataka jengo hilo linapokamilika na kuanza kutumika kusiwe na changamoto ya makazi.

Alimuomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kulihimiza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kukamilisha haraka nyumba 20 za halmashauri hiyo ili hospitali itakapoanza kufanya kazi watumishi wawe wanaishi kwenye nyumba hizo. Alisema wameweka nguvu nyingi kwenye ujenzi huo, ili ukamilike kwa muda uliopangwa na serikali na kwamba mambo mengine yatafuata baada ya kukamilika.

"Tunazo nyumba za halmashauri ambazo zinajengwa na Shirika la Nyumba, lakini hazijakamilika, hivyo tunamuomba waziri atusaidie kuwahamasisha wenzetu wa NHC, ili wakamilishe haraka na watumishi wa hospitali yetu wakae humo," alisema Msangi.

Mwanzoni mwa Mei mwaka huu, Rais John Magufuli alipokuwa kwenye ziara ya kikazi wilayani Mbarali, aliziagiza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais, na Tamisemi kuhakikisha hospitali hiyo inakamilika.

Rais Magufuli alizitaka wizara hizo kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali kusimamia na kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa maelezo kuwa fedha zipo.

# Alama ya kale ya unyayo wa binadamu yaonekana

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

ALAMA ya unyayo wa binadamu wa kale yaonekana, ukiwa kwenye jiwe kandokando ya moja ya vyanzo vya mto Mbarali, huku ukidaiwa kuwa miongoni mwa vivutio vya watalii ambavyo vinatakiwa kutangazwa.

Alama hizo zilibainika juzi wakati maofisa wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Mpanga – Kipengele iliyopo katikati ya wilaya za Mbarali, Makete na Wanging'ombe walipokuwa wanatoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa wananchi wa maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo.

Wakati wataalamu hao wanawaeleza wananchi wa Igawa wilayani Mbarali kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na baadhi ya vivutio vya utalii, na baadhi ya wananchi waliwaeleza maofisa hao kuwa kuna sehemu kuna nyayo za binadamu juu ya jiwe na maofisa walipoonyeshwa wakabaini kuwa ni kweli.

Pascal Mbendo alisema alianza kuziona nyayo hizo mwaka 1982 wakati anasoma shule ya msingi na kwamba walikuwa hawaelewi kuwa alama hizo zinaweza zikawa kivutio cha watalii.

Alisema baada ya kuelimishwa na maofisa wa hifadhi ya Mpanga-Kipengele ndipo walianza kubaini kuwa ni muhimu na ndio maana wakawaambia maofisa hao kuwa kuna kitu cha aina hiyo, ili wakaangalie na kwamba walipoangalia waliwaambia kuwa ni sahihi.

"Mpaka sasa hatuelewi ilikuwaje mpaka nyayo za mtu huyo zikabaki kwenye jiwe na zimedumu mpaka sasa bila kufutika, kwa miaka yote tulikuwa tunaziona na hatukujua kama ni kitu cha ajabu kuonekana," alisema Mbendo.

Naye Shdrack Mhanga, aliwaomba maofisa wa hifadhi kulizungushia eneo hilo ili kulifanya kuwa miongoni mwa vivutio vya watalii ambavyo vinaweza kuwa na manufaa kwa wakazi wa eneo hilo na taifa kwa ujumla.

Alisema wao walikuwa wanaziona nyayo hizo kama kitu cha kawaida na kwamba walikuwa wanaziona mara kwa mara wanapoenda kuangalia skimu ya umwagiliaji ya Igomelo ambayo walijengewa, lakini hawakutoa taarifa kutokana na kutojua.

Mhifadhi katika hifadhi hiyo, Emmanuel Silayo, alisema tangu muda mrefu walikuwa na taarifa za uwepo wa nyayo kwenye hifadhi hiyo na kwamba walikuwa wanaendelea kuzisaka ili wazifanyie uchunguzi.

Alisema kuonekana kwa nyayo hizo nje ya hifadhi ni kiashiria tosha kuwa taarifa walizokuwa nazo ni sahihi kwa madai kuwa yawezekana aliyekanyaga kwenye jiwe hilo ndiye aliyepita na ndani ya hifadhi.

"Nyayo hizi zinatufanya sasa tuongeze juhudi kuzisaka zingine na tutahakikisha tunaziwekea mazingira mazuri na kuzitangaza pamoja na vivutio vingine vilivyopo ndani ya hifadhi hii ili watalii wavutiwe kuja kuona," alisema Silayo.

Naye Meneja wa Hifadhi hiyo, Alphonce Mng'ong'o, alisema kuwa hifadhi yake inao mkakati wa kuibua vivutio vya utalii ndani na nje ya hifadhi hiyo, ili wavitangaze kwa lengo la kuvutia watalii na kuvifanya vianze kunufaisha jamii na taifa.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (kulia), akipata maelezo ya uandaaji wa kitalu cha maparachichi, wakati wa maonyesho ya Kilimo Biashara, yaliyofanyika jijini Mbeya juzi. Wapili kulia ni Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti (Tari) Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geofrey Mkamilo (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Tari, Dk. Yohana Budeba. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima wapewa somo kiwango ukaushaji mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wameshauriwa kuhakikisha mazao yao yanakauka na kufikia unyevu nyevu wa chini ya asilimia 15 kabla ya kuhifadhiwa, ili kuepuka kutengeneza sumu kuvu ambayo ni hatari kwa afya zao na watumiaji wengine.

Ushauri huo ulitolewa na mtafiti wa mazao kutoka katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) ya Uyole jijini Mbeya, Leonard Sabula, wakati wa maonyesho ya kilimo biashara yaliyoandaliwa na Shirika la Nafaka ukanda wa Afrika Mashariki.

Maonyesho hayo yalifanyika katika eneo la mashamba ya Tari – Uyole na kushirikisha zaidi ya wakulima 1,500 kutoka maeneo mbalimbali ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wanunuzi wa mazao, wasindikaji na kampuni za uzalishaji wa mbegu.

Sabula alisema changamoto inayowakabili wakulima wengi nchini ni namna ya kuhifadhi mazao hayo ambapo alisema wengine wanahifadhi mazao ambayo yanakuwa hayajakauka vizuri.

Alisema hali hiyo inasababisha mazao hayo kutengeneza ukungu ambao ndio chanzo cha sumu kuvu ambayo alidai kuwa ni hatari kwa afya endapo mazao hayo yataliwa.

"Sumu kuvu ina madhara makubwa sana, wakati mwingine inasababisha madhara ya haraka kama iliyowahi kutokea Dodoma, ambapo watu walikufa, lakini nyingine inaathiri taratibu kulingana na kiasi ambacho mtu anakula," alisema Sabula.

Alisisitiza kuwa sumu kuvu pia ndio chanzo cha kansa ya utumbo ambayo inazidi kuongezeka duniani pamoja na aina zingine za kansa zinazoleta madhara.


Meneja Programu wa Baraza la Nafaka ukanda wa Afrika Mashariki ofisi ya Tanzania, Ikunda Terry, aliwataka wakulima kuhifadhi vizuri mazao yao ili yaweze kuuzika hata nje ya nchi na kuwaletea tija.

Alisema endapo mazao yao yatakuwa yamebainika kuwa yameshambuliwa na ukungu wa sumu kuvu, hayatakiwi kuliwa wala kuuzwa na badala yake yanatakiwa kuharibiwa ili kuepuka madhara ya kibinadamu.

Alisisitiza kuwa hata wanyama hawatakiwi kulishwa chakula kinachotokana na mazao hayo kwa madai kuwa nao wataathirika na sumu hiyo ambayo alidai ni hatari.

"Hata kuku akilishwa mazao yenye sumu kuvu bado italeta madhara maana mayai ya kuku huyo yanahifadhi sumu na yakiliwa na binadamu lazima apate madhara ya kiafya ikiwamo kupata kansa," alisema Terry.

Alisisitiza kuwa sumu kuvu inatengenezwa kwenye mazao yote ya nafaka na jamii ya mikunde na kwamba wakati mwingine mazao ya wakulima wa Tanzania yanakosa soko kwa sababu hiyo.





## Wampongeza JPM kupandisha vyeo Zimamoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HATUA ya Rais Dk. John Magufuli kuwapandisha vyeo na kuwateua maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuongoza vitengo mbalimbali, kutasaidia kupunguza malalamiko katika jeshi hilo ya kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu imeelezwa.

Uteuzi wa Rais Magufuli kwa Manaibu Makamishna na Makamishna wasaidizi waandamizi, umeanza toka Juni Mosi, mwaka huu.

Akizungumza wakati akiwavisha vyeo hivyo Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, alisema anamshukuru Rais Magufuli kwa kuwakumbuka jeshi hilo, kwa sababu itasaidia kwa kiasi kikubwa maofisa hao kufanya kazi kwa bidii katika majukumu waliyopangiwa.

Alisema maofisa walioteuliwa wametokea vitengo mbalimbali ambavyo vitawasaidia wao kufanya kazi kwa urahisi katika shughuli za uokoaji zinazotokea katika maeneo mbalimbali.

Akitolea mfano kwa ofisa aliyeteuliwa kutoka Halmashauri ya Bariadi, alisema halmashauri ndizo zinazotoa viwanja, hivyo itasaidia kwa Jeshi la Zimamoto kutoa elimu kwa wananchi ni wapi wanatakiwa kujenga ili kuepusha maafa.

"Namshukuru rais kwa uteuzi alioufanya, ameangalia umuhimu wa kila mmoja katika kitengo alichopangiwa," alisema Kamishna Jenerali Andengenye.

Hata hivyo, alisema kwa wale ambao hawajabahatika katika uteuzi huo, wasikate tamaa waendelee kuchapa kazi kwa sababu Rais na uongozi wa Jeshi hilo ikiwamo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itawaona katika utendaji wao.

Manaibu kamishna waliopandishwa vyeo na kuteuliwa katika vitengo mbalimbali ni ACF Fikiri Salla (Usalama dhidi ya Moto), ACF Maria Kullaya (Mipango, Utafiti na Takwimu), SF Keneddy Komba (Mkuu wa Chuo cha Zimamoto), ASF Chalo Mangare (Usimamizi na Udhibiti wa Viwango), ASF Hamis Rutengo (Ugavi), ASF Gerald Shoo (Fedha na Uhasibu), ASF Bashiri Madhehebi (Maokozi).

Manaibu makamishna wengine ni ASF Athuman Rwahila (Utawala na Rasilimali ), ASF Ully Mbuluko (Usimamizi Uzimaji Moto), ASF Happines Shirima (Usafirishaji na Mawasiliano) na ASF Lusekelo Chaula (Sheria).

Kwa upande wa Kamishna Msaidizi Mwandamizi waliopandishwa vyeo ni ASF Kondo Magoma, ACF Hamis Telemkeni, ACF Abdalah Maundu, SSF Mohamed Jihad, ASF Athuman Basuka, ASF Ivo Ombella, ASF Ambwene Mwakibete, ASF Puyo Nzalayaimisi, ASF Julishael Mfinanga, ASF Yusuph Semtana, ASF Taki Nguzo, ASF Christina Sunga, ASF Elia Kakwembe, ASF Salum Mohamed, ASF Zabrone Muhumha, ASF James John, ASF Goodluck Zerote Urio na ASF Laizer Lokwetikya.

Alisema kinachotakiwa kwa waliopata nafasi hizo kwenda kuzitumia kwa ajili ya maslahi ya taifa ili kuhakikisha wanapambana vilivyo na majanga ya ukoaji.

Akitoa shukrani kwa niaba ya waliopandishwa vyeo ASF James John, alisema wanamshkuru Rais Magufuli kwa dhamana aliowapa na kuahidi kwenda kufanya kazi kulingana na majukumu waliokabidhiwa.

Alisema kuwaamini kwao nao watatumikia vyeo walivyopewa kwa maslahi ya taifa na si maslahi binafsi.

Naye ACF Kullaya, alisema kitendo cha wao kupata nafasi hiyo wataitumia vizuri, ili kuhakikisha wanawasaidia watu katika majanga mbalimbali.

# Serikali kuridhia mkataba wa wafanyakazi majumbani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu imesema serikali itaridhia na kupitisha mkataba wa kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) wa wafanyakazi wa majumbani namba 189 pindi wadau watakapokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mkataba huo.

Hayo yalisemwa jijini hapa na Mkurugenzi Msaidizi Elimu, Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Andrew Mwalwisi, kwa niaba ya Kamishna wa Kazi, wakati akizungumza na wadau mbalimbali wa kupanga mkakati wa kuboresha haki za wafanyakazi wa majumbani. Mwalwisi alisema mchakato wa mkataba huo umefanyika kilichobaki ni kutoa elimu ili waajiri, wafanyakazi na wadau wengine kupata fursa kuuelewe na kuutekeleza kwa urahisi.

Alisema ni bora kuwa na mkataba ambao unatekelezeka kuliko kuridhia, lakini hautekelezeki, serikali imegundua wadau wengi bado hawajauelewa vizuri.

"Tumeridhia mikataba mingi, lakini baada ya kuwa na uelewa wa hali ya juu, serikali inatambua na iko tayari katika suala hilo baada ya kuwa na uelewa mkubwa," alisema.

Mwalwisi aliwataka waajiri kutimiza malengo ya sheria na kuwapa haki wafanyakazi hao kwa mujibu wa sheria, ya kuwalipa mishahara, kulinda haki zao, kupata likizo na kuwapa mikataba.

Awali mratibu wa kanda ya Afrika kutoka shirikisho la vyama vya wafanyakazi duniani, Vick Kanyoka, aliomba serikali kuridhia na kupitisha mkataba huo ili wafanyakazi hao kuwezeshwa kupata haki zao kisheria.

Alisema serikali imekuwa na kigugumizi kwenye suala la kuidhinisha na kupitisha mkataba huo na kusema inatakiwa kukaa pamoja na wadau ili kuzungumzia changamoto za wafanyakazi hao.

Hata hivyo, aliwataka waajiri kusimamia sheria kama zinatekelezeka hususani suala la kutoa mikataba kwa wafanyakazi hao.

Jenipha Sudai, mmoja wa mfanyakazi wa majumbani alisema changamoto wanazokutana nazo ni kukosekana kwa mikataba ya kazi pamoja na kutothaminiwa kama wafanyakazi wengine.

Jenipha alisema hata kama mfanyakazi anaumwa anapatiwa Paracetamol na kuambiwa aendelee na kazi bila kupumzika.



Watoto wa vituo mbalimbali vya kulelea watoto wenye uhitaji maalumu mkoani Dodoma, wakipata futari iliyoandaliwa na kampuni ya QNET, juzi. Zaidi ya watoto 200 walihudhuria hafla hiyo, iliyoongozwa na Sheikh wa Mkoa huo, Mustapha Shaaban na wawakilishi toka Bakwata. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mabaraza ya kata yajengewa uwezo kisheria

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

KITUO cha Amani, Haki na Msaada wa Kisheria Tanzania (PLAJC), chini ya ufadhili wa UNDP kwa ushirikiano na Wizara ya Katiba na Sheria kimeendesha mafunzo ya kisheria ya kuwajengea uwezo mabaraza ya kata ya ardhi na kamati za ulinzi wa mtoto na mwanamke.

Aidha, kituo hicho kimepanga kuwezesha Klabu za Amani na Haki za Binadamu katika shule mbalimbali katika wilaya za Dodoma na Chamwino mkoani hapa.

Katika uanzishaji wa klabu hizo wamelenga kufikia kata 24 na hivyo kuwa na klabu 24, mabaraza ya kata na vitongoji na mitaa na kamati za ulinzi wa mtoto kwa idadi kama hiyo.

Akizungumza wakati wa mafunzo yaliyofanyika sambamba na utoaji wa msaada wa kisheria, Wakili Petro Nziku, kutoka PLAJC alieleza lengo la kufanya mafunzo hayo ni kuwezesha mabaraza hayo kutekeleza majukumu yao vizuri, ili kupunguza changamoto nyingi za kiutendaji na kisheria wanazokutana nazo kila siku.

Wakili Nziku alisema kuwa mafunzo hayo yatasaidia kuhakikisha haki za wanyonge na ambao hawana uwezo wa kuzifikia huduma za kimahakama wanapata msaada wa kisheria katika wilaya za Dodoma na Chamwino mkoani hapa.

Naye Wakili Hussein Asseri, alisema mafunzo hayo yamelenga kutoa uelewa katika maeneo yote ya sheria ikiwa ni pamoja na masuala ya jinai, madai, mirathi na ardhi.

Alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa kuwa mabaraza yamekuwa yakilalamikiwa kushindwa kutekeleza majukumu yao vizuri na wananchi wengi hivyo kusababisha haki za watu wengi kupotea.


Ofisa Maendeleo Mkoa wa Dodoma, Happy Hiza, alisema mpango huo ni mzuri na mafunzo hayo yatasaidia kutekeleza Mpango wa Taifa wa Ulinzi wa Watoto na Wanawake nchini.

Alisema ni matumaini yake kuwa mafunzo hayo yatasaidia kupunguza au kuondoa kabisa ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto mkoani humo kwa waathirika kujengewa uwezo wa ujasiri wa kutafuta msaada wa kisheria.

Aidha, alisema elimu hiyo itawezesha wahusika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia unaoendelea maeneo mbalimbali mkoani humo.

Akifafanua kuhusu uanzishaji wa klabu za amani na haki za binadamu shuleni, alisema umelenga kupata mabalozi wa kueneza ujumbe wa amani katika jamii, na kujifunza masuala mbalimbali yahusuyo ukatili wa kijinsia.

"Hivyo klabu hizi zitamfanya mwanajamii akiwa bado mdogo kuelewa namna ya kujikinga na ukatili wa kijinsia na namna bora ya kutoa taarifa endapo anatendewa ukatili wa kijinsia," alisema.







Mke wa Rais wa Zanzibar mama Mwanamwema Shein, akisalimiana na kuagana na Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Karume, baada ya kumalizika kwa hafla ya futari ilioandaliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, katika viwanja vya Ikulu Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Biashara Zanzibar na Bara yaporomoka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BIASHARA kati ya Zanzibar na Tanzania Bara imeshuka kutoka thamani ya Sh. bilioni 33.66 hadi bilioni 24.29 kutokana na vikwazo visivyokuwa vya kiushuru katika soko la pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2017/2018.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Biashara na Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Balozi Amina Salum Ali, alipokuwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara.

Balozi Amina alisema kushuka kwa bidhaa zinazoingizwa katika soko la Tanzania Bara kumesababishwa na kupungua kwa upelekaji wa bidhaa hasa magari tangu mwaka 2015 na bidhaa zingine zikiwamo za viwandani.

"Mheshimiwa Spika hali hii ilitokana na vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru hasa vibali vya kuingiza bidhaa Tanzania Bara na masuala ya usajili wa bidhaa kabla ya kuingia katika soko la pamoja," alisema.

Kwa mujibu wa Balozi Amina, biashara hizo zinahusisha bidhaa za vyakula, vifaa vya kielektroniki, dawa na vinywaji vinavyozalishwa Zanzibar.

Alisema utafiti wa utambuzi wa vikwazo vya biashara uliofanywa na wizara kwa kushirikiana na Trade Mark East Africa, umeonyesha wafanyabiashara Zanzibar hukumbana na vikwazo vya ukaguzi wa bidhaa za aina moja kwa taasisi za ubora wa viwango. Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), Mamlaka za Chakula na Dawa za Zanzibar (ZFDA) na ile ya Tanzania (TFDA).

"Ni imani yangu kuwa utafiti huu utakuwa chachu ya maendeleo ya kupunguza vikwazo vya biashara vilivyopo baina ya Zanzibar na Tanzania Bara," alisema.

Hata hivyo, alisema uingizaji wa bidhaa Zanzibar kutoka Tanzania Bara unaendelea kuimarika baada ya bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 244.24 kuingizwa katika soko la Zanzibar kuulinganisha na zile za awali zenye thamani ya Sh. bilioni 206.48 mwaka 2017.

Balozi Amina alisema mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa Zanzibar umefikia asilimia 17.8 kutoka asilimia 17.0 sawa na ongezeko la aslimia 0.8 baada ya uzalishaji wa viwandani kuongezeka.

Alisema katika utekelezaji wa mpango wa Zanzibar kuwa na uchumi wa viwanda, viwanda 22 vinatarajiwa kujengwa vikiwamo vya chumvi, mafuta ya majani ya karafuu, nyanya, viberiti na kuchakata minofu ya samaki.

Alivitaja viwanda vingine kuwa ni vya mafuta ya mkaratusi, kukausha dagaa, kusarifu ndimu, vifaranga vya kuku na vingine vitatu vya vifungashio.

Balozi Amina alisema kukua kwa uchumi wa viwanda kutasababisha kuongezeka kwa ukuaji wa uzalishaji katika sekta ya kilimo, kupungua uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi na kuongeza ajira na pato la taifa visiwani Zanzibar.

Katika kuweka mazingira mazuri, ufanyaji wa biashara na uwekezaji, alisema wizara imefanyia mapitio sera ya biashara ya mwaka 2006 kwa kushirikiana na Trade Mark East Africa na taratibu za kuwasilishwa serikalini zinafanyika mwaka huu.

# Utekelezaji uchumi wa kati waanza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeanza kutekeleza rasimi mpango wa Zanzibar kuwa na uchumi wa viwanda kwa kutenga maeneo maalum ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji miradi ya viwanda Visiwani Zanzibar.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alisema jana katika Baraza la Wawakilishi alipokuwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yanayokadiriwa kuwa Sh. bilioni 15.5 kwa mwaka wa fedha wa 2019/20.

Balozi Amina alisema wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi, imetenga maeneo ya Nungwi, Dunga, Nyamazi na Chamanangwe kisiwani Pemba kuwa maeneo ya uwekezaji wa viwanda Zanzibar.

"Mheshimiwa Spika, eneo la Chamanangwe Pemba litakuwa maalum kwa ajili ya viwanda vya usanifu wa mazao ya kilimo, yakiwamo chumvi, mwani na maziwa katika mpango wa Zanzibar kuwa na uchumi wa viwanda," alisema Balozi Amina.

Alisema serikali imeamua kuanzisha Wakala wa Kusimamia na Maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati (Smida) kwa madhumuni ya kuongeza uzalishaji na kuwaendeleza wajasiriamali kupitia viwanda vidogo vidogo Zanzibar.

Alisema wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), imeendelea kuifanyia mapitio Sera ya Maendeleo ya Wajasiriamali Zanzibar, ili kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mitaji na masoko.

Pia Balozi Amina alisema serikali itaendelea kununua karafuu kwa bei ya asilimia 80 ya kuuzia katika soko la nje kutoka kwa wakulima licha ya bei ya karafuu kukosekana utulivu wa bei katika soko la dunia.

Alisema Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) litaendelea kununua karafuu kilo moja daraja la kwanza kwa Sh. 14,000, daraja la pili Sh. 12,000 na daraja la tatu Sh. 10,000 wakati karafuu za kilimo hai zitauzwa kwa Sh. 17,500 kwa kilo moja.

Balozi Amina alisema katika mwaka 2018/19 ZSTC ilipanga kufanya mauzo ya tani 3,250 za karafuu zenye thamani ya Sh. bilioni 58.4 baada ya kununua kutoka kwa wakulima Unguja na Pemba.

# Balozi Iddi ataka uaminifu benki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema uaminifu mkubwa wa watendaji wa taasisi zote zinazosimamia masuala ya fedha unatakiwa ili kuwezesha jamii kujenga imani ya kuwekeza mitaji yao.

Balozi Iddi alisema hayo juzi baada ya futari ya pamoja iliyoandaliwa na uongozi wa Benki ya Afrika (BOA) mjini hapa.

Alisema uaminifu ni silaha kubwa na ya msingi inayoleta msukumo wa kujenga imani thabiti baina ya wateja na taasisi zinayosimamia na kutunza mitaji yao, jambo linalopaswa kuzingatiwa kwa uadilifu uliotukuka.

Kwa mujibu wa Balozi Iddi, ukombozi wa mitaji ya wateja ambayo wakati mwingine hufanywa na watendaji wasio waaminifu, husababisha baadhi ya taasisi kufungwa na mamlaka za serikali baada ya kufilisika.

Hata hivyo, aliwapongeza viongozi na watendaji wa BOA kwa kufanya kazi kwa uadilifu uliosababisha tawi la Zanzibar kuongoza katika utoaji wa huduma za kibenki kulinganisha na matawi ya benki zingine nchini.

Alisema uadilifu huo umemtia moyo na kushawishika kuwa tayari kufungua akaunti ndani ya benki hiyo na kuwashawishi wananchi na watumishi wa taasisi za umma kuitumia fursa hiyo adhimu kwa maslahi yao ya sasa na baadaye.

Kiongozi huyo aliuhakikishia uongozi wa benki hiyo kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa tayari muda wowote kutoa msaada katika kuona malengo ya benki hiyo yanatimizwa kama yalivyopangwa.

Naye Meneja wa BOA Tawi la Zanzibar, Juma Burhan, alisema taasisi hiyo ya fedha imefanya mambo makubwa tokea kuanzishwa kwake Zanzibar miaka mitatu iliyopita kutokana na kuungwa mkono na SMZ na wananchi mbalimbali.

Burhani alisema kipindi hicho cha miaka mitatu kimeiwezesha benki hiyo kutia saini mkataba na SMZ kwa ajili ya kutoa mikopo kwa watumishi wa wizara 10 za serikali hiyo.

# Watu wenye ualbino sasa waomba ulinzi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WATU wenye albinism katika Manispaaa ya Bukoba mkoani Kagera wameomba kuongezewa ulinzi, ili kuondoa hofu ya kufanyiwa vitendo vya ukatili wakati huu kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu wa mwakani.

Walisema uchaguzi unapokaribia wanapata vitisho vya ukatili katika maeneo mbalimbali hali inayowafanya kuishi kwa hofu na kubakia ndani kama hatua ya kujiokoa.

Agusta Agustine, mkazi wa Kata Nshambya, aliiambia Nipashe kuwa matukio ya ukatili dhidi ya ubinadamu hushusha uzalishaji kutokana na kushindwa kujishughulisha na shughuli za kujitafutia kipato, badala yake wao hubakia majumbani kujificha, hivyo kuwa tegemezi.

"Maisha ya hofu yanaingia pale ambapo unasikia sehemu nyingine ndani ya wilaya au nje ya mkoa mtu kama mimi mwenye maumbile ya ngozi kama yangu amefanyiwa ukatili kuondolewa viungo kwenye mwili au kufa kabisa," alisema na kuongeza:

"Jamani tupendane na si hilo tu, kubaki bila kujishughulisha ni kuwa tegemezi kwa kuwa sote watu wazima sasa."

Florence Florian, mkazi wa Mtaa wa Buyekera Kata ya Bakoba, alisema serikali itoe elimu kwa jamii ambayo bado haina uelewa katika masuala ya maumbile ya watu hususan wenye albinism sambamba na kuwaelimisha wenye kuamini ushirikina, ambazo husababisha kuwaondolea uhai binadamu wengine.

Aidha, watu wenye ulemavu wa ngozi waongezewe ulinzi kipindi hiki hadi wakati wa kampeni, na kwamba wanasiasa wasaidie kuielimisha jamii huhusiana na jambo hilo kwa kuwa wanaishi karibu na jamii.

Alisema wanasiasa pia wasaidie kuwapatia elimu waganga wa jadi kuacha imani za kishirikina.

"Endapo viongozi wetu wa dini, wadau na serikali wakiingilia kati kutoa elimu kwa wanasiasa na waganga wa jadi, vitendo vya ukatili dhidi ya wenye albinism vitakoma," alisema Florian.

Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Polisi na ushirikishwaji wa jamii mkoani Kagera, Nsubisi Mwakisambwe, alisema ushirikishwaji wa jamii kwenye masuala ya matukio ya kihalifu na uvunjifu wa amani ni njia mojawapo ya kutatua changamoto.

Mwakisambwe alisema njia hiyo ni msaada pekee wa kujua usalama kwa kila hatua pale inapooneka kuna hali yoyote katika mazingira ya wanajamii hasa wenye ualibinism, jeshi hilo kupitia kitengo cha polisi jamii kipatiwe taarifa.

Alisema mikakati iliyopo ni kutambua idadi kamili ya watu hao na kuwapatia viongozi wa mitaa ambao watakuwa washiriki zaidi katika ulinzi na usalama kwa kuitisha mikutano shirikishi ya kuwapa elimu wanajamii.

Naibu Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Jimmy Kalugendo, alisema wanasiasa wamekuwa walengwa wa kuzaniwa kwamba ni watafutaji kura kwa njia zisizokuwa sahihi na hushirikiana na waganga wa jadi.

"Nafasi ya uongozi inakuja kwa kujinadi kwa wapigakura na kuwatekelezea yale ambayo yanatakiwa na sio vitendo vya kikatili vinavyotolewa taarifa nyakati za uchaguzi," alisema Kalugendo.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Bukoba, Japhet Kanoni, alisema kama halmashauri bado inatakiwa kuwapatia elimu watu hao kujilinda kwenda kwenye maeneo hatalishi nyakati za usiku.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Reliance Insurance, Ravi Shankar (kushoto), akiagana na baadhi ya wageni waliohudhuria hafla ya futari iliyoandaliwa na kampuni hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Sababu watoto kuzaliwa na miguu kifundo zaelezwa

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa watoto, zaidi ya 2,000 nchini Tanzania huzaliwa na ugonjwa wa miguu kifundo (nyayo zilizopinda).

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji kutoka CCBRT, Brenda Msingi, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Msangi alisema kila Juni 3 ni Siku ya Miguu Kifundo Duniani, ambapo mwaka huu maadhimisho yake yalifanyika mkoani Dodoma. Alisema mguu kifundo ni aina ya ulemavu unaotokana na matatizo ya mifupa.

"Ulemavu huu niwakuzaliwa nao na unaweza kumpata mtoto yeyote duniani," alisema.

Aliongeza kuwa hakuna sababu sahihi inayohusishwa na watoto kuzaliwa na miguu ya aina hiyo. Anaongeza kuwa wataalamu wanasema kuna uwezekano mkubwa wa mtoto kuzaliwa hivyo kama wazazi au mzazi mmoja akikuwa na ulemavu huo.

Anaongeza kuwa wataalamu wanasema kila katika vizazi hai 1,000 kuna uwezekano wa kuzaliwa mtoto mmoja au wawili wenye nyayo zilizopinda.

"Takwimu za Tanzania zinaonyesha kuwa watoto 2,500 hadi 2,800 wanazaliwa na hali hiyo kila mwaka," alisema.

Dk. prosper Aute, daktari bingwa wa mifupa wa CCBRT, alisema wapo watoto ambao wanaupata ugonjwa huo kwa kurithi.

Aliongeza kuwa watoto wanaozaliwa na ugonjwa huo wanatibiwa na kupona.

"Mtoto hata akizaliwa leo akagundulika na tatizo anatibiwa matibabu yake ni rahisi na akiwa ana miaka miwili anafanyiwa upasuaji," alisema.

Aliongeza kuwa matibabu yanatolewa bure CCBRT jijini Dar es Salaam na kituo chake kilichopo Moshi. Kwa mujibu wa Dk. Prosper kila mwaka wanawatibu watoto 400 wenye ugonjwa huo.

# Kamati yataka huduma bora mawasiliano

**Na Dege Masoli,** TANGA

KATIBU wa Kamati ya Ushauri ya Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Mkoa wa Tanga (TCRA), Lulu George, ameikumbusha sekta ya mawasiliano juu ya wajibu wao wa kutoa huduma bora kwa wateja.

Lulu alieleza hayo wakati wa maonyesho ya saba ya kibiashara na utalii ya kimataifa yanayofanyika mkoani hapa kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na mambo mbalimbali yanayoendelea kwenye sekta ya mawasiliano.

Alieleza kuwa hiyo inatokana na ukweli kwamba kila mtumiaji wa huduma ya mawasiliano anayo haki ya kulalamika endapo ataona huduma anayoipata siyo stahiki jambo ambalo alidai halitatokea kama sekta hiyo inatekeleza wajibu wake ipasavyo.

Aidha, alielezea mafanikio yaliyopatikana kutokana na watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kiwango kikubwa wamejua haki zao na wapi pa kupeleka malalamiko yao zinapojitokeza changamoto mbalimbali ikiwamo utapeli wa kupitia huduma za simu za mkononi.

"Matukio kama yakutapeliwa yanapotokea huwashauri jambo la kwanza kufikisha taarifa hiyo kwenye vyombo vya dola ili kupewa muongozo husika na wao kama kamati wanapita maeneo mbalimbali kutoa elimu hiyo licha ya changamoto kubwa tunazokutana nazo kwani watumiaji wa huduma hiyo miongoni mwao hawatimizi wajibu wao katika kutafuta habari," alieleza Lulu.

Naye Kaimu Mkuu wa TCRA Kanda ya Kaskazini, Mhandisi Imelda Salum, aliwaonya na kuwatahadharisha watu wanaoweka picha zisizokuwa na maadili zikiwamo za utupu kwenye mitandao ya kijamii kwamba watashughulikiwa ili kukomesha vitendo hivyo kwa kuwa ni kinyume cha mila na tamaduni za Tanzania.

Imelda alisema TCRA kama mamlaka ya udhibiti wanaendelea kufuatilia na kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaofanya vitendo hivyo vya kupiga picha za utupu na kuweka kwenye mitandao.

## Trump, Meya London warushiana maneno

**LONDON, Uingereza**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amewasili Uingereza jana kwa ziara ya kiserikali, akikabiliwa na ukosoaji mkali wa Meya wa Jiji la London.

Trump aliandika ujumbe wa Twitter kabla ya ndege yake kutua London akisema kwamba meya huyo, Sadiq Khan, ambaye amekuwa akipinga kuhusu kukaribishwa kwa hadhi kubwa Rais Trump, amefanya kazi mbovu kabisa.

Trump amemuita meya huyo kuwa mtu aliyeshindwa vibaya kwenye kazi yake.

Rais huyo wa Marekani pamoja na mkewe Melania watakaribishwa na Malkia Elizabeth wa Pili katika kasri la Buckingham baadaye walijumuika kula chakula cha jioni.

Khan kutoka chama cha Labour anaongoza harakati kubwa za kuipinga ziara hiyo ya siku tatu ya Rais Trump nchini Uingereza. Jana, Khan alimtaja Trump kama mtu hatari kabisa kwa dunia ya sasa.

**DW**

## Katazo pombe mifuko plastiki

**KAMPALA, Uganda**

UGANDA imepiga marufuku uuzaji na unywaji wa pombe zinazouzwa kwenye mifuko ya plastiki au viroba ambavyo maofisa wanasema kuwa vina madhara makubwa ya kiafya.

Viroba hivyo vya pombe za spiriti au Konyagi wakati mwingine huwa na kiwango cha kileo cha asilimia 45 kilichokubalika.

Vinywaji hivyo hupendelewa zaidi na wanywaji wenye kipato ya chini kwa sababu huwa vinauzwa kwa bei ya chini, sawa na senti 13 za Marekani.

Watengenezaji wa vinywaji hivyo nchini Uganda sasa watatakiwa kusindika vinywaji vyao kwenye machupa yenye ukubwa wa chini ya mili lita 200.

Waziri wa Biashara na Vyama vya Ushirika nchini humo, Amelia Kyambadde, ameiambia BBC kuwa viroba vilikuwa vinanunuliwa pia na watoto wa shule.

**BBC**

# Watu tisa wauawa katika vurugu Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

WATU tisa wameuawa kwa kupigwa risasi wakati Jeshi la Sudan likiwatawanya waandamanaji waliopiga kambi nje ya Makao Makuu ya Jeshi mjini Khartoum.

Kwa mujibu wa waandamanaji hao, milio ya risasi imekuwa ikisikika na tayari watu tisa wameripotiwa kufa na kadhaa kujeruhiwa.

Vikosi vya usalama vilivyokuwa kwenye magari yaliyobeba bunduki vimetumwa kote katika mji mkuu, wakati waandamanaji wakiweka vizuizi na kuzifunga barabara za mji huo.

Kamati Kuu ya Madaktari wa Sudan ambayo inawaunga mkono waandamanaji awali iliandika kwenye ukurasa wa mtandao wa kijamii wa Facebook kuwa watu wengine watatu wameuawa kwa kupigwa risasi na baraza la kijeshi na kufikisha idadi ya vifo kufikia watano, huku majeruhi wakiwa wengi.

Msemaji wa baraza la kijeshi, Luteni Jenerali Shams El Din Kabbashi, alisema uvamizi huo wa kijeshi uliwalenga wahalifu na kuwa waandamanaji wako salama.

Kabbashi alisema vikosi vya usalama vilijaribu kuwatawanya wahalifu katika eneo la Colomboa karibu na kambi ya maandamano na ndipo vurugu zikaibuka.

Aliongeza kuwa baraza la kijeshi bado linaunga mkono suluhisho la kisiasa na lipo tayari kurejea haraka iwezekanavyo kwenye meza ya mazungumzo kuhusu kuundwa kwa serikali ya kiraia.

Msemaji wa upinzani nchini humo, Shariff Mohammed Osman, alisema: "Haifai, sio vizuri na haikubaliki katika sheria zozote au kanuni zozote kwa wanajeshi wenye silaha nzito kuwakabili raia wasiokuwa na silaha bila kujali vitendo walivyovifanya."

Chama cha Wasomi cha Sudan, SPA ambalo ni kundi lililoanzisha maandamano hayo Desemba, kimesema kuna jaribio hilo la jeshi kujaribu kuuvunja mkusanyiko huo wa waandamanaji unachukuliwa kuwa mauaji ya kinyama na kuwataka Wasudan kushiriki katika "uasi kamili wa kiraia" ili kuliangusha baraza la kijeshi.

Marekani na Uingereza zimetoa wito wa kusitishwa ukandamizaji huo dhidi ya waandamanaji ambao wanawataka viongozi wa kijeshi waliomuondoa madarakani Rais wa muda mrefu, Omar al-Bashir, wakabidhi madaraka kwa utawala wa kiraia.

Sudan imekuwa chini ya utawala wa Baraza la Kijeshi la Mpito toka Rais Omar al-Bashir alipopinduliwa Aprili na waandamanaji wamekuwa wakilazimisha utawala urejeshwe mikononi mwa serikali ya kiraia.

Balozi wa Uingereza Sudan, Irfan Siddiq, amesema alisikia milio ya risasi akiwa katika makazi yake.

Ubalozi wa Marekani mjini Khartoum umesema mashambulizi ya vikosi vya usalama dhidi ya waandamanaji na raia wengine hayastahili na lazima yasitishwe.

The Alliance for Freedom and Change, kundi linalounda vuguvugu la maandamano hayo, limeitisha maandamano na mikutano ya amani kote nchini humo na vizuizi kuwekwa barabarani zikiwamo za mji mkuu Khartoum.

Mazungumzo kati ya viongozi wa maandamano na baraza tawala la kijeshi yamevunjika, baada ya pande zote kushindwa kukubaliana kama serikali ya mpito inayopangwa inapaswa kuongozwa na kiongozi wa kijeshi au wa kiraia.

***DW***



Vikosi vya ulinzi nchini Sudan vimetumia nguvu kujaribu kuwatawanya waandamanaji katika kambi nje ya Makao Makuu ya Jeshi jijini Khartoum, jana. **PICHA:BBC**

# Sketi fupi zawaongezea mshahara wanawake

**MOSCOW, Urusi**

KAMPUNI ya Urusi ya Tatprof, imekosolewa kwa kuwalipa wanawake fedha za ziada ili wavae sketi au gauni zenye urefu usiozidi sentimita tano juu ya magoti wawapo kazini.

Kampuni hiyo ambayo hutengeneza bidhaa za aluminiamu inaendesha kampeni ya "muonekano wa mwanamke" hadi 30 Juni, mwaka huu.

Wafanyakazi wanawake wanaovaa sketi "ambazo zina urefu usiozidi sentimita tano juu ya magoti" wanalipwa dola za marekani 1.50, zaidi ya mshahara wao wa kawaida.

Ili kupata pesa hizo za ziada, wanawake wanatakiwa kutuma picha zao kwa kampuni hiyo.

Watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii wameonyesha kukasirishwa na kitendo hicho, huku baadhi wakielezea hatua ya kampuni kuwa "udhalilishaji mkubwa wa wanawake".

Blogi maarufu inayoendesha harakati za wanawake na mwandishi wa habari maarufu nchini humo, Zalina Marshenkulova wameelezea hatua hiyo ya kampuni ya Tatprof kama "taarifa ya enzi ya zamani" kwenye ukurasa wa Instagram.

Kampuni hiyo, ambayo mwaka 2014 iliuza bidhaa za michezo ya Olyimpiki ya majira ya baridi katika mji wa Sochi na Kombe la Dunia la mpira wa miguu mwaka jana, imeviambia vyombo vya habari vya Urusi kuwa, inakana shutuma za ubaguzi wa kijinsia na kueleza wanawake 60 tayari wameshiriki katika kampeni zao.

"Asilimia 70 ya wafanyakazi wa kiwanda chetu ni wanaume. Aina hizi za kampeni zinatusaidia kupumzika. Hii ni njia ya kuifanya timu ya wafanyakazi iwe na umoja.

"Wanawake wengi huvaa suruali kazini, ndio maana tunatumaini kampeni yetu itawaelewesha wanawake na kuwaruhusu kujihisi ni wanawake na wenye furaha wanapovaa sketi au gauni." Msemaji wa kampuni hiyo, Govorit Moskva amesema akihojiwa na kituo cha radio.

***BBC***

## Pasipoti za zamani sasa kubadilishwa kabla Julai

Na Salome Kitomari

IDARA ya Uhamiaji nchini imewataka Watanzania wenye pasi za kusafiria za zamani na wanakusudia kusafiri nje ya nchi kuzibadili kabla ya Julai, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na kusainiwa na Msemaji wa Idara ya Uhamiaji nchini, Ally Mtanda, yenye kichwa cha habari kusitishwa kwa matumizi ya pasipoti za zamani zinazosomeka kwa mashine ifikapo Januari 3, 2020.

Taarifa iliyopo ilisema kuwa ni vyema wananchi wakabadili kabla ya Julai, ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza wa kucheleweshwa katika viwanja vya ndege na vituo vya mipakani wakati wa kutoka nchini.

"Ni hitajio la kisheria kwa pasipoti kuwa na angalau uhai wa kuanza miezi sita ili mwenye pasipoti hiyo aweze kuomba Visa ya nchi anayokwenda na kuruhusiwa kuondoka nchini kupitia vituo vya kuingia na kutoka nchini," alisema.

Alisema Idara ya Uhamiaji nchini imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya utaoji wa huduma ya pasipoti mpya katika miaka 29, Ofisi ya Uhamiaji makao makuu, Ofisi Kuu ya Uhamiaji Zanzibar na balozi 23 zilizopo nje ya nchi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, nchi zitakazofunguliwa mfumo huo hivi karibuni ni Afrika Kusini, Msumbiji na Zimbabwe.

Alisema balozi zilizobaki kazi ya ufungaji mitambo ya huduma hiyo inaendelea na itakamilika kufikia Julai, mwaka huu.

Mtanda alisema matumizi ya pasipoti za zamani yatasitishwa ifikapo Januari, mwaka 2020.

**"Ni hitajio la kisheria kwa pasipoti kuwa na angalau uhai wa kuanza miezi sita ili mwenye pasipoti hiyo aweze kuomba Visa ya nchi anayokwenda na kuruhusiwa kuondoka nchini kupitia vituo vya kuingia na kutoka nchini," alisema.**

# Kunyongwa hadi kufa kisa mauaji Scolastica

INATOKA UK. 2

kwa kukusudia bali baada ya kupokea simu kutoka kwa mshitakiwa wa kwanza walienda katika eneo la tukio na kushauriana kuutupa mwili wa marehemu" alisema Jaji.

Alisema kulingana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo, mahakama hiyo imewafutia kosa lililokuwa likiwakabili la kuuwa kwa kukusudia mshitakiwa wa pili na tatu lakini imewatia hatiani kwa kosa la kushiriki jinai baada ya tukio la mauaji chini ya sheria namba 213 kifungu kidogo cha 16 ya sheria ya Adhabu.

Aliongeza kuwa, kosa walilotiwa hatiani nalo linaadhabu ya kifungo kisichopungua miaka saba jela lakini kutokana na maombi yaliyotolewa na mawakili wao mahakama imewahukumu kutumikia kifungo cha miaka minne jela.

Katika hukumu hiyo, Jaji Matogolo alisema mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo, Hamisi Chacha ambaye ni mlinzi wa shule hiyo ametiwa hatiani kwa kosa la mauaji ya kukusudia.

**WAWILI JELA MIAKA MINNE**

Mshtakiwa wa pili, Edward Shayo maarufu kama 'King Size' na mshtakiwa wa tatu, Laban Nabiswa ambaye ni Mwalimu wa Nidhamu wa Shule hiyo, wao wametiwa hatiani kwa kosa la kushiriki jinai baada ya tukio la mauaji hayo.

Jaji Matogolo wakati anatamka ushiriki wao katika kesi hiyo, alisema mahakama imewafutia kosa la mauji ya kukusudia mshtakiwa wa pili na wa tatu lakini imewatia hatiani kwa kosa la kushiriki jinai.

Mwanafunzi huyo anadaiwa kuuawa usiku wa Novemba 6, 2017 na baadaye mwili wake kutupwa Mto Ghona, uliopo umbali wa takribani mita 300 kutoka katika shule hiyo.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa mfululizo katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi, kuanzia Aprili 2 hadi 16 mwaka huu na kisha kuahirishwa kwa muda hadi iliapoanza kusikilizwa tena Aprili 16 hadi Aprili 29 na baaade kuanza teana hadi Mei.

Vielelezo vilivyopokewa na mahakama ni pamoja na panga linalodaiwa kutumika katika mauaji hayo, ripoti ya uchunguzi wa kifo iliyotolewa na daktari pamoja na ile ya vinasaba (DNA) kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Ripoti ya DNA (sampuli za vinasaba) ilitolewa na shahidi wa 12 kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Hadija Mwema ikieleza sampuli zilizochukuliwa kwenye mwili wa Humphery zilioana na zile za baba yake, Jackson Makundi na mama, Joyce.



Vielelezo vingine ni ripoti ya mawasiliano ya simu zinazodaiwa kuwa za washtakiwa pamoja na maelezo ya ungamo ya mshtakiwa wa kwanza (Chacha) anayodaiwa kuyatoa kwa mlinzi wa amani, Novemba 20, 2017.

Pia simu za washtakiwa zilipokewa kama vielelezo. Kabla ya kupokewa kwa maelezo hayo, mahakama hiyo iliingia katika hatua ya kesi ndani ya kesi ili kujiridhisha kama uchukuaji wake ulifuata sheria na iwapo mshtakiwa aliyatoa kwa hiari.

**USHAHIDI WA CHACHA**

Mshtakiwa Chacha alipoanza kutoa ushahidi akiongozwa na wakili wake David Shillatu, alieleza siku ya tukio aliingia kazini saa 11 jioni na kutoka saa 12 asubuhi siku iliyofuata.

Alieleza kuwa saa mbili usiku, kuna mtu alikurupuka jirani na ukuta wa shule na kukimbilia uraiani, lakini hakumfahamu na wala hakumkimbiza kuelekea uraiani alikokuwa amekimbilia.

Alikiri kuwasiliana na washtakiwa wenzake siku hiyo saa tatu usiku, lakini aliwapigia simu kuwaeleza juu ya mtu aliyemkurupusha na si kuwaita katika eneo la tukio kama inavyodaiwa.

Kwa mujibu wa shahidi huyo, alikamatwa na polisi Novemba 17, 2017 saa 11 jioni na kudai kwamba aliteswa hadi Novemba 19, 2017 akilazimishwa kukiri kuua na pia awaunganishe washtakiwa wenzake.

**MAELEZO YA UNGAMO**

Katika maelezo hayo ya ungamo yaliyosomwa mahakamani neno kwa neno, ilidaiwa Chacha alieleza mbele ya mlinzi wa amani kuwa Novemba 6, 2017 saa 2:58 usiku, alisikia kishindo cha mtu akishuka.

Anadaiwa kueleza kuwa alimulika tochi kuelekea eneo hilo na mtu huyo alianza kukimbia na yeye kumkimbiza na kwa vile alikuwa na silaha aina ya panga, alimpiga nalo kwa ubapa.

"Nilimpiga bapa mgongoni na aliendelea kukimbia, nikakimbizana naye na kuna sehemu alifika na kuanguka chini na alipasuka kwenye paji la uso, baada ya hapo akawa katulia.

"Nikampiga bapa la pili na ndio mauti yalipomkuta palepale. Nilimpigia simu mwalimu Laban nikamwambia kuna mtu nimemkimbiza lakini sijui kama ni mwanafunzi au mtu wa nje"

"Ndipo mwalimu Laban ambaye ni mwalimu wa nidhamu akaja. Palepale akaniuliza nimeshampigia mkuu wa shule nikamjibu kuwa nilishampigia mzee wa shule mzee Shayo anakuja.

"Baada ya hapo nilimwambia mwalimu Laban inawezekana huyu mtu kazirai tumbebe tumpeleke hospitali mwalim Laban akadai tumsubiri Mzee Shayo afike. Mzee Shayo alivyofika ndio nikamueleza.

"Mzee Shayo akamuuliza mwalimu Laban unamfahamu huyu mtu Laban alijibu naona kavaa sare za shule lakini siwezi kumfahamu kwa muda huu," ananukuliwa mshtakiwa katika maelezo hayo.

"Mzee Shayo akasema kama humfahamu kwa muda huu (mwili) ukatupwe huko mtoni labda ni kibaka na mimi na mwalimu Laban tulienda kumtupa huko mtoni," anadaiwa kueleza Chacha.

"Tulivyomaliza kumtupa nilimwambia Laban nenda uitishe rokoo (roll call) labda ni mwanafunzi. Akaitisha roll call. Laban alinipigia simu wanafunzi wote wapo na mimi nilirudi ndani ya fence (uzio)"

**MAHAKAMA YAONA WANA KESI**

Mei 3 mwaka huu, iliwaona washtakiwa wote watatu katika kesi ya mauaji ya kukusudia ya mwanafunzi wa Sekondari ya Scolastica, Humphrey Makundi, wana kesi ya kujibu.

**Imeandikwa na Godfrey Mushi na Paul William**

# Tril 9.7/- kulipa deni la taifa

inatoka uk. 2

miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la tatu la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, ujenzi wa miradi ya umeme, barabara na madaraja makubwa.

Alisema pamoja na ukopaji, wizara imeendelea kufanya tathmini ya deni la taifa kwa mwaka ili kupima uhimilivu wake.

Matokeo ya tathmini iliyofanyika Desemba, mwaka jana, alisema yanaonyesha deni hilo ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

"Viashiria katika tathimini hiyo vinaonyesha kuwa thamani ya sasa ya deni kwa pato la taifa ni asilimia 27.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70," alisema.

Dk Mpango alisema: "Thamani ya sasa ya deni la nje pekee kwa Pato la Taifa ni asilimia 55 ya sasa ni asilimia 157.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240 na ulipaji deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa za nje ni asilimia 15.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23."

Waziri huyo aliongeza kuwa serikali imeendea kuhakikisha inalipa deni kwa wakati kwa kadri linavyoiva na kwamba katika mwaka huu wa fedha, serikali ilitenga Sh. trilioni 1.41 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani.

"Hadi kufikia Aprili mwaka huu, kiasi cha Sh. trilioni 1.06 kimelipwa sawa na asilimia 75.18 ya lengo. Serikali pia ilitenga Sh. bilioni 588.30 kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la nje," alisema.

Dk. Mpango alisema wizara itaendelea kusimamia Deni la Serikali kwa kuzingatia sheria ya mikopo, dhamana na misaada Sura 134 pamoja na mkakati wa muda wa kati wa kusimamia madeni.

Aprili mwaka jana, Dk Mpango aliwaambia waandishi wa habari bungeni jijini Dodoma kuwa wizara yake imekuwa ikishindwa kutoa fedha kutekeleza miradi ya kisekta kutokana na kiasi kikubwa cha makusanyo kuelekezwa kulipia Deni la Taifa na mishahara ya watumishi wa umma.

Alibainisha kuwa kila mwezi, serikali hutoa wastani wa Sh. bilioni 550 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa umma na Sh. bilioni 600 kulipia Deni la Taifa na kwamba kuna kipindi wanalazimika kulipa hadi Sh. bilioni 900 kwa mwezi kulipia Deni la Taifa kulingana hatifungani zinazoiva.

Ukurasa wa 177 wa kitabu cha hotuba ya waziri huyo iliyosimwa bungeni jana, kinaonyesha kuwa katika mwaka huu wa fedha, wizara hiyo iliidhinishiwa Sh. trilioni 9.226 kwa ajili ya Deni la Taifa. Hadi kufikia Aprili mwaka huu, Sh. trilioni 7.014 zilikuwa zimetumika.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NAFASI ZA KAZI

**SALES LADY ANAHITAJIKA,** SALES LADY ANAHITAJIKA MWENYE UZOEFU WA COMPUTER, MITANDAO YA KIJAMII INSTAGRAM NA FACEBOOK. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NAMBA: 0715 88 55 33

**NAFASI ZA KAZI,** IT - DIPLOMA anahitajika kidato cha nne na sita. MESSENGER kidato cha nne na sita. Mawasiliano: 0715 885533.

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ELISABERTH MARIA STEGMAIER,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari ya kampuni ya makoa farm limited yenye tin no, 101339645. Yenye namba za usajili T 228 AAJ aina ya Toyota Landcruiser.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: BNG/RB/2083/2019.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**VUMILIA CHRISTOPHER YAHYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 977 DKW TOYOTA PASSO.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DAR/OST/RB/25284/2019.**

115258502

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.41 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late of Dodoma City FRANCIS LYAMBO MWAISELA**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by ROIDA G. LWENGE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before 12th /06/2019.

Dated at Dodoma this ….31st /05/2019

115259602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi No; **120/2019**

Ombi la **PATRICK OSCAR KILLIWE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu O**SCAR KARATTA SHEMGHANGA KILLIWE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 3/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/06/2019..

115259502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ISABELLA MALULA KOMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 226 DFG TOYOTA RAV 4.** Chassis namba ZCA250002531 na Engine namba IZZ0687361.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KW/RB/19.**


## GOROFA INAUZWA



**BOKI KAMWANGA STR LOW DENSITY AREA BLOC "C", PLOT NO. 65**


**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

## CHETI KIMEPOTEA



**DR. MUTABAAZI JULIUS LUGAZIYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.115/0073** kilichotolewa na **KAHORORO SEKONDARI,** BUKOBA mwaka 1980. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **CD/RB/3096/2019.**

## KUPOTELEWA NA PASIPOTI



**HASSAN MOHAMED** anatangaza kupotelewa na pasipoti yake ya kusafiria yenye Namba. **AB647134** aliyopewa na Idara ya Uhamiaji. Alipotezea maeneo ya Pongwe, January, 2018.
Amefika Polisi kutoa taarifa na kupewa Loss Report **TAN/RB/2162/2018**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**JUSTINE FRANCIS MRAWA**
Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye **No, AB 647445** iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji mwaka 2014.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi:
**RB NO MOS/RB/6058/17.**

## CHETI KIMEPOTEA



**ANASTELA KAJWAHULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha UALIMU chenye index namba **E528/003** kilichotolewa na TANDALA T.T.C mwaka 1990.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DAW/RB/680/19.**


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## NEYMAR AKANA KUBAKA

**SAO PAULO, Brazil**

NYOTA wa Brazil na Paris Saint-Germain, Neymar, amekanusha madai ya kumbaka mwanamke mmoja hotelini Paris.

Kwa mujibu wa ripoti ya polisi iliyowasilishwa mjini Sao Paulo, mwanamke huyo amedai kwamba shambulio hilo lilifanyika katika hoteli moja katika mji huo ambapo Neymar anaichezea Klabu ya Paris St Germain.

Neymar ameamua kutoa utetezi wake kwa kurekodi video na kuonyesha kile alichokiita mfululizo wa ujumbe wa WhatsApp baina yake na mwanamke huyo.

Neymar kwa sasa yuko nchini Brazil kwenye kambi ya timu ya taifa katika maandalizi ya Kombe la Copa America.

Kulingana na ushahidi wa polisi, mwanamke huyo ambaye jina lake halijatajwa alijuana na Neymar kupitia mtandao wa Instagram na Neymar akashauri wakutane Paris.

Alimtumia tiketi ya ndege kutoka Brazil kuelekea Ufaransa mbali na kumlipia chumba cha kulala katika hoteli ya kifahari ya Sofitel Paris arc Du Triomp.

Neymar mwenye umri wa miaka 27, amerekodi video yake ya kujitetea na tuhuma hizo katika ukurasa wake wa Instagram.

Mchezaji huyo ambaye hajaoa ameambatanisha video hiyo na maelezo kuwa: "Kutokana na kulazimishwa kutoa fedha, nalazimika kuanika maisha yangu na ya familia yangu."

"Kilichotokea siku ile kilikuwa na faragha ya wapenzi wawili, yalikuwa ni mahusiano ya mwanaume na mwanamke ndani ya kuta nne. Siku ya pili hakukuwa na mengi yaliyotokea. Tuliendelea kutumiana ujumbe kwenye simu, akaniomba nimtumie zawadi (ya mtoto wake)," alisema Neymar.

Katika video hiyo Neymar ameonesha msururu wa kile alichokiita ujumbe wa simu baina yao na mpaka picha za msichana huyo akiwa amevalia nguo zake za ndani tu.



# LACAZETTE

## AONEKANA MITAA YA BARCELONA

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Alexandre Lacazette, ameonekana katika mitaa ya Jiji la Barcelona juzi na kuibua maneno kwamba kuna uwezekano wa kusajiliwa katika klabu hiyo.

Baada ya kuonekana huko, ndio wadau wa soka wakadai kwamba Lacazette huenda ametua kukutana na viongozi wa klabu ya soka.

Barcelona inajulikana inasaka mshambuliaji miongoni mwa mastaa akiwamo Lacazette ambaye amepachika mabao 19 katika mechi 48 ambazo ameichezea Arsenal msimu wa 2018/19.

Klabu hiyo inatafuta mbadala wa Luiz Suarez, ambaye umri unazidi kumtupa mkono akiwa na umri wa miaka 32.

Ili kumpata mshambuliaji huyo, Barcelona itapaswa kupanga bajeti ya kiasi cha pauni milioni 57.

Hata hivyo, taarifa zinasema kuwa fowadi huyo yupo kwa mapumziko katika mji wa Barcelona baada ya kumalizika kwa msimu.

# Kipigo bondia Joshua chamuibua Wilder

**NEW YORK, Marekani**

BONDIA wa uzito wa juu kutoka nchini Marekani, Deontay Wilder, ameshindwa kuficha hisia zake juu ya pambano la juzi ambapo bondia Anthony Joshua alinyukwa na Andy Ruiz Jr.

Ulimwengu wa masumbwi kwa muda sasa umekuwa na shauku kubwa ya kushuhudia pambano baina ya Wilder na Joshua ambaye ni Muingereza mwenye asili ya Nigeria.

Pambano hilo la mabondia hao wawili ambao mpaka juzi wote walikuwa hawajawahi kupigwa, limekuwa likipigiwa upatu kama mpambano mkali zaidi wa ndondi za uzani wa juu kuwahi kutokea katika miaka ya hivi karibuni.

Hata hivyo, Wilder mara kadhaa amekuwa akimtuhumu Joshua kwa kuzuia pambano hilo kwa kutengeneza vikwazo lukuki ili wasikutane ulingoni.

Kutokana na tuhuma hizo, haishangazi namna ambavyo Wilder amepokea matokeo ya ushindi wa Ruiz Jr dhidi ya Joshua.

Kupitia ukurasa wake wa twitter, Wilder maarufu kama Bronza Bomber ameandika: "Hakuwa bingwa wa kweli. Maisha yake yote ya ndondi yalikuwa yametawaliwa na uongo, kujichanganya na zawadi. Sasa tunajua ni nani ambaye alikuwa anamkimbia mwenzake."

Katika pambano hilo lililopigwa jijini New York, Joshua alilambishwa sakafu mara nne na Ruiz Jr kabla ya mwamuzi kuvunja pambano katika raundi ya saba.

Kwa ushindi huo, Ruiz ambaye hakupigiwa upatu kabla ya pambano amemvua Joshua mikanda mitatu ya ubingwa wa WBA, WBO na IBF.

Pambano hilo ni la kwanza kwa Joshua kupigwa, ameshinda mapambano yote 22 kabla.

Kilichompata Joshua kinalinganishwa na kilichowakumba mabingwa wa zamani Lennox Lewis na Mike Tyson ambao pia waliwahi kupigwa na wapinzani ambao hawakupigiwa upatu na kuzua mshangao mkubwa kwenye ulimwengu wa masumbwi.

Tyson alitandikwa na James 'Buster' Douglas mwaka 1990, na Lewis alichapwa na Hasim Rahman mwaka 2001.

Bondia mwingine anayewekwa kwenye mizani sawa ya ubora na makali na Wilder na Joshua kwa sasa ni Tyson Fury.

Wilder na Fury walizichapa Desemba Mosi, mwaka jana japo pambano hilo liliisha kwa sare, wachambuzi wengi wanaamini Fury alinyimwa ushindi wa wazi.

Fury ambaye pia ni raia wa Uingereza hajaonyesha kusherehekea kupigwa kwa Joshua.

Badala yake amemtumia salamu kupitia ukurasa wake wa Twitter akimwambia vitu kama hivyo (kupigwa) ni vya kawaida na amemtaka kunyanyuka na kujipanga upya.

Promota wa Joshua Eddie Hearn ametangaza kuwa bondia wake atarejeana na Ruiz kabla ya mwaka kuisha kwenye Novemba ama Desemba jijini London.

Hearn amebainisha kwa sasa mazungumzo yoyote ya kuzipiga dhidi ya Fury ama hata Wilder yamesitishwa.

## HABARI MICHEZO



# WENGER: LIVERPOOL MARA ZOTE YA MIUJIZA

**LONDON, England**

ARSENE Wenger anaamini kwamba, mara zote Liverpool inafanya miujiza baada ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya kocha, Jurgen Klopp.

'Wekundu' hao walitwaa taji lao la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuifunga Tottenham mabao 2-0 mjini Madrid Jumamosi kwa mabao ya Mohamed Salah na Divock Orig.

Liverpool ilitinga fainali baada ya kupindua matokeo ya Barcelona ambao katika mchezo wa kwanza walishinda 3-0 kabla ya kuchapwa 4-0 kwenye Uwanja wa Anfiled.

Na sasa kocha wa zamani wa Arsenal, Wenger amebainisha kwamba, Liverpool walifanya muujiza na hilo ni kawaida kwao.

"Liverpool ni jiji la muziki, lenye watu wa daraja la juu na wanaopenda mpira wa miguu. Tumeona mfano usiku wa Jumamosi, walionyesha kile ambacho wengi hawakukitarajia," amesema Wenger akinukuliwa na beIN Sports. "Kwa mtu yeyote aliyefundisha soka England anajua kwamba Liverpool ni sehemu maalumu kwa soka na ndio mara zote wanaweza kufanya maajabu."

Liverpool pia walitinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na wakifungwa na Real Madrid mabao 3-1 mjini Kiev.



# Rais Caf auitia kikao ubingwa Esperance

**CAIRO, Misri**

RAIS wa Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), Ahmad Ahmad, ameitisha kikao cha dharura cha Kamati ya Utendaji ya shirikisho hilo kufuatia sintofahamu katika mchezo wa pili wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mei 31, mwaka huu nchini Tunisia kati ya wenyeji Esperance de Tunis na Wydad Casablanca ya Morocco, mchezo uliisha kwa sintofahamu kufuatia Klabu ya Wydad kugomea kuendelea na mchezo baada ya bao lao la kusawazisha kukataliwa katika dakika ya 62 ya mchezo.

Taarifa ya Caf imesema kuwa kikao hicho kitafanyika leo Jumanne, ambapo ajenda kuu itakuwa ni juu ya sheria zanazopaswa katika kutatua sintofahamu ya mchezo huo.

Kwenye mchezo huo, Wydad walisawazisha bao, ambalo lingeufanya mchezo kuwa sare ya 1-1, lakini mwamuzi alikataa bao hilo na halikurudiwa katika teknolojia ya usaidizi wa video VAR kwa kile mwamuzi alichodai kuwa mashine kuharibika.

Baada ya Wydad kugoma kuendelea na mchezo, mwamuzi alimaliza mchezo na kuipa ushindi wa bao 1-0 Klabu ya Esperance pamoja na ubingwa wa michuano hiyo.

# MESSI, RONALDO
## NDANI KIKOSI CHA UEFA 2019

**MADRID, Hispania**

LIONEL Messi na Cristiano Ronaldo wote wamejumuishwa kwenye kikosi cha Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya kushindwa kufika fainali.

Ronaldo na Juve walifika robo fainali kabla ya kutolewa na Ajax, huku Barca ilitolewa na Liverpool kwenye hatua ya nusu fainali.

Messi ambaye ana mabao 12 ndio ametwaa tuzo ya mfungaji bora wa michuano hiyo msimu wa 2018-19.

Baada ya kufika nne bora, Ajax imetoa wachezaji watano kwenye kikosi hicho ambao ni Matthijs de Ligt, Frenkie de Jong, David Neres, Hakim Ziyech na Dusan Tadic ambao walipoteza kwenye nusu fainali na Tottenham ambayo imetoa wachezaji Jan Vertonghen, Lucas Moura na Moussa Sissoko.

Washindi wa kombe hilo, Liverpool imetoa mabeki watatu kwenye kikosi hicho, Trent Alexander-Arnold, Andy Robertson na Virgil van Dijk pamoja na Georginio Wijnaldum, Sadio Mane na golikipa Alisson.

Uchaguzi huo umefanywa na kamati ya ufundi ya shirikisho la vyama vya soka barani Ulaya (Uefa), pia wamemjumuisha kiungo wa Lyon, Tanguy Ndombele na wakali wa Manchester City, Kevin De Bruyne na Raheem Sterling.

Miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Ufundi ya Uefa ni pamoja na Kocha Mkuu wa Ubelgiji, Roberto Martinez, Kocha wa England, Gareth Southgate na bosi wa zamani wa Manchester United, David Moyes.

Kikosi kamili cha Ligi ya Mabingwa Ulaya:

Alisson (Liverpool), Marc-Andre ter Stegen (Barcelona); Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Matthijs de Ligt (Ajax), Andy Robertson, Virgil van Dijk (wote Liverpool), Jan Vertonghen (Tottenham); Kevin de Bruyne (Manchester City), Frenkie de Jong (Ajax), Tanguy Ndombele (Lyon), David Neres (Ajax), Moussa Sissoko (Tottenham), Raheem Sterling (Manchester City), Georginio Wijnaldum (Liverpool), Hakim Ziyech (Ajax); Sadio Mane (Liverpool), Lionel Messi (Barcelona), Lucas Moura (Tottenham), Cristiano Ronaldo (Juventus) na Dusan Tadic (Ajax).



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI NDIYE ATATWAA BALLON D'OR - VAN DIJK

●●● Nadhani bado ni mchezaji bora duniani, anastahili hili kwa kuwa bado anacheza, si kitu ambacho ninakiwazia ila kama itatokea...

**Liverpool, England**

Virgil van Dijk amesisitiza kuwa Lionel Messi anapaswa kushinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia wa Mwaka ['Ballon d'Or'] licha ya yeye kuisaidia Liverpool kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi ya fainali dhidi ya Tottenham jijini Madrid Jumamosi iliyopita.

Beki huyo wa kati, Van Dijk alitangazwa mchezaji bora wa mechi, wakati kikosi hicho cha Jurgen Klopp kikitwaa kombe kufuatia kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Tottenham katika Uwanja wa Wanda Metropolitano.

Liverpool ilikuwa mbele ndani ya dakika mbili kupitia bao la mkwaju wa penalti uliozamishwa kimyani na Mohamed Salah, lakini shukrani ziliwaendea zaidi Van Dijk na kipa Alisson kwa ulinzi mathubuti dhidi ya Spurs kabla ya Divock Origi kupigilia msumari wa pili dakika mbili kabla ya mechi kumalizika.

Van Dijk ametwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Kulipwa wa Mwaka Ligi Kuu England, PFA kwa msimu huu wa 2018-19 na anapewa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachezaji watakaotwaa Ballon d'Or baada ya kiwango chake bora Jumamosi.

Hata hivyo, nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi, alisema ni lazima kuwapo na mgombea mmoja tu.

"Nadhani Messi ni mchezaji bora duniani," aliwaambia wanahabari. "Anastahili hili kwa kuwa bado anacheza, hivyo Ballon d'Or si kitu ambacho ninakiwazia. Kama itatokea ni wazi nitaichukua, lakini sidhani kama kuna [nafasi] yeyote.

"Bado ni mchezaji bora duniani. Haijalishi kama hayupo katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Alisson alionyesha kiwango cha kuvutia kwa kuokoa michomo muhimu katika kipindi cha pili na kuisaidia Liverpool kupata ushindi, ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kufungwa mabao 3-1 na Real Madrid kwenye mechi ya fainali ya michuano hiyo na lawama kumwendea kipa Loris Karius aliyefanya makosa ya kizembe.

Van Dijk, ingawa, hadhani kwamba mabadiliko ya kipa ni nguzo ya mafanikio yao kipindi hiki.

"Siyo tofauti kuu," alisema. "Soka si kuhusu mchezaji mmoja. Tunashinda pamoja, tunapoteza pamoja.

"Ali alikuwapo pale kutuokoa na michomo kadhaa kutoka kwa Son [Heung-min] na kila mmoja alikuwa akijaribu kufanya kidogo kwa timu.

"Katika kipindi cha pili tulipaki basi kidogo, waliongeza presha kwetu, ilionekana hatari kidogo - inatokea katika mechi. Lakini tulijiandaa kwa hilo, unajua kuna wakati katika mechi unakuwa na matatizo. "

## KWA UFUPI

### INTER YAMFUATA LUKAKU
Inter Milan inamtaka mshambuliaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 26, lakini Manchester United inamdhaminisha na pauni milioni 62. ***(Sportmediaset - in Italian)***

### SARRI KUANZA NA TRIPPIER JUVE
BEKI wa kulia wa Tottenham na England, Kieran Trippier, 28, atakuwa usajili wa kwanza kwa Maurizio Sarri atakapotua Juventus, kama kocha huyo wa Chelsea ataamua kurudi Italia. ***(Star)***

### POCHETTINO KUWEZESHWA SOKONI
KOCHA wa Spurs, Mauricio Pochettino anajiandaa kupewa fungu analohitaji kutoka bodi ya klabu hiyo- na ofa iliyokataliwa kwa kiungo wa Real Betis, Muargentina Giovani lo Celso, 23, na kiungo wa Lyon, Tanguy Ndombele, 22. Pia wanamtaka straika wa Celta Vigo, Muuruguay, Maxi Gomez na winga wa Fulham, Ryan Sessegnon, 19. ***(Mirror)***

### BAINES APEWA MWAKA EVERTON
Everton inatumai beki wao wa kushoto, Muingereza Leighton Baines, 34, atakubali ofa mpya ya miezi 12. ***(Liverpool Echo)***

### KOEMAN AIKATALIA BARCELONA
KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman, amesema hawezi kuacha majukumu yake na kwenda kuinoa Barcelona, endapo mabingwa hao wa Hispania wataamua kumtimua Ernesto Valverde. ***(De Telegraaf - in Dutch)***

### VAN GAAL AMPELEKA DE LIGT CITY
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal amesema beki wa Ajax, Mholanzi Matthijs de Ligt, 19, anapaswa kujiunga na Manchester City. ***(Manchester Evening News)***

### SHAQIRI KUKOMAA LIVERPOOL
MSHAMBULIAJI wa Uswisi, Xherdan Shaqiri, 27, anataka kubaki na kupigania namba Liverpool, licha ya kuwapo kwa tetesi kuhusu mustakabali wake wa baadaye klabuni hapo. ***(Express)***

### EVERTON YAMTAKA UNDER
Everton imetoa ofa ya pauni milioni 24 kwa winga wa Roma na Uturuki, Cengiz Under, 21. ***(Star)***

### RICHARLISON AKUNWA NA BARCA
MSHAMBULIAJI wa Everton, Mbrazil Richarlison, 22, amesema amepagawa na taarifa zinazomhusisha na kutakiwa na Manchester United pamoja na Barcelona. ***(Teamtalk)***

### MORENO AZIDI KUNUKIA BARCA
UWEZEKANO wa mshambuliaji Mhispania Rodrigo Moreno, 28, kujiunga na Barcelona akitokea Valencia umeongezeka kwa kiasi kikubwa. ***(Sport - in Spanish)***

### BENITEZ ATEGA WAWILI NEWCASTLE
KOCHA wa Newcastle, Rafael Benitez ameweka mitego yake miwili ya usajili kama Bin Zayed Group litafanikiwa kuinunua klabu hiyo - Mshambuliaji wa Venezuela, Jan Hurtado, 19, anayeichezea Klabu ya Gimnasia La Plata ya Argentina na kipa wa Paris St-Germain, Mjerumani Kevin Trapp, 28, ndio anaowawinda. ***(Express)***

### STROOTMAN AFUNGUKA KUUZWA
KIUNGO Mholanzi Kevin Strootman, 29, amesema Marseille inataka kumuuza. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***



## HABARI MICHEZO

# MAKONDA AGAWA FEDHA SIMBA, KUHAMIA YANGA

**Na Somoe Ng'itu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewataka wachezaji wa Simba kuendelea kujituma ili waweze kulinda heshima ya klabu yao katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mbalimbali ya kimataifa ambayo watashiriki.

Makonda alisema hayo jana kabla ya kukabidhi zawadi za fedha ambazo aliahidi kuwapatia wachezaji wa timu hiyo walioshinda tuzo za "Mo Simba 2019" zilizofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

Kiongozi huyo alisema kuwa lengo la kutoa zawadi hizo ni kuheshimu mchango wa wachezaji hao na kuwahamasisha wafanye vema katika msimu ujao, ili kuifanya Simba iendelee kupata matokeo mazuri.

Alisema pia anampongeza Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohammed 'MO' Dewji kwa kuandaa tuzo hizo na kuzitaka klabu nyingine kuiga mfano huo kwa sababu zinasaidia kuhamasisha wachezaji kupambana na hatimaye kufanya vema katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki.

"Wachezaji hawa wamefanya mashabiki wawe na imani nao, wamefanya Watanzania wapende kuja uwanjani kuiangalia timu, nawaomba 'spidi' hii na mwenendo huu mliokuwa nao, muuendeleze, mfanye vizuri zaidi ili kuhakikisha heshima ya Simba haishuki," alisema Makonda.

Wachezaji waliopata zawadi hiyo ya fedha jana ni pamoja na golikipa Aishi Manula ambaye alipewa Sh. milioni 10, huku nyota wengine walipokea Sh. milioni moja ni pamoja na Erasto Nyoni, James Kotei, John Bocco, Rashid Juma, Meddie Kagere na Clatous Chama.

Hata hivyo, Makonda jana alitangaza kuongeza zawadi kwa Mchezaji Bora Mwanamke wa Simba Queens, Mwanahamisi Omary ambaye sasa atampa Sh. milioni mbili badala ya Sh. milioni moja ambayo aliahidi wiki iliyopita.

"Nimeamua kumwongezea Mwanahamisi zawadi kwa sababu ni mwanamke pekee, amekuwa mfano wa kuigwa kwa wengine, hii itawasaidia kuhamasisha wachezaji wengine wanaochipukia," alisema Makonda.

Alizitaka klabu nyingine kuiga mfano wa tuzo hizo na kuahidi atahudhuria katika harambee ya Yanga itakayofanyika Juni 15, mwaka huu kwa sababu anaamini kufanya vema kwa klabu hizi kunasaidia uchumi wa Halmashauri ya Temeke kuongezeka.

**...AMPONGEZA MANARA**

Makonda pia alimkabidhi Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, kitita cha Sh. milioni tatu kutokana na kutambua mchango wake wa kuhamasisha mashabiki kuhudhuria uwanjani katika mechi mbalimbali, hasa zile za Ligi ya Mabingwa Afrika ambazo timu hiyo ilicheza.

Zawadi hiyo haikutangazwa kabla na Makonda amesema kuwa Manara ameufanya mchezo wa soka sasa kupendwa zaidi kutokana na "mbwembwe" zake licha ya kuzomewa au kutukanwa wakati anatekeleza majukumu yake.

Manara alimshukuru Makonda kwa zawadi hiyo na kusema atagawana na wafanyakazi wenzake katika sekretarieti ya Simba, huku kiasi cha Sh. 500,000 atakitoa kwa Chama cha Walemavu Tanzania ili kusaidia changamoto walizonazo.

## Samatta kupewa mtaa D'Salaam

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa KRC Genk inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji na nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, anatarajiwa kupewa mtaa hapa jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Uamuzi wa Samatta kupewa mtaa unatokana na mafanikio mbalimbali ambayo ameyapata mshambuliaji huyo ambaye msimu ujao atashiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akizungumza jana jijini, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alisema maandalizi ya kumpa mtaa yako katika hatua za mwisho na itakuwa ni kwenye barabara ya lami.

Makonda alisema kuwa wanaamini uamuzi huo ni sehemu ya kumuenzi mshambuliaji huyo wa zamani wa Simba na African Lyon ambaye pia anatumika kama balozi wa utalii kwa kuitangaza nchi kimataifa.

"Ninatambua kutokana na kazi yake aliyoifanya huko, amefanikiwa kufanya mambo makubwa, tutamkabidhi rasmi mtaa ambao barabara yake itakuwa na lami safi, taa, hii itafanya aendelee kukumbukwa wakati wote," alisema Makonda.

Alieleza kuwa makabidhiano ya mtaa huo yatafanyika kabla ya kikosi cha Taifa Stars hakijasafiri kuelekea Misri kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) ambazo zitaanza kuchezwa baadaye mwezi huu.

Aliongeza kuwa serikali imejipanga kuwaenzi wanamichezo wote watakaopeperusha vema bendera ya Tanzania na watakaokuwa na maadili safi, kwa sababu hii inasaidia kuwajenga wanamichezo wanaochipukia.

Pia, Makonda alisema kuwa serikali haitasita kutoa adhabu kwa wanamichezo ambao watafanya vibaya na kuchafua jina la nchi.

Wakati huo huo, Makonda, alisema kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E), wako katika hatua nzuri za kujenga uwanja wa michezo pamoja na kujenga ukumbi wa kisasa kwenye eneo la Tanganyika Packers, Kawe.




Mmoja kati ya washindi wa Jackpot bonasi, Mgaya Manandi (kushoto), akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 11.9 na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13. **PICHA: SPORTPESA**

# SportPesa haipoi, yagawa Smartphone 24

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanikisha ziara ya Klabu ya Sevilla nchini kwa kushirikiana na waendeshaji wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya Michezo ya SportPesa Tanzania, imedhihirisha kwamba "haipoi" kufuatia kugawa simu za kisasa za mkononi (Smartphone) 24 kwa Watanzania mbalimbali walioshinda kupitia Promosheni ya "Usibahatishe Cheza na SportPesa".

Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, akiwatangaza washindi hao jana, alisema bado wanaendelea kuwafaidisha Watanzania kupitia michezo mbalimbali ya kubahatisha wanayoendesha.

"Huu ni mwendelezo wa promosheni yetu tuliyoizindua wakati wa maandalizi ya ziara ya timu ya Sevilla ya Hispania ambapo mbali ya zawadi za simu, pia tulitoa zawadi za tiketi kwa washindi 45 na kuona mechi ya Simba na Sevilla huku watano wakishinda tiketi za VVIP na kulipiwa malazi, usafiri na chakula siku ya mechi hiyo," alisema Tarimba.

Tarimba alisema droo za kuwapata washindi wa Smartphone zinafanyika kila Jumatano kwa wiki 15, hivyo kuwa na jumla ya washindi wa 'simu janja' za kisasa Smartphone 200, tiketi 45 za mechi ya Simba dhidi ya Sevilla FC iliyochezwa Mei 23, mwaka huu na Sevilla kuibuka na ushindi wa mabao 5-4 na tiketi 10 za mchezo wa Kariobangi Sharks na Everton ya England utakaochezwa nchini Kenya Julai mwaka huu.

Aidha, Tarimba aliwataja walioibuka na ushindi katika droo hiyo kuwa ni Amran Samwel Mwanga, Jimmy Joseph, Frank Paulo, Juma Issa, Tiblus Dominik, Kassim Mbaga (kutoka Dar es Salaam), Sebastian Mathias, Emmanuel Adebayor (Mwanza), Omary Mohammed, Yahaya Kindenge (Morogoro), Aliehas Butwah, Yohana Malimi (Geita), Hawa Ramadhani, Hemed Mussa (Tanga) na Juma Hamisi kutoka mkoani Singida.

Wengine ni Sylvester Myoka (Songea), Raphael Philimon, Festo Mgasa (Arusha), Damian Warwa (Simyu), Lucas Mzalinga (Tabora), Alex Baynic (Dodoma), Anthony Mwembe, Ibrahim Swallo (Njombe) na Jadil Jena anayetokea mkoani Mtwara.

# Michezo

Jumanne Juni 4, 2019

Nipashe



## Messi ndiye atatwaa Ballon d'Or - Van Dijk

HABARI UK 30

MAFURIKO...




Mji wa Liverpool ukiwa umefurika maelfu ya mashabiki wa timu hiyo waliojitokeza kusherehekea mitaani jana, baada ya kurejea na Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya ililoshinda Jumamosi baada ya kuifunga Tottenham kwa mabao 2-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Wanda Metropolitano jijini Madrid, Hispania. Wachezaji walikuwa katika gari ya wazi na kombe lao. **PICHA: DAILY MAIL**

# Afcon yamkataa Kapombe, aumia

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI mshambuliaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), John Bocco, amewataka wadau wa soka nchini kukiamini kikosi cha timu hiyo ambacho kinajiandaa na fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), beki wa kulia, Shomary Kapombe ameumia tena akiwa na kikosi hicho.

Awali Kapombe aliumia akiwa katika kikosi cha Stars kilipokuwa nchini Lesotho mwaka jana na majeraha hayo yalimfanya akae nje kwa muda mrefu na kushindwa kuitumikia ipasavyo klabu yake ya Simba iliyomrejesha akitokea Azam FC.

Meneja wa Stars, Danny Msangi, aliliambia gazeti hili jana kuwa Kapombe alijitonesha mwenyewe juzi wakati akifanya mazoezi yake binafsi.

"Ni kweli ameumia, amejitonesha mwenyewe akiwa hotelini wakati akiendelea na programu zake binafsi za mazoezi, leo (jana) hata mazoezini hajatokea kabisa," alisema kwa kifupi meneja huyo.

Akizungumza baada ya mazoezi ya jana asubuhi, Bocco, alisema kuwa kila mchezaji anataka kufanya vizuri kwa sababu wanafahamu ni nafasi nyingine ya kujitangaza kimataifa.

Bocco alisema: "Mazoezi yanakwenda vizuri, tunajua huko mambo yatakuwa si rahisi, ila mpira una matokeo mazuri na vile vile una matokeo yanayoumiza, tunajiandaa ili twende tukapambane, hatuna wasiwasi kwa sababu wote tuna nafasi sawa."

Naye beki wa kushoto wa timu hiyo, Gadiel Michael anayetokea Yanga, alisema: "Kupata nafasi hii kwangu ni jambo ambalo lilikuwa ninaliwaza sana, ni ndoto ambayo nilikuwa nayo kwa muda mrefu, tutaenda huko kupambana kwa sababu tunajua ni fursa nyingine ya kujiuza, mawakala na watu mbalimbali watakuwapo huko kufuatilia wachezaji."

# YANGA YAIGARAGAZA SIMBA USAJILI NYOTA

**Yanasa wakali waliokuwa wakiwaniwa Msimbazi, akiwamo Mayanga na...**

**Na Somoe Ng'itu**

KATIKA kuimarisha kikosi chake ili kiweze kurejesha makali yake msimu ujao, Yanga imewazidi kete watani zao mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kwa kumsajili mshambuliaji kutoka Ndanda FC ya Mtwara, Vitalis Mayanga na golikipa, Farouk Shigalo kutoka Bandari ya Kenya.

Simba ilikuwa katika rada za kutaka kumsajili Mayanga baada ya kuonyesha kiwango kizuri katika mzunguko wa kwanza wa msimu uliomalizika, lakini kabla ya kukamilisha mchakato huo, tayari Yanga yenye uongozi mpya, imefanikiwa kunasa saini ya mshambuliaji huyo.

Taarifa kutoka Yanga, zinaeleza kuwa imemsajili mshambuliaji huyo kwa kumpa mkataba wa miaka miwili baada ya kukamilisha mazungumzo na nyota huyo kuridhia kujiunga na klabu hiyo inayofundishwa na Kocha Mwinyi Zahera kutoka DR Congo.

**Habari zaidi zinaeleza kuwa Yanga imeendelea kujiweka katika nafasi nzuri kwa kumsajili Shigalo, ambaye alikuwa anaichezea klabu hiyo ya Ligi Kuu Kenya pamoja na Timu ya Taifa ya Kenya (Harambee Stars) kwa kumpa mkataba wa miaka miwili.**

Kiongozi mmoja wa klabu hiyo (jina tunalihifadhi), aliliambia gazeti hili jana kuwa klabu yake imewasajili Mayanga ambaye alikuwa amemaliza mkataba na Ndanda pamoja na Shigalo kama ambavyo kocha wao, Zahera alivyopendekeza katika ripoti yake. "Ndio, tumemsajili kama mchezaji huru, mkataba wake na Ndanda FC umeshamalizika, sasa rasmi Mayanga ni mchezaji wa Yanga, amesaini miaka miwili," alisema kwa kifupi kiongozi huyo.

Yanga ilianza kumfuatilia mshambuliaji huyo katika kipindi cha dirisha dogo mwaka jana, lakini mchakato wa kumsajili ulishindwa kukamilika kirahisi kutokana na nyota huyo kubanwa na mkataba wake. Msimu uliomalizika Yanga imemaliza katika nafasi ya pili nyuma ya mabingwa Simba, huku pia ikipoteza tiketi nyingine ya kushiriki mashindano ya kimataifa baada ya kukubali kutolewa katika hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la FA na Lipuli ya Iringa.

Hata hivyo, bado Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), halijafungua rasmi dirisha la usajili wa wachezaji kwa ajili ya Ligi Kuu Bara na Ligi Daraja la Kwanza msimu ujao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >